# UKANDAMIZAJI WA JAMII UNAVYODHIHIRIKA KATIKA UANDISHI WA CLARA MOMANYI NA SHEILA ALI RYANGA

**NA**

**NYAMWEYA OMARI SAMWEL**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI, KATIKA IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**CHUO KIKUU CHA MOI**

**AGOSTI, 2018**

# IKIRARI

Tasnifu hii ni yangu na haijawahi kuwasilishwa popote pale katika shughuli yoyote ile wala kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote. Ni makosa na hatia kutoa nakala ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi au kutoka kwa Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret.

………………………. ……….………………….

**Nyamweya Omari S.** Tarehe

**SASS/PGK/04/12**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa kutahiniwa kwa ridhaa yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret.

……………………… ……….………………….

**Dkt. Makoti Vifu** Tarehe

Idara ya Isimu na Lugha

Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii,

Chuo Kikuu cha Machakos,

**MACHAKOS**.

……………………………………….. …………………………..

**Dkt. Kandagor Mosol** Tarehe

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii,

Chuo Kikuu, Moi,

**ELDORET**.

# TABARUKU

Kazi hii naitabarukia wazazi wangu wapendwa; Mzee Omari na Mama Moraa na ndugu zangu Nyabera, Mititi na Nyaboke, na, mjomba wangu Seki Mititi.

## SHUKURANI

Ningependa, kwa dhati, kuwashukuru wapenzi wa lugha hii teule ya Kiswahili; wahadhiri wote waliohakikisha hamu yangu ya Kiswahili inaongezeka. Wasimamizi wangu Dkt Vifu Saidi Makoti na Dkt Kandagor Mosol, shukran. Mliniongoza kwa kila hatua ya utafiti wangu.

Shangazi yangu Bi Catherine Omare, mjombangu Seki Mititi, mmekuwa welekezi wangu wa karibu katika maswala ya kiakademia. Mungu awabariki. Mzee Justus Omari, bibiye Annah Moraa ambaye pia ni mamangu mzazi, ndugu zangu wapendwa Nyabera Omari, Mititi na Nyaboke; shukran zangu za dhati pia mzipokee. Heshima zisizo kifani zimwendee Maulana. Kwako shukran hazitoshi.

Wote walionifaa kwa njia yoyote ile, pokeeni shukran zangu na Mungu awazidishie neema.

# IKISIRI

Waandishi wanawake wameonyeshwa kama wanaondika kuhusu unyanyasaji wa wanawake pekee hata ikiwa mawanda ya kazi yao ni mapana. Pia, watafiti wengi wameguzia swala la ukandamizaji wa wanawake bila kuzungumzia wanajamii wanaokandamizwa. Utafiti huu ulichunguza usawiri wa wanaokandamizwa katika jamii na wanajamii kulingana na jicho la mwanamke: yaani jinsi waandishi wanawake wanavyowasawiri. Katika kuuendeleza na kuuchanganua zaidi, nilitumia riwaya mbili zilizoandikwa na waandishi wanawake: *Nakuruto* (2009) iliyoandikwa na Clara Momanyi na *Dago wa Munje* (2008) iliyoandikwa na Sheila Ali Ryanga. Riwaya hizi ziliweka wazi jinsi wanawake wanavyowaumba waliotengwa na kukandamizwa miongoni mwa wanajamii. Utafiti huu umebainisha waliotengwa ni akina nani kwa minajili ya kuwatambua wanavyosawiriwa katika riwaya hizi na pia katika jamii. Nadharia ya Jinsia-Hakiki ilitumika kuongoza utafiti huu. Nadharia hii iliasisiwa na Elaine Showalter na ilitokana na nadharia ya ufeministi. Nadharia ya Jinsia-Hakiki inanuia kutofautisha waandishi wanawake na waandishi wanaume. Nadharia hii inadai kuwa waandishi wanawake hushughulikia mambo ya kijamii zaidi tofauti na yale yanayoshughulikiwa na waandishi wanaume. Carter, akichangia kuhusu mihimili ya nadharia hii, anasema kuwa waandishi wanawake huandika kuhusu mada ambazo zimeepukwa na waandishi wanaume. Aidha anasema kuwa kuna tofauti kubwa kati ya waandishi wanaume na waandishi wanawake katika kiwango cha maudhui na hata jinsi ya kusawiri wahusika. Tumetumia nadharia hii katika kuangalia jinsi waandishi wa kike wanawasawiri waliotengwa katika jamii na jinsi wanawasuluhishia matatizo yanayowakumba. Utafiti huu si linganishi. Utafiti huu ulitumia sampuli ya kimaksudi katika kupata data ambayo tuliishughulikia kuuendeleza utafiti. Tumewasilisha data kwa njia ya maandishi. Pia utafiti huu umechanganua jinsi waandishi wanawake wanavyowasawiri wanajamii wanaokandamizwa katika kazi zao za kifasihi mintarafu waandishi Clara Momanyi na Sheila Ali Ryanga; wakiwa ni waandishi wa kutoka Kenya. Waandishi wanawake wamepanua masuala wanayoyashughulikia katika kazi zao za kifasihi. Wanajamii wanawake kwa wanaume wanakandamizwa japo kwa viwango tofauti. Utafiti huu utasaidia kuwaheshimu waliokandamizwa na jamii na pia utawafaa wanafunzi, wahadhiri na wahakiki wa fasihi kuelewa zaidi kuhakiki kazi za fasihi zilizoandikwa na waandishi wanawake. Utafiti zaidi unafaa kufanywa kwa kazi tofauti za waandishi wanawake wengine.

## ABSTRACT

Women writers have always been depicted to only write about women oppression even when their works' scope is wide. Also, many researchers have examined women oppression without specifically looking at how society members are oppressed in literary works. This research investigated the portrayal of the oppressed in the society from women writers' perspective. In undertaking this research, two Swahili novels were used. These novels were written by women writers. *Nakuruto* (2009) has been written by Clara Momanyi while *Dago wa Munje* (2008) has been written by Sheila Ali Ryanga. These novels were used in critiquing the way women writers portray the oppressed in the society. This research sought to unearth who exactly the oppressed are among members of the society and how they are viewed by the other members of the society. The gynocriticism theory was used for purposes of carrying out this research. The theory was coined by Elaine Showalter and it emanated from the feminist theory. This theory seeks to differentiate between women writers and men writers. The gynocriticism theory claims that women writers concentrate and write more on different matters affecting the society than those written by men writers. Carter contributes on the tenets of this theory and says that women writers venture into types of writings which men writers have shied from. He adds that there is a big difference between women and men writers thematic-wise and in characterisation. We used this theory in evaluating how a woman writer portrays the oppressed in the society and how she resolves their problems. This research was library based. We used deliberate sampling when collecting data. The research aimed at analysing how women writers portray the oppressed in the society in their works with reference to writers Clara Momanyi and Sheila Ali Ryanga: both being Kenyan women writers. This research clearly exposes who in the society are oppressed and how they are oppressed according to the two novels. Women writers have expanded the issues tackled in their literary works. Both women and men are oppressed in different levels. This research will help literature students, lecturers and literary critics have a better understanding on how to give an objective and balanced critique of any literature written by women. More research can be done on the how other Kiswahili women writers portray the oppressed in the society in their literary works.

# YALIYOMO

IKIRARI .......... ii
TABARUKU .......... iii
SHUKURANI .......... iv
IKISIRI .......... v
ABSTRACT .......... vi
YALIYOMO .......... vii
**SURA YA KWANZA .......... 1**
**MISINGI YA UTAFITI .......... 1**
1.0 Utangulizi .......... 1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti .......... 1
1.2 Suala la Utafiti .......... 2
1.3 Malengo ya Utafiti .......... 3
1.4 Nadharia Tete .......... 3
1.5 Sababu ya Kuchagua Mada .......... 3
1.6 Umuhimu wa Utafiti .......... 5
1.7 Upeo wa Utafiti .......... 5
1.8 Misingi ya Kinadharia .......... 7
1.9 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada .......... 9
1.10 Mbinu za Utafiti .......... 15
1.10.1 Sampuli .......... 16
1.10.2 Ukusanyaji data .......... 16
1.10.3 Vifaa vya ukusanyaji data .......... 16
1.10.4 Uchanganuzi wa data .......... 17
**SURA YA PILI .......... 18**
**HISTORIA YA CLARA MOMANYI NA SHEILA RYANGA NA KAZI ZAO .......... 18**
2.0 Utangulizi .......... 18
2.1 Waandishi Wanawake .......... 18
2.1.1 Clara Momanyi .......... 19
2.1.1.1 Ngome ya Nafsi (2004) .......... 19
2.1.1.2 Tumaini (2005) .......... 21
2.1.1.3 Nakuruto (2009) .......... 23
2.1.2 Sheila Ali Ryanga .......... 24

2.1.2.1 Dago wa Munje (2008)....................25
2.2 Hitimisho....................27
**SURA YA TATU....................28**
**UKANDAMIZAJI WA JAMII KAMA UNAVYODHIHIRIKA KATIKA *DAGO WA MUNJE* ....................28**
3.0 Utangulizi....................28
3.1 Mielekeo ya Ukandamizaji....................28
3.1.1 Ukandamizaji wa Watoto Kutoka kwa Watu Wazima....................29
3.1.1.1 Ukandamizaji wa Walimu kwa Watoto....................30
3.1.1.2 Ukandamizaji wa Wazazi kwa Watoto....................33
3.1.2 Ukandamizaji Baina ya Watoto....................36
3.1.3 Ukandamizaji wa Nafsi....................39
3.1.4 Ukandamizaji wa Mwanamke....................43
3.2 Suluhisho la Ukandamizaji....................44
3.2.1 Suluhu Kutoka kwa Watoto....................44
3.2.2 Suluhu Kutoka kwa Watu Wazima....................45
3.2.2.1 Mama....................45
3.2.2.2 Baba....................46
3.2.2.3 Mwalimu Sifa....................47
3.2.3 Utambuzi wa Nafsi....................48
3.3 Hitimisho....................49
**SURA YA NNE....................50**
**UKANDAMIZAJI WA JAMII UNAVYODHIHIRIKA KATIKA *NAKURUTO*50**
4.0 Utangulizi....................50
4.1 Mielekeo ya Ukandamizaji....................50
4.1.1 Ukandamizaji dhidi ya ‘Wanaoota’....................51
4.1.2 Ukandamizaji wa Maazimio ya Vijana....................52
4.1.3 Ukandamizaji wa Mazingira....................59
4.1.3.1 Athari za ukandamizaji wa Mazingira....................61
4.1.4 Ukandamizaji kutoka kwa Serikali....................66
4.1.4.1 Unyakuzi wa Ardhi....................66
4.1.4.2 Ufisadi....................68
4.1.5 Ukandamizaji wa Mwanamke....................69
4.1.5.1 Ukandamizaji wa Mwanamke kutoka kwa Mwanamume....................70

4.1.5.2 Ukandamizaji wa Mwanamke kutoka kwa Mwanamke ........................... 71
4.1.6 Ukandamizaji wa Mwanajamii kutoka kwa Wakoloni .................................. 77
4.2 Suluhisho la Ukandamizaji ..................................................................... 79
4.2.1 Utambuzi wa Nafsi ............................................................................ 79
4.2.2 Mwanamke ........................................................................................ 81
4.2.3 Sera za Vijana ................................................................................... 82
4.3 Changamoto za Ukombozi ...................................................................... 83
4.3.1 Utengano wa Kimawazo Miongoni mwa Wanajamii .................................. 83
4.3.2 Ukosefu wa Ujuzi na Tajriba ............................................................... 84
4.4 Hitimisho ............................................................................................. 85
**SURA YA TANO ..................................................................................... 86**
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ................................................................ 86**
5.0 Utangulizi ............................................................................................ 86
5.1 Muhtasari wa Tasnifu ............................................................................ 86
5.2 Mchango wa utafiti ............................................................................... 86
5.3 Hitimisho ............................................................................................. 88
5.4 Mapendekezo ........................................................................................ 88
MAREJELEO ............................................................................................. 90

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii inaangazia usuli wa utafiti huu. Pia, katika sura hii, tutaangalia malengo ya utafiti, nadharia tete, sababu ya kuchagua mada, umuhimu wa utafiti, upeo wa utafiti na misingi ya kinadharia. Tutakuwa na sehemu ya yaliyoandikwa kuhusu mada, mbinu za utafiti, usampuli na vifaa vya kukusanya data na hati,maye uchanganuzi wa data.

## 1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Waandishi wanawake wamekuwa wakiandika kazi za kifasihi kwa muda, hivi kwamba wataalamu kadha wa kadha wamefanya tafiti kuhusu suala la jinsia na uandishi: ikiwa fasihi za mwandishi mwanamke ni tofauti na za mwandishi mwanamume. Eagleton (1986), anachangia kuhusu uandishi wa waandishi wanawake na kusema kuwa si lazima mwandishi mwanamke akiandika kazi yoyote ya fasihi iwe inaakisi hali zinazomkumba mwanamke. Anasema kuwa mwandishi huyu lazima awe amejitenga na hisia za kike anapoandika ili kazi yake iweze kuwa yakinifu. Eagleton anasema kuwa huenda tofauti bayana ikajitokeza kati ya mwandishi mwanamke na mwandishi mwanamume.

Barret katika Eagleton (1986) anasema kuwa kuna tofauti bayana kati ya mwandishi mwanamke na mwandishi mwanamume. Anaendelea na kudai kuwa uandishi wa kiume unabainishwa kuwa ule wa kawaida na pindi mwandishi mwanamke anapoandika basi kunakuwepo na ulinganisho kati ya jinsia hizi mbili. Lugha ya kiume ina uthabiti fulani ikilinganishwa na lugha ya kike ambayo inasheheni hisia nyingi. Hata hivyo waandishi wote wanawake hawafanani kiuandishi kwa sababu hali za kimazingira na kitamaduni zinazowakumba ni tofauti kulingana na wanakotoka waandishi hawa.

Waandishi wanawake hushughulikia matatizo yanayoikumba jamii kwa njia ya kipekee. Kwa njia hii pia, waandishi hawa huwasawiri waliokandamizwa na jamii na kuwakuza kwa njia inayosheheni mguso ili kuwavutia wasomaji. Wanaunda ulimwengu mpya katika fasihi wanazoandika na kutumia mbinu ambazo zinamteka msomaji.

Utafiti huu, kwa hivyo, ulichunguza suala hili la usawiri wa wanaokandamizwa kupitia kazi za kifasihi zilizoandikwa na waandishi wanawake. Kwa minajili ya utafiti huu basi, tumetumia kazi mbili za kifasihi zilizoandikwa na waandishi wanawake katika karne ya ishirini na moja; *Nakuruto* (Clara Momanyi: 2009) na *Dago wa Munje* (Sheila Ali Ryanga: 2008).

**1.2 Suala la Utafiti**

Matini za waandishi zinazozungumzia nafasi ya mwanamke katika jamii zimechapishwa na waandishi wengi. Pia, matini zilizoandikwa na wanawake zinazoitetea nafasi ya mwanamke katika jamii zimechapishwa kwa wingi. Mfano wa matini kama hizi ni *Mama Ee!* (Ari Katini Mwachofi: 1987), *Nguzo Mama,* (Peninah Muhando: 1982), *Tumaini, Nakuruto,* (Clara Momanyi: 2006, 2009) *Mwisho wa Kosa, Mali ya Maskini* (Zainabu Burhani: 1987, 1981). Matini hizi zinajikita katika kupigania haki za mwanamke na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutombagua mwanamke kwa misingi ya uana. Pia, tafiti nyingi zimefanywa kuhusu jinsi mwanamke anasawiriwa katika jamii katika jicho la mwandishi mwanamke na mwanamume. Kuna madai kuwa usawiri wa wahusika na matatizo katika jamii yanavyoshughulikiwa na waandishi wanawake ni tofauti na ule wa waandishi wanaume. Waandishi wanawake huzama ndani zaidi, kuandika masuala nyeti na kuwasawiri wahusika wao kwa njia ya kuteka hisia za wasomaji na kuwahurumia. Inachukuliwa kuwa wanaotengwa na

kukandamizwa na jamii zaidi ni wanawake. Lakini katika utafiti huu, tunachunguza, si wahusika wanawake tu, bali wahusika wote; wahusika waume na watoto, wanavyotengwa na kukandamizwa katika jamii. Kufuatia mtazamo huu, utafiti umechunguza na kuchanganua usawiri wa waliotengwa na kukandamizwa na jamii katika jicho la mwandishi mwanamke. Tumechunguza jinsi mwandishi mwanamke anamtazama aliyetengwa na jamii, jinsi anavyomtetea au kumsawiri na jinsi anapendekeza utatuzi wa matatizo yake. Tumechunguza jinsi Clara Momanyi na Sheila Ryanga wanavyozamia swala la ukandamizaji katika jamii.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu ni:

1. Kutathmini mwandishi mwanamke anavyolijadili swala la ukandamizaji na anavyowasawiri waliotengwa na jamii.
2. Kuchanganua jinsia ya kiume na kike zinatengwa kwa njia moja.
3. Kubainisha mwandishi mwanamke anavyopendekeza kusuluhisha matatizo ya waliotengwa.

## 1.4 Nadharia Tete

1. Mwandishi mwanamke huzamia kwa undani zaidi swala la ukandamizaji na unyanyasaji katika jamii.
2. Wanawake hukandamizwa na kutengwa zaidi ya wanajamii wengine.
3. Jinsia zote mbili zimetengwa na jamii japo kwa viwango tofauti kulingana na hali ya mazingira mwanajamii huyo aliyoko.

## 1.5 Sababu ya Kuchagua Mada

Matini nyingi za fasihi zimezungumzia maswala mengi yanayoathiri mwanajamii yakiwemo taasubi ya kiume au ukandamizaji wa mwanamke, ukandamizaji wa

mwanamume, uongozi mbaya, ufisadi, maadili mema, ndoa, na hata umuhimu wa elimu. *Kilio cha Haki* (Alamin Mazrui, 1981) ni tamthilia ambayo inazungumzia kunyanyaswa kwa mwanamke na wafanyakazi wenziwe na wengine. Nyingi ambazo zinazungumzia ugandamizaji wa jinsia ya kike zimeelemea sana upande wa mwanamke pekee bila ya kuwazungumzia wanajamii wengine wanaonyanyaswa vile vile. Kuna watalaamu wengi kwa mfano Mule (1991), Mnyetto (1994), Wegesa (1996), Mboya (1997), Momanyi (1998), Kisurulia (2000), Isiaho (2001), Kimani (2003) na Kobia (2004) ambao walishughulikia swala la ukandamizaji wa mwanamke pekee. Vipengele vya jinsia na uana vimeshughulikiwa na watafiti mbalimbali hivyo basi kuna umuhimu wa kushughulikia vipengele vingine vinavyowaathiri wanajamii.

Wandera (2002) anasema kuwa tafiti nyingi zimechunguza kuhusu maswala ya kike na kugundua kwamba mwanamke amenyanyaswa na jamii kidini, kitamaduni, kisiasa na hata kiuchumi. Anaendelea kusema kuwa, mwanamke amechukuliwa kama kiumbe duni na anapewa nafasi ya pili baada ya mwanamume.

Niliichagua mada hii ili kujaribu kuonyesha jinsi ambavyo hawa 'wengine' wanasawiriwa na waandishi wanawake kwani wametengwa kwa muda na kwa sababu ni uwanja ambao ni wachache sana walioutafitia. Pia, nimechagua waandishi wanawake ili kuchunguza iwapo nao (waandishi wanawake) huonyesha ukandamizaji wa jinsia tofauti na ile ya kike.

Utafiti huu unanuia kuweka wazi baadhi ya mateso wanajamii hawa hupitia na ni akina nani ambao wanawanyanyasa. Mwishowe, tuliangalia jinsi suluhisho linaweza kupatikana ili kukomesha matendo haya. Wanajamii wengi huteswa lakini wanaoweza kupata afueni ni wanawake ambao unyanyaswaji wao umezungumziwa sana na hata kufanyiwa tafiti nyingi. Hivyo basi, utafiti huu unazungumzia hawa wanajamii wengine

waliokandamizwa, kando na wanajamii wanawake, ambao hawazungumziwi bayana na waandishi. Mada hii ilichaguliwa kwa sababu tafiti nyingi huchunguza tu swala la mwanamke. Utafiti huu unapanua mtazamo wa kuangalia wanaokandamizwa wakiwemo wasiokuwa wanawake na waandishi wanawake wenyewe.

**1.6 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu utasaidia kutambua kuwa hatutengwi kwa misingi ya jinsia hivyo kupendekeza tiba faafu. Unaonyesha kuwa si wanawake tu waliotengwa na kukandamizwa bali hata wanaume na kwamba wote wanahitaji usaidizi. Unafaa zaidi wanafunzi wa fasihi wa Vyuo Vikuu na hata wahadhiri katika kupanua zaidi maarifa yao juu ya uhakiki wa fasihi hususan inayozungumzia wanajamii waliotengwa na pia katika kuelewa zaidi matini za fasihi zinazomtetea aliyetengwa. Pia, tasnifu hii ina maarifa ya kuhakiki kazi zilizoandikwa na waandishi wanawake kuhusu waliotengwa na jamii. Itawapa wanajamii fursa ya kuwaona waandishi wa kike wakichangia katika kuangazia maswala ya kijamii kwa jumla.

**1.7 Upeo wa Utafiti**

Kuna riwaya nyingi za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi wanaume zinazoonyesha kutengwa na kukandamizwa kwa mwanajamii. Mfano wa riwaya hizi ni *Utengano* (1985), *Kiza Katika Nuru* (1988), *Chozi la Mwanamke* (2009) za Said A. Mohamed, *Maisha Kitendawili* (2000) ya John Habwe na zingine, lakini nimeteua za waandishi wanawake tu, ili kuchunguza jinsi wanavyolishughulikia suala hili la unyanyasaji katika jamii. Ninaangazia waliotengwa na kukandamizwa kiuchumi, kielimu, kisaikolojia, na kitamaduni. Nimeangazia vipengele hivi kuonyesha jinsi unyanyapaa unaendelezwa miongoni mwa wanajamii. Kuna waandishi wengi wanawake ambao wametunga kazi za kifasihi katika lugha ya Kingereza na Kiswahili. Margaret Ogola, Marjorie Oludhe Macgoye, Goro wa Kamau, Micere Githae Mugo, Grace Ogot,

Muthoni Likimani, ni baadhi ya waandishi wanawake wa humu nchini Kenya walioandika kazi mbalimbali za kifasihi katika lugha ya Kingereza. Pia, kunao waandishi wanawake waliotumia lugha ya Kiswahili kutunga kazi za kifasihi: Mwana Kupona, Peninah Muhando, Rayya Timammy, Rebecca Nandwa, Pauline Kea Kyovi, Zainabu Burhani, Clara Momanyi na Sheila Ali Ryanga ni baadhi yao. Kwa ajili ya utafiti huu, nimetumia waandishi wanawake wawili, wazaliwa wa nchini Kenya, Clara Momanyi na Sheila Ali Ryanga. Waandishi hawa wametunga kazi zao katika lugha ya Kiswahili. Pia, wametunga kazi katika utanzu wa riwaya. Ingawa kunazo riwaya zingine ambazo zimeandikwa na Clara Momanyi na Sheila Ali Ryanga kuhusu waliotengwa katika jamii kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili, nimetumia riwaya *Nakuruto* na *Dago wa Munje* kuuendeleza utafiti wangu kwani kazi hizi zitatosha kubainisha malengo yangu ya utafiti. Uteuzi wa kazi hizi uliongozwa na vigezo hivi: riwaya hizi zinashughulikia unyanyasaji wa wanajamii wote kwa jumla na pia ni riwaya zilizoandikwa katika karne ya ishirini na moja. Nimetumia istilahi ‘waandishi wanawake’ wala sio ‘waandishi wa kike’ kwa sababu istilahi hiyo ya pili (waandishi wa kike) inaelekeza kuwepo na ‘ujinsia hasi’ dhidi ya waandishi hao. Istilahi ‘waandishi wanawake’, kwa maoni yangu, haina makali ya kijinsia kama ilivyo istilahi ‘waandishi wa kike’. Nimeshughulikia upekee wa kazi za waandishi wanawake bila ya kuangalia tofauti kati ya waandishi wanawake na waandishi wanaume. Kuna kazi nyingi za kifasihi zilizoaandikwa na waandishi wanawake kama *Zinduko* (Muhando: 1985), *Mali ya Maskini*, *Mwisho wa Kosa na Kipimo cha Mizani* (Burhani: 1981, 1987 na 2004), *Yanarudia Tena* Himid (2007) na nyingine ambazo sikuzitumia katika tasnifu hii kwa sababu upeo wangu ulibanwa katika waandishi wanawake wawili walioandika riwaya katika karne ya ishirini na moja na waliondika kazi zao katika kipindi cha kati yam waka 2000 na 2010.

**1.8 Misingi ya Kinadharia**

Utafiti huu umetumia nadharia ya Jinsia-Hakiki ambayo iliasisiwa na Elaine Showalter, mhakiki ambaye alikuwa ni mfeministi. Nadharia hii iliundwa ili kutumika kuhakiki kazi za kifasihi ambazo zimeandikwa na waandishi wanawake. Carter (2006) anamnukuu mwasisi huyu Showalter, na kusema kuwa alibuni istilahi hii ya jinsia-hakiki ili aweze kuchambua kazi za waandishi wanawake. Showalter anaainisha nadharia hii kwa kudai kuwa itasaidia kuchimbua historia ya kifasihi ya waandishi wanawake. Anaendelea kujadili kuwa kunayo tofauti bainifu kati ya uandishi wa wanawake na ule wa wanaume na kuwa mwandishi mwanamke hushughulikia matatizo ya kimsingi ambayo kwa njia moja au nyingine yameepukwa na waandishi wanaume. Nadharia ya jinsia-hakiki haitazami tu jinsia bali inaangazia mawazo ya ndani ya mwanamke. Kwa mujibu wa Showalter, hadi kufikia karne ya 20, utamaduni wa fasihi ya wanawake ulikuwa umejengeka kwa taswira na maadili yaliyotazamwa kwa jicho la kifeministi kutokana na wingi wa taasubi za kiume miongoni mwa wanajamii. Anaongeza kuwa iliibuka kutoka kwa udadisi-saiko wa Sigmund Freud.

Uchipuzi wa utamaduni wa nadharia hii ulitokana na nadharia ya kifeministi na umegawika katika awamu tatu. Awamu ya kwanza ilianza mwaka wa 1840 hadi mwaka wa 1880 ambayo Showalter anaiita ‘awamu ya kike’. Awamu hii inahusishwa na wahakiki George Eliot na Elizabeth Gaskell. Anadai kuwa wakati huu ulikuwa na waandishi wengi wa kiume na kuwa waandishi wa kike waliwekwa pembeni na hawakutakiwa kuandika kazi ambazo zilikuwa zinajihusisha na hali za kijamii zinazolingana na utamaduni wa jamii husika. Ni katika awamu hii ambapo mhakiki Marry Anne Evans alibadilisha jina lake akaanza kujiita ‘George Eliot’. Awamu ya pili ilihusishwa na wafeministi wakereketwa Olive Schreiner na Elizabeth Robins. Awamu hii ilianza mwaka wa 1880 hadi mwaka wa 1920 na ilijulikana kama ‘awamu ya

ufeministi’. Awamu ya mwisho na ya tatu ilihusisha Rebecca West na Katherine Mansfield na ilijulikana kama ‘awamu ya mwanamke’.

Carol (1986) anafafanua Jinsia-Hakiki kama nadharia ambayo inajaribu kumuinua mwandishi mwanamke na kumweka katika mizani moja na ile aliyowekwa mwandishi mwanamume. Anasema kuwa kumbainisha mwanamke chini ya utambuzi wa ‘waandishi wanawake’ ni kumdunisha kwani hakuna utambuzi wa ‘waandishi wanaume’. Uandishi wa kawaida, anadai, unachukuliwa kuwa ni wa ‘waandishi wanaume’ hata ikiwa haujatambuliwa hivyo. Carol anasema kuwa hakufai kuwa na utambuzi wa aina hii na kuwa nadharia hii itasaidia kuwapa waandishi wanawake uwezo na nguvu sawa na zile za waandishi wanaume.

Jacobus (1986) katika The Difference of View: Women Writing and Writing about Women’, anasema nadharia ya jinsia-hakiki ina uwezo mkubwa wa kuwasilisha maandishi ya kazi za waandishi wanawake kama yanayoendeleza furaha kuliko kutengwa kwa wale wanaonyanyaswa na jamii. Anasema kuwa katika vipindi hivi ambapo mwanamke amepata uhuru wa kujieleza na kujikomboa kutoka kunga za taasubi za kiume, mwandishi mwanamke anatumia uandishi wake kudhihirisha ushindi wa waliotengwa hata ikiwa wananyanyaswa. Uandishi huu unaonyesha kuja kwa matumaini k’wa wanawake katika jamii na wale waliotengwa miongoni mwa wanajamii.

Showalter (2000) katika makala ‘*Defining the Feminine: Gynocritics and the Woman’s Test’* anamrejelea Virginia Wolf anayedai kuwa uandishi wa wanawake huwa unasheheni ufeministi; hauwezi kuepuka ufeministi lakini ugumu wake hutokea wakati wa kufafanua ni nini ufeministi. Anasema kuwa uhakiki wa kifeministi umebadilika kutoka kuchambua kazi zote zilizoandikwa na waandishi wanawake na wa kiume hadi

kuanza kuhakiki kazi zilizoandikwa na waandishi wanawake. Showalter anasema kuwa kinyume na wahakiki wafeministi, wahakiki wa jinsia-hakiki wanapeana uwanja mpana zaidi wa uhakiki wa waandishi wanawake. Wahakiki hawa wanathamini mwandishi wa kazi ya kifasihi kuliko anachokiandika kwani wanaanza kwa kuangalia jinsia ya mwandishi wa kazi husika. Wao huhakiki kazi kwa jicho la mwanamke, wanaielewa kazi kupitia kwa jinsia ya mwandishi.

Kimsingi, nadharia hii ilitumika katika utafiti huu kuelewa jinsi waandishi hawa wanawake wanavyoandika na jinsi wanavyowasawiri wahusika hususan waliotengwa au kukandamizwa. Ilitusaidia kuonyesha upekee wa waandishi hawa katika kuumba ulimwengu wa kifasihi katika kazi wanaoziandika.

Nadharia ya Jinsia-Hakiki inajikita katika mihimili ifuatayo:

1. Historia ya fasihi ya waandishi wanawake.
2. Kushughulikia matatizo ya kimsingi ambayo waandishi wanaume huyaepuka.
3. Kuendeleza furaha zaidi kuliko swala la kutengwa.
4. Kudhihirisha ushindi wa waliotengwa hata kama wananyanyaswa.
5. Matumaini kwa wanawake na waliotengwa.

Mihimili hii iliniongoza katika kuuendeleza utafiti wangu na katika kuchanganua data.

**1.9 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

Schermerhorn (1960) anaeleza kuwa hakuna taifa lolote duniani ambalo halina watu waliotengwa. Anaendelea na kusema kuwa wanajamii waliotengwa huwa ni vikundi vidogo vidogo ambavyo vinawakilisha jamii na vinavyotengwa kimsingi kwa sababu ya tofauti za hali za kitamaduni. Anasema kuwa hali hizi za kitamaduni huwa ni za kidhahania na zilizojengeka tu kwa akili kidini, kijamii na hata kimawazo. Hivyo basi,

katika jamii kunakuwepo kutengwa kwa baadhi ya wanajamii na kutengwa huku kunazidi kadri mabadiliko ya kijamii yanavyozidi kufanyika.

Senkoro (1976) anaangazia jinsi utamaduni wa Wakoloni na wageni waliokuja Afrika Mashariki awali katika karne ya kumi na nane hadi mwanzo wa karne ya kumi na tisa ulivyoathiri kazi za kifasihi ya Kiswahili hususan riwaya. Anadai kuwa waandishi wengi waliathirika na utamaduni huo hivyo kukandamizwa na wakoloni na wageni hao. Ukandamizaji huu ni wa kipekee kwa sababu unajitokeza katika kiwango cha juu: kiwango cha waandishi wa kazi za kifasihi. Anendelea kusema kuwa, migogoro mingi inayokuzwa katika kazi za kifashi za Kiswahili imejikita katika mifumo mipya ya kuishi iliyoletwa na mfumo mpya wa jamii iliyoundwa kwa njia zilizoathiriwa na mambo ya utamaduni wa kigeni.

Carole (1986) anadai kuwa kumbainisha mwanamke kama mwandishi tofauti ni kumdunisha. Maoni yake kuhusu kazi za kifasihi ni kuwa, waandishi wote ni sawa na hakuna wa kiume au wa kike. Anajadili na kusema kuwa waandishi wote ni sawa na tunapowabainisha kwa misingi ya jinsia, tunawadunisha waandishi wanawake kwani hakuna waandishi wanaume. Waandishi ni waandishi tu.

Mule (1991) alichunguza swala la mwanamke katika baadhi ya tamthilia za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake. Alizichambua taswira za mwanamke ambazo zimejitokeza katika kila mojawapo ya tamthilia alizozichagua. Anadai kuwa wahakiki wengi waliojishughulisha na swala la kusawiriwa kwa mwanamke katika fasihi wametoa hoja kuwa taswira mbaya na za kupotosha tunazozipata katika fasihi zinatokana na hali kuwa waandishi wengi ni wanaume. Anasema kuwa waandishi hawa mara nyingi huwakilisha itikadi walizozipata katika jamii walimokuzwa. Alitalii ikiwa kuna tofauti yoyote ya jinsi waandishi wanawake na wanaume wanavyowasawiri

wahusika wao katika kazi wanazoandika. Katika utafiti huu wetu, hatukubainisha utofauti uliopo kati ya usawiri wa wanaokandamizwa katika jamii bali tulichunguza tu jinsi waandishi wanawake wanavyowasawiri wanaokandamizwa.

Mule (1991), akimrejelea Mbughuni (1982), anasema kuwa Mbughuni ameandika makala kuhusu taswira ya mwanamke katika maandishi ya riwaya ya Tanzania. Katika makala yake, Mbughuni anadai kuwa mwanamke anasawiriwa kuwili. Kwanza, mwanamke anasawiriwa na wanajamii kama mlaghai na mhalifu. Usawiri huu unalandana na taswira ya 'Hawaa' wa Bibilia ambaye anawakilisha uovu wote katika jamii; mchoyo, mlaghai, mvuruga amani, shetani na kadhalika. Taswira ya pili kulingana naye ni ile ya kumweka mwanamke jikoni huku akiwa ametawaliwa na mwanaume. Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza usawiri wa wahusika wa kike na mitizamo ya waandishi wa kike kama inavyodhihirika katika kazi hii. Utafiti huu wetu unatofautiana na huu kwani tulijishughulisha na kuchunguza waandishi wanawake wanavyowasawiri wanaokandamizwa kwa jumla bila ya kuegemea upande wa jinsia au uana. Aidha, Mule (1991) amemrejelea Chesaina (1987) na kusema kuwa Chesaina alihakiki jukumu la usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za Kiafrika. Kwake yeye, waandishi wanawake na waandishi wanaume wanatofautiana kwa kiasi kikubwa katika jinsi wanavyowasawiri wahusika wa kike. Utafiti wa Chesaina ni tofauti na wetu kwa sababu yeye alilinganisha na wetu si linganishi.

Katika kuangazia jinsi wanawake wanawasawiri waliotengwa, Wolf (1995) anasema kuwa wanawake wamekuzwa katika hali za kuwafanya wawe na umakini zaidi ya wanaume na wasipofanya hivyo watakuwa na hisia fulani ngeni kwani akili zao zimeumbwa kuwajali walio karibu nao. Hivyo basi, kwa mujibu wa Wolf, mwanamke anapoandika kazi yoyote ya fasihi huwa anaegemea pande zote mbili

(anayenyanyaswa na anayenyanyasa). Wolf pia anamnukuu Camille Paglia anayedai kuwa wanawake hawawezi kuwa wasanii wakuu kwa sababu hawana uasilia kamili, yaani wanategemea hali zinazowazunguka. Hatuelewi madai ya Camile juu ya utofauti wa uasilia na hali zinazowazunguka waandishi wanawake. Iwapo waandishi wanawake wanaandika hali zinazowazunguka, basi huu ni uasilia. Kwa hivyo madai haya kwetu ni potofu.

Wegesa (1996) ameangazia ukandamizaji wa mwanamke kabla na baada ya uhuru wa Mwafrika. Anapendekeza kuwa suluhisho la wanawake wanaokandamizwa litapatikana t'u ikiwa watapata elimu na kupata njia za heshima za kujitafutia riziki, na hivyo kujitegemea. Pia, Wegesa anapendekeza kuwa waandishi wa fasihi wanafaa wamsawiri mwanamke kama kiumbe ambaye anajitegemea na aliye na matumaini maishani.

Mboya (1997) amejadili mwanamke katika kumuumba upya mbele ya jicho la mwandishi Marjorie Oludhe McGoye katika riwaya zake *Murder in Majengo, Coming to Birth, The Present Moment* na *Homing In.* Mboya anamsawiri mwanamke kama kiumbe anayepitia changamoto zilizojengwa na mwanamume. Anaendelea kudai kuwa mwanamke amehukumiwa vibaya na historia ambayo anasema inamkandamiza asiweze kuonekana kama aliyeshiriki upiganiaji uhuru. Anajadili kuwa ni mwanamke amekandamizwa na wanajamii ambao wamejazwa na ubabedume kwa kuwaona wanawake kama wanajamii walio duni. Mboya anatamatisha akisema kuwa mwanamke anatambuliwa kama asiye na nguvu. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa hatuchunguzi mhusika mwanamke. Tulichunguza waandishi wanawake wanavyojadili swala la wanaokandamizwa katika jamii.

Ogbu (1998) alifanya utafiti wa wanafunzi waliotengwa ambapo alichunguza athari zinaoandamana na kutengwa huko katika masomo. Aligundua kuwa wale wanafunzi waliotengwa walifanya vibaya katika mitihani kwa sababu ya jinsi walivyonyanyaswa na wenzao. Utafiti huu uliangalia kutengwa kwa mwanajamii (mwanafunzi) katika uwanja wa elimu, wanawake kwa wanaume. Hakujikita katika jinsia moja. Sisi tulichunguza ukandamizaji wa mwanajamii sio tu chuoni bali pia anapoishi.

Katika kiwango cha kiuchumi-kidini pia, wanajamii huweza kutengwa. Zakaria (2001) alitafitia kuhusu kutengwa kwa wanawake Waislamu katika biashara. Katika utafiti huu, Zakaria aliwatafitia wanawake Waislamu ambao hawaruhusiwi kufanya biashara sokoni lakini wanaendeleza biashara kisirisiri mitaani wanakoishi. Aligundua kuwa wanawake hawa hupata faida zaidi ya wanawake ambao wana uhuru wa kuendeleza biashara zao sokoni. Wanawake hawa, anasema, wanaonekana kuwa ni 'vyombo' vya kuonewa huruma na haviwezi kuzalisha mali miongoni mwa jamii. Utafiti huu uligusia mwanamke kama aliyetengwa katika kiwango cha kidini na pia kiuchumi, lakini utafiti wetu ulichunguza jinsi mwandishi mwanamke anavyodhihirisha madhila yanayowakumba wanaotengwa katika jamii, wanawake kwa wanaume.

Momanyi (1998) alichunguza anavyosawiriwa mwanamke Mwislamu katika ushairi wa Kiswahili. Aliangalia jinsi watunzi wa mashairi wanavyomuumba mwanamke na mbona wanamuumba jinsi wanavyofanya. Alichambua tungo za washairi mbalimbali walioteuliwa ili kutathmini mwanamke anavyoumbwa katika ushairi huo.

Isiaho (2001) anadai kuwa mwanamke amepewa taswira mbili. Taswira ya kwanza ni ile inayomsawiri mwanamke kama kiumbe mwadilifu na mwongofu na taswira hasi zinazomsawiri kama kiumbe muovu na mchafuzi wa mazingira. Isiaho anajadili kuwa mwanamke hashirikishiwi katika shughuli za kiuchumi na za kijamii, swala

linalomfanya kutojisimamia na hivyo kuwa mwepesi kuny'anyaswa na wanajamii wengine. Anapendekeza suluhisho la kumkomboa mwanamke ni kumfunza mtoto msichana jinsi ya kukaa katika jamii na kuitumikia.

Kimani (2003) alishughulikia maudhui ya dhuluma dhidi ya wanawake kama mojawapo ya maudhui mengi yaliyoshughulikiwa na wahakiki. Alichunguza tanzu za riwaya na tamthilia pekee. Mtafiti huyu alitumia vitabu vinne ili kuendeleza uchunguzi wake: *Rosa Mistika, Maumbile si Huja, Mama Ee* na *Nguzo Mama.* Kimani alipendekeza utafiti zaidi uendelezwe kuhusu ukandamizaji wa mwanamume pia, kwani kuna visa kadhaa vya wanaume kudhulumiwa katika nyakati za sasa. Anaendelea kupendekeza kuwa uchunguzi huu unaweza kujikita katika kuchunguza kazi zilizoandikwa katika nyakati hizi ili kuona kama swala hili linajitokeza. Mapendekezo haya yamechangia katika kuuendeleza utafiti wetu.

Kobia (2004) anasema kuwa ukombozi wa mwanamke katika jamii za kiafrika hauwezi kupatikana bila kuihusisha jamii nzima, wanaume wakiwemo. Kobia anafafanua umoja unaohitajika ili kumkomboa mwanamke na jinsi ulivyo na umuhimu kwa wanajamii wote kwani mwanamke akikombolewa, basi jamii yote itakuwa huru. Anaendelea kusema kuwa "kumwelimisha mwanamke kuna ubora kwa kumfanya awafundishe watoto wake njuno bora na utamaduni ambao haumdhalilishi mwanamke. Kuelimisha mwanamke ni kuelimisha taifa zima kwa vile msichana atakuja kuwa mama atakayepata watoto, na atakayekuwa mwalimu wao wa kwanza ni yeye."

Wachira (2006) alishughulikia taswira ya mwanamke na inavyojitokeza katika nyimbo za kisasa za *rap*. Alihakiki tungo za wasanii wa kike na kiume ili kuchunguza zaidi kuhusu picha anayopewa mwanamke na wasanii hao wanaotumia mtindo wa kisasa wa

*rap*. Alipata kuwa wasanii wa nyimbo hizo hawafaulu kuchora picha ya mwanamke halisi anayestahili kuigwa katika jamii.

Noordin (2008) anagusia swala la waliotengwa kwa kutumia nadharia ya ufeministi wa Kiislamu katika fasihi ya Kiswahili. Katika makala hiyo, Noordin anasema kuwa mwanamke mwislamu alikuwa na haki sawa na mwanamume hasa katika kupata elimu kwa manufaa ya kibinafsi na kitaifa: Ufeministi wa Kiislamu ulijihusisha na mwamko wa wanawake kidini, kijamii na kitamaduni. Kupitia nadharia hii, Noordin anawapa waliotengwa kijinsia miongoni mwa Waislamu nguvu za kuweza kupewa nafasi sawa na ile wanayopewa wanaume. Anatumia mfano wa hadithi fupi – '*Uteuzi wa Moyoni'* – iliyoandikwa na Rayya Timmamy katika kuelezea matumizi ya nadharia hii.

Mawazo haya ya wahakiki na waandishi niliowataja yatanisaidia kutambua ni vipi haswa waliotengwa wanavyochukuliwa na wanajamii na pia jinsi wanavyoumbwa na waandishi wanawake. Tafiti hizi pia zitanisaidia kuuelewa upekee wa uandishi wa waandishi wanawake ili nitambue mbinu wanazozitumia kujenga ulimwengu wa fasihi wanaoumba wanapoandika.

**1.10 Mbinu za Utafiti**

Utafiti huu ulihakiki matini za kifasihi za Kiswahili na tulitumia mbinu tatu kuendeleza utafiti.

Nilitumia utafiti wa maktabani ambapo nilipitia majarida, vitabu, magazeti na matini mbalimbali ili kukusanya habari kuhusu utafiti wangu. Kusoma huku kulinipatia mawazo ya wahakiki na waandishi mbalimbali kuhusiana na mada ya utafiti. Vile vile, nilisoma maandishi yoyote juu ya riwaya nilizoteua katika utafiti huu na zingine zilizoandikwa na waandishi wanawake.

Mashauriano na wahadhiri na wanafunzi wa shahada ya kwanza, uzamili na uzamifu yalitumiwa kupata ufahamu mpana zaidi kuhusu kazi nilizoteua kutafitia. Pia niliingia kwenye tovuti zilizungumzia waandishi wanawake na maswala ya ukandamizaji katika jamii.

### 1.10.1 Sampuli

Riwaya hizi mbili: *Dago wa Munje* na *Nakuruto,* ziliteuliwa kupitia kwa usampuli wa kimaksudi. Riwaya hizi zimeandikwa na waandishi wanawake ambao ni wa humu nchini Kenya na wanaoandika katika lugha ya Kiswahili. Riwaya hizi zinaonyesha kuwa zina vipengele fulani vya waliotengwa na kukandamizwa na jamii, jinsi wanavyokombolewa na jinsi visa hivi vinatamatishwa. Riwaya hizi zimeteuliwa kwani waandishi hawa wana tajriba katika kazi za fasihi na walishawahi kufunza katika Vyuo Vikuu na shule za upili. Pia, riwaya hizi zilichaguliwa kwani ni za hivi punde, karne ya ishirini na moja. Aidha riwaya hizi zimejikita zaidi katika suala la ukandamizaji katika jamii zetu.

### 1.10.2 Ukusanyaji data

Data ilikusanywa kutoka kwa riwaya zilitoteuliwa: *Dago wa Munje* na *Nakuruto,* mtandao, na kutoka vitabu, tasnifu na makala maktabani.

### 1.10.3 Vifaa vya ukusanyaji data

Tulitumia kalamu, daftari, tarakilishi na kinyonyi katika kukusanya data zangu. Daftari na kalamu zilitumika kuandikia niliyoyasoma kutoka kwa vitabu mbalimbali. Tarakilishi ilitumika kuhifadhi makala nilizozitoa kwenye mtandao. Kinyonyaji kilitumika katika kubeba makala kutoka kwa tarakilishi moja hadi nyingine.

### 1.10.4 Uchanganuzi wa data

Data iliyochanganuliwa ilitokana na riwaya hizi mbili: *Nakuruto* na *Dago wa Munje.* Data hii ilichanganuliwa kimaelezo na kitakwimu. Ilichanganuliwa kwa kutumia mihimili ya nadharia ya Jinsia-Hakiki ambapo tulijaribu kutambua upekee wa mwandishi mwanamke kuhusu usawiri wa waliotengwa na wanaokandamizwa ulivyojitokeza katika riwaya zilizotafitiwa. Tuliratibu katika jedwali kwa asilimia (%) ni kwa kiwango gani kila riwaya ilizungumzia ukandamizaji wa mwanamke na ule usio wa mwanamke. Vile vile tulitumia maelezo kufafanua yale tuliyopata katika data. Data hii ilitusaidia kutathmini iwapo ni kweli kuwa waandishi wanawake huzungumzia maswala mengine.

# SURA YA PILI

# HISTORIA YA CLARA MOMANYI NA SHEILA RYANGA NA KAZI ZAO

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inaangazia historia za waandishi Clara Momanyi na Sheila Ali Ryanga na kazi mbalimbali walizoandika kutoka miaka ya sabini (1970). Ilichunguza viwango vya elimu vya waandishi hawa, tajriba zao katika uandishi wa kazi za fasihi kwa ujumla na kipengele kingine chochote kuhusu maisha yao. Pia, katika sura hii tumeangalia maudhui yaliyoangaziwa na waandishi hawa kwenye kazi hizo. Nimeangazia kazi zao za tamthilia na hadithi fupi zilizoandikwa katika lugha ya Kiswahili.

## 2.1 Waandishi Wanawake

Waandihi wanawake wamekuwa wakiwekwa pembeni katika utunzi wa kazi za fasihi hususan andishi (Jenner, 2010). Ijapokuwa ni wachache wametunga kazi za kifasihi, wengi wao wamechipuka miaka ya tisini (1990) na ndio wakati ambao kazi zao zilianza kuchapishwa. Miongoni mwa waandishi wanawake maarufu wa Kiswahili ni Mwana Lemba na Mwana Kupona (1830-1865). Waandishi hawa ni wanawake wa kwanza kutunga kazi za kifasihi (ushairi) wakitumia Kiswahili. Mwana Lemba ndiye anayedaiwa kuwa miongoni mwa waasisi wa kwanza wa fasihi ya Kiswahili. Aliishi katika kisiwa cha Pate na alitunga *Utenzi wa Siri L'Asirari* (1663) wenye beti mia tano na sitini na tatu (563). Ndio utenzi wa kale zaidi miongoni mwa ushairi wa Kiswahili. Mwana Kupona Binti Mshamu alitunga utenzi maarufu *Utenzi wa Mwana Kupona* (1858) wenye beti mia moja na mbili (102) kwa mujibu wa Allen (1972). "Utenzi huu ulitungwa na Mwanakupona Binti Mshamu kwa ajili ya binti yake aliyeitwa Mwana Hashima binti Mataka mwaka wa 1275 (Baada ya Kristo)": Mulokozi (1999:101). Mtunzi huyu pia anadai kwamba utungo huo ni mmojawapo wa tungo za kitamaduni na mawaidha za kipindi hicho.

Waandishi wengine wa kike wamejitokeza na kuandika riwaya, tamthilia, mashairi na hadithi fupi. Miongoni mwao ni; Peninah Mlama Muhando, Rayya Timammy, Rebecca Nandwa, Pauline Kea Kyovi, Zainabu Burhani, Clara Momanyi na Sheila Ali Ryanga.

### 2.1.1 Clara Momanyi

Clara Momanyi sasa hivi ni profesa na mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Katoliki, Nairobi. Ameandika kazi za kifasihi na kitaaluma kadha wa kadha zikiwemo: *Tumaini* (2009): *Ngome ya Nafsi* (2004), "The Effects of Persians on the Kiswahili Language" (2004), katika *The Guide, Journal of East Africa*, Vol.11 no. 11, Dec/Jan; "Swala la Uana katika Utafiti wa Fasihi ya Kiswahili" (2002) katika *Utafiti wa Kiswahili*, Kiswahili katika Karne ya Ishirini na Moja, (mh. n.w), 2002, "Nafasi ya Mwanamke katika Ushairi wa Shaaban Robert" (2001) *Kiswahili*, Vol.1.no.64, "Usawiri wa Wahusika wa kike katika Fasihi ya Kiswahili Baada ya 2000: Kuyumbisha Uhalisi", 2000, *Kiswahili* (2000) na "Nadharia ya Uchanganuzi Nafsia katika Mtazamo wa Kike na Uhakiki wa Kifasihi", 1996/97, *Kioo cha Lugha*, Vol. 2.

Kazi hizi zinazungumzia nyanja mbalimbali za maisha ya mwanajamii hususan unyanyasaji wa mwanajamii. Ni mmojawapo wa waandishi wa kike ambao wameweza kuandika kazi nyingi kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii.

Nilitumia kazi yake *Nakuruto* ili kupata mtazamo wake katika kuzungumzia wale wanaonyanyaswa katika jamii.

#### 2.1.1.1 Ngome ya Nafsi (2004)

*Ngome ya Nafsi* ni hadithi fupi inayoangazia nafasi ya mwanamke katika jamii hususan haki za mtoto wa kike.

Clara Momanyi anamuumba mhusika Naseko akiwa katika familia ambayo inathamini mali kuliko maisha ya mwanadamu. Mifugo wanaletwa kwao na hakuna anayethubutu kuuliza ni wa nini, hata mamake Naseko anaogopa kwa sababu ya ukali wa Mzee Mengo na utamaduni. Siku moja Naseko anaelekea mtoni kuteka maji. Hapo ndipo mpango wa babake unakamilika na ananyakuliwa na wavulana hadi kwa Mzee Sakaja. Babake, Mzee Mengo, anamwoza kwa Mzee Sakaja ambapo anatoroka na kukimbilia nyumba ya wasichana waliodhulumiwa. Bi. Tesi anamkaribisha kwa furaha na kumwambia kuwa hapo ndipo kwao kwa sasa; ambapo hakutakuwa na mtu atakayemsumbua. Kisa chenyewe kinaisha tukiwa tunaona haki inatendeka kwa Naseko lakini kwa 'wadhulumu' hatuambiwi hatua inayochukuliwa na serikali.

Hadithi yenyewe inamulika dhuluma dhidi ya mtoto wa kike na inadhihirisha waziwazi jinsi anavyoteswa na kunyimwa haki zake zikiwemo haki ya kupata elimu bora na ya kutoolewa akiwa na umri mdogo na kwa lazima na kunyimwa uhuru wa kujichagulia mchumba au mume. Mwandishi huyu anafaulu kuweka bayana dhuluma dhidi ya mwanamke na kuonyesha jinsi mwanamke ni adui wake mwenyewe. Mamake Naseko anashiriki kupanga ndoa ya mtoto wake na hata ingawa Clara anajaribu kumsawiri kama ambaye anaipinga kwa kiasi ndoa hiyo, kwa kiwango kikubwa ameruhusu hayo kumtendekea Naseko. Inawezekana ikiwa angeipinga kwa dhati ndoa hiyo, au basi angemuarifu Naseko mapema ili atoroke kabla siku hiyo ya kunyakuliwa haijafika. Mama Naseko naye, anakandamizwa na utamaduni kwamba baba ndiye kichwa na haulizwi kwa lolote afanyalo. Hangethubutu.

> Naseko aliacha kulia na kuvuta fikra ili ajue namna ya kupatoroka mahali pale. Hapa ndipo picha za matukio yaliyoandama kutoroshwa kwake zilipomjia akilini. Naam, sasa alielewa fika kwa nini wazee fulani walikuwa wakija nyumbani kwao mara kwa mara, kuongea na wazazi wake. Alielewa kwa nini ng'ombe na mbuzi walikuwa wakiletwa kwao jioni jioni na watu asiowafahamu.

> Kila alipomuuliza mamake kuhusu mifugo hao, mama mtu alimjulisha kuwa waliletwa hapo kwa muda tu ili mwenyewe apate nafasi ya kujenga zizi kubwa zaidi la kuwasitiri. (uk 104)

Mamake hakushughulika kumtahadharisha kuhusu yaliyokuwa yanamkodolea macho bali aliamua kutulia tuli kwa kumuogopa mumewe, Mzee Mengo.

Ni hadithi ya kifeministi kwani inapigania haki za wanawake na za mtoto wa kike. Inaonyesha jinsi watoto wa kike na wanawake kwa jumla hawana hiari ya kujichagulia au kufanya jambo: wanaamuliwa na wanaume.

**2.1.1.2 Tumaini (2005)**

Mwaka mmoja baadaye, alichapisha kazi nyingine ya fasihi aliyooiita *Tumaini*. Riwaya hii ya uhalisia inaangalia matukio ya mhusika msichana anayeitwa Tumaini. Vitushi vyote riwayani vinamzunguuka mhusika huyu anayetumika na mwandishi kuleta ukombozi wa mwanajamii msichana na kwa wanawake wote kwa jumla.

Clara anaanza kusimulia kisa chake kwa kutuonyesha Tumaini anavyohepa kwao nyumbani wakati wa asubuhi. Hapo hapo tunaonyeshwa ukatili wa Mzee Masumbuko, ambaye ni babake. Clara anamuua mwanamume kiutu ili iweze kuwa rahisi kwake kumsawiri mwanamume kama anayempinga mwanamke na anapinga maendeleo yake katika riwaya yote.

Mhusika Tumaini anazingirwa na hali ngumu ambazo hata kwa mtoto wa kiume bado zingelikuwa za changamoto kubwa lakini mwandishi anampa nguvu zaidi za kuweza kuzistahimili. Msichana huyu anaumbwa na uwezo zaidi ya msichana wa kawaida ili aweze kuwa mfano kwa wanajamii wengine: msichana mpya, wa jamii mpya iliyokombolewa. Anavuka vikwazo vingi maishani vikiwemo vya taasubi ya kiume

iliyomo kwa wanajamii wenzake, kuolewa kwa lazima, kupashwa tohara na hata kunyimwa karo ya shule ya sekondari.

> Hakuweza kufanya hivyo kwani maneno ya babake yalimgonga masikioni, yakamchoma moyoni mfano wa kisu chenye makali. Kero la uchungu lililokuwa kifuani mwake lilimchafyachafya, likamfanya kupukutika machozi kupukupu pale alipokaa. Aliwaza jinsi alivyojaribu kumshawishi babake ili aweze kuelewa dhamira yake lakini akawa haambiliki hasemezeki. Kushindana naye hakungefaa chochote, kwa hivyo akaamua kuchukua hatua aliyochukua ya kutoroka. (uk 5)

Taasubi ya kiume hapa inajitokeza bayana kwani babake Tumaini hamsikizi yeyote hata ikiwa ni yeye mwenyewe aliye na makosa. Daima anajiona yu sahihi na mwanamke hazungumzi mambo ya maana. Haya ni mambo ambayo hutokea katika jamii yetu ambapo mwanamke hawezi kutoa ushauri juu ya jambo zito katika familia au jamii.

Babake pia alijaribu kusitisha elimu yake na anataka aolewe baada ya kukamilisha masomo ya darasa la nane:

> Tumaini alikuwa amekamilisha darasa la saba katika shule ya msingi ya Kivulini, kijijini Mabuyuni. Hata hivyo, hakuwa na matumaini ya kuyabadilisha mawazo ya babake kuhusu kuendelea na masomo ya darasa la nane. Matumaini yake yalizidi kufifia babake alipoanza kufanya mipango ya kumpasha tohara…Wasichana wengi mle kijijini walipashwa tohara hata ingawa serikali ilikataza ukeketaji wa watoto wa kike. Tumaini alielewa pia kwamba idadi kubwa ya wale waliotahiriwa, ililazimishwa kuolewa mara moja. Ndoa za mapema na za lazima katika jamii hii lilikuwa jambo la kawaida. (uk 14-15)

Mjombake Shabani na mke wake Bi. Halima, wanafadhili elimu yake ya shule ya upili na anafuzu vyema na kufaulu kujiunga na Chuo Kikuu ambapo sasa ataenda kusomea kozi aliyokuwa anaipenda na kuitamani: ‘*Doctor of Medicine’.*

> “Nami naenda kusomea udaktari katika mawanda ya matibabu mbalimbali,” alitamka Tumaini. “*Doctor of Medicine! How great!”*
> (uk 155)

Alimweleza rafikiye wa utotoni Sifa, ambaye alikuwa ameitwa kusomea shahada ya udaktari, taaluma ya meno.

Kisa chote kinamzunguka binti Tumaini ambaye hatimaye anakuwa 'tumaini na mwanga' kwa wote wanaonyanyaswa hususan wasichana na hata wanawake. Kisa hiki kinapigania ukombozi wa mwanamke na Clara amevifinyanga vitushi kwa ustadi mkubwa katika kufanikisha dhamira hii ya ukombozi wa mwanamke. Clara ni mtetezi mkubwa wa haki za wanawake hapa nchini Kenya tukizingatia kazi zake za fasihi.

### 2.1.1.3 Nakuruto (2009)

Miaka minne baada ya kuchapishwa kwa riwaya ya *Tumaini*, Clara akachapisha riwaya nyingine anayoiita *Nakuruto*. Hii ndiyo riwaya ya mwisho ya Clara kufikia 2014 iliyochapishwa. Ni riwaya ya kuvutia ambayo inaunganisha dunia halisi na ile ya uhalisia mazingaombwe katika kujenga maudhui yake.

Mhusika Nakuruto anasukwa kama jasiri anayepitia hali ngumu za kimaisha japo hatimaye analeta ukombozi kwa wanajamii wote.

Kinyume na kazi zingine za Clara, hii inaleta upana wa maudhui anayoshughulikia Clara kwani inaangazia uchafuzi wa mazingira, kudorora kwa maadili ya jamii, haki za mwanamke, ukoloni mamboleo na hata swala la uongozi na uchumi. Kazi hii inalenga kufufua matarajio ya wanajamii waliokumbwa na shida mbalimbali zikiwemo ukosefu wa chakula. Kando na kumulika uhasama dhidi ya mwanamke, riwaya hii inahubiri ukombozi kwa wanajamii wote waliokuwa katika ngome mbalimbali za kimaisha.

> Nakuruto alimweleza mipango yake ya kuufifisha unyonyaji na kuwarudisha wanakijiji mali zao za asili, ukiwemo ule mgodi. Baada ya nasaha nyingi, Mfumwa alikubali shingo upande kwani alijua kuwa asipoungana na wenziwe, mambo huenda yangemharibikia. Alimuenzi Wellingtone kiasi cha kumpigia magoti. Uhusiano wake naye ulimfaidi. (uk 66)

Ndiyo riwaya tuliyoitafitia katika tasnifu hii.

### 2.1.2 Sheila Ali Ryanga

Profesa Charlotte Sheila Ali Ryanga ni mmojawapo wa wasomi wa kike nchini Kenya. Kwa sasa hivi ni mkurugenzi katika Chuo Kikuu cha Kimethodisti, Kenya, Bewa la Mombasa. Alifuzu kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi na shahada ya kwanza ya Falsafa katika Dini, Isimu na Lugha za Kiafrika mnamo mwaka wa 1977. Alijiunga na chuo hicho kusomea shahada ya uzamili katika Kiswahili. Miaka kumi na minane baadaye, mnamo mwaka wa 1995, alifuzu na shahada ya uzamifu kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Ameshawahi kushikilia nyadhifa mbalimbali katika taasisi za elimu na bodi mbalimbali humu nchini. Alianza kufunza Chuo cha Walimu cha Shanzu Mombasa, mwaka wa 1981 hadi 1982 kama mhadhiri. Kwa miaka kumi na minne iliyofuata, Ryanga alikuwa mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Mnamo mwaka wa 1997 aliteuliwa kuwa naibu wa msajili mkuu, wadhifa alioshikilia hadi mwaka wa 2000 alipokuwa Mhadhiri Mkuu. Pia alikuwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Masomo ya Mbali ya Chuo Kikuu cha Kenyatta (Institute of Open Distance Learning, Kenyatta University).

Ryanga ameandika kazi nyingi zikiwemo za kiakademia, kitaaluma na za kifasihi zikiwemo: *Dago wa Munje* (2008), *Dhana, Mbinu za Utafiti na Utendakazi wake* (2007), Ryanga, S. A. na wengine (Assoc. eds.): *Women Writing Africa, the Eastern Africa Volume* (2006), Ryanga, S. A. na Kawoya, V. *Kiswahili Subject Methods* (2005), *Joy and Her friends. Primary School Reader* (2004), *The Birthday Party*. *Primary School Reader* (2004) na *Kiswahili Language Skills I* (2003).

Riwaya yake ya kwanza, *Dago wa Munje* (2009) ilishinda tuzo la “Jomo Kenyatta Foundation Publisher” katika ‘kitengo cha vijana’. Pia ameandika tamthilia inayoitwa *Zinduko* (1985) iliyochapishwa na shirika la uchapishaji la Oxford. Pia ameandika vitabu vya kiada vya shule za msingi na sekondari:

1. 1985: Ireri Mbaabu na Sheila Ryanga. Lugha: *Kiswahili kwa Shule za Msingi*, Book 1. By Kenya Publishing and Book Marketing Co.
2. 1987: Ireri Mbaabu na Sheila Ryanga. Lugha: *Kiswahili kwa Shule za Msingi*, Book 2. By Kenya Publishing and Book Marketing Co.

Ryanga ni mwanachama wa Chama cha Kiswahili cha Kitaifa (CHAKITA) Kenya na Chama cha Kiswahili cha Afrika Mashariki (CHAKAMA).

Amewahi kuwasimamia wanafunzi wengi katika viwango vya shahada ya kwanza, uzamili na uzamifu. Akiwa mtahini wa Chuo Kikuu cha Moi—Eldoret, aliwahi kumtahini Dkt. Noordin Mwanakombo Mohamed katika tasnifu yake ya uzamifu ya mada; “*Ufasiri wa Ufeministi wa Kiislamu katika Utamaduni wa Mwanamke Mswahili: Mkabala au Ushirikisho?* (2009).

**2.1.2.1 Dago wa Munje (2008)**

Hii ni riwaya yake ya kwanza kuandika. Ni kazi ya kifasihi ambayo inaangazia unyanyapaa wanaopitia watoto wanapokuwa katika jamii. Inazungumzia pia jinsi mwanajamii asiye na uwezo wa kifedha anavyoweza kupoteza matumaini na kuchukiwa na wanajamii wenzake kiasi kuwa anapoteza mwelekeo wa kimaisha.

Kisa hiki kinamzunguka mhusika mmoja anayeitwa Dago anayetoka kijiji cha Munje. Ni mvulana mdogo ambaye ametoka katika familia maskini lakini anajikakamua na

kujaribu kusoma ili aweze kuifaa familia yake siku za usoni. Dago anabwabwaja, na kitendo hicho kinamfanya atengwe na wenzake shuleni na pia yeye mwenyewe anakosa kujiamini katika kutekeleza mambo ya kawadia kama wafanyavyo watoto wa kiume wa umri wake.

> Chumba chake Dago kilikuwa na ukubwa wa kiasi cha kutosha matandiko yake kwa upande mmoja, na pembezoni mwa upande mwingine palikuwa na sanduku la mabati lililochakaa na kudhihirisha miaka yake ya utumishi. (uk 2)
>
> …Kwa mwanafunzi wa darasa la sita, vitabu hivi vilionekana vichache mno. Hili si jambo lililomsumbua Dago pia. Kando na vitabu hivyo palikuwa na kalamu fupi ya risasi ambayo ncha yake iliisha hivi kwamba kama ingetumika kuandikia, hati zake hazingesomeka kwa njia sahihi na ingekwaruza karatasi iliyotumika. Hili halikuwa jambo geni. Pamoja na kalamu hii ya risasi, palikuwepo na biro moja iliyokaribia kuisha wino, na ambayo ncha yake ilikuwa imetafunwatafunwa kiasi cha kufanana na mswaki wa kijiti uliotafunwa. (uk 4)

Hapa mwandishi anatuonyesha jinsi umaskini ulivyokithiri nyumbani kwa akina Dago.

> Kijana huyu alikuwa katika darasa la sita, na alikuwa keshatiwa jandoni. Lakini, bado alikuwa mara kwa mara akirudiwa na ile tabia ya kukojoa kitandani usiku…
>
> Tabia hii ya kujilowesha kitandani ilimtia haya na hakuweza kuwatazama wenzake bila wasiwasi, kwa woga wa kujulikana. Aidha kukojoa kitandani kulimtia hofu asiweze kushirikiana na wenzake shuleni na hata pale kijijini. Alijishuku na kujiona tofauti akihisi kuwa alikuwa na kasoro ya kimaumbile. (uk 7-8)
>
> Dago alijua hana mtetezi. Alikumbuka maneno ya mwalimu kwamba ikiwa hangefanya bidii darasani angechapwa mbele ya wanafunzi wote wa shule wakati wa paredi. Aibu! Alipofikiria habari ya kuchapwa mbele ya wanafunzi wote, mwili ulimwingia baridi. Itakuwaje achapwe mbele ya wasichana ambao tayari walikuwa wamekwisha kushuhudia akidunishwa na wavulana wenzake! (uk 69)

Katika dondoo hizi tunaona jinsi anavyojiona tofauti na wenzake na kuogopa kuishi maisha ya kawaida kwa kuhofia mwalimu Sifa na wanafunzi wenzake.

Mwandishi huyu amemsuka Dago kama kijana asiyekata tamaa kwa urahisi japo kunao wakati ambao anakaribia kupoteza matumaini. Hilo halifanyiki na anajikomboa

kimawazo na kufanya kama wenzake na hatimaye anafuzu vyema na kujiunga na shule nzuri ya upili.

Riwaya hii inatuonyesha jinsi ambayo jamii mbalimbali zinawadhulumu baadhi ya wanajamii, wake kwa waume, kwa sababu wamekosa baadhi ya mahitaji ya kawaida. Inatuonya dhidi ya kuwatenga baadhi ya wanajamii kwa sababu ya kutopata mahitaji ya kimsingi kama inavyotarajiwa kwa wanajamii wote. Riwaya hii imejitenga na kawaida ya waandishi kuandika juu ya mtoto-mke na kuangazia hali ya mtoto-mume vilevile. Ni riwaya tuliyoitafitia katika tasnifu hii.

## 2.2 Hitimisho

Waandishi hawa wanawake wamejadili kuzorota kwa ndoa, ulanguzi wa dawa za kulevya na athari za ukosefu wa ajira kwa vijana. Peninah Muhando ameangazia ukandamizaji wa mwanamke kutoka kwa wanajamii na wanawake. Amezungumzia jinsi wanawake wanapinga ukombozi wao kwa kutokubali kushirikiana na wenzao. Aidha, waandishi wanawake wamezungumzia maswala tofauti tofauti katika jamii.

Waandishi Clara Momanyi na Sheila Ali Ryanga wametunga kazi zao ili kujenga jamii ambazo zina dosari kadha wa kadha, kama tu zilivyo jamii za kawaida; za kuwadhulumu baadhi ya wanajamii kama vile watoto wa kike, wanawake, maskini, na wale wasio na uwezo wa kifedha. Pia wamemulika maovu yanayofanyika katika jamii kama vile ufisadi, uongozi mbaya, ukoloni mamboleo, uharibifu wa mazingira na ukabila.

Kazi hizi zimezungumzia ukandamizaji unaoendelezwa dhidi ya wanajamii. Pia kupitia kwa usawiri wa wahusika, wanajamii wameonyeshwa hatari na madhara yanayoletwa na ukandamizaji huu kwa wanajamii wote kwa jumla. Kwa hivyo waandishi wanawake wanaangazia maswala mbalimbali yanayoikumba jamii.

# SURA YA TATU

# UKANDAMIZAJI WA JAMII KAMA UNAVYODHIHIRIKA KATIKA *DAGO WA MUNJE*

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii ukandamizaji wa mwanajamii kupitia jicho la mwandishi mwanamke umejadiliwa na kuchanganuliwa. Tumeangazia jinsi mwandishi Sheila Ali Ryanga alivyouangalia ukandamizaji katika riwaya yake ya *Dago wa Munje* (2008).

Riwaya ya *Dago wa Munje* (2008) ni ya kiuhalisia. Kuisoma mara ya kwanza, msomaji hupata yanayozungumziwa moja kwa moja kwa sababu yaliyomo ni maswala ya kawaida. Kisa chenyewe kinaakisi mambo ya uhalisia yanayotokea katika jamii tunayoishi. Hata hivyo, mwandishi ameshughulikia maswala ya kimsingi ya ukandamizaji unaotokea miongoni mwa wanajamii pasipo wao kutambua kuwa wanauendeleza ukandamizaji. Ryanga ameeleza hatua zinazotumika katika kuendeleza ukandamizaji huu ambao hatimaye unasababisha unyanyapaa miongoni mwa wanajamii wanaokandamizwa.

## 3.1 Mielekeo ya Ukandamizaji

Katika sehemu hii tunachanganua mielekeo ya ukandamizaji kama anavyoiwasilisha mwandishi Ryanga katika riwaya, *Dago wa Munje*. Tunaelezea jinsi unyonyaji huu unaendelezwa kwa wanajamii.

Mwelekeo ni dhana inayotumiwa kuelezea mtazamo au mkabala anaochukua msanii au unaochukuliwa na jamii kuhusiana na jambo, tukio, suala au wahusika fulani (Wamitila, 2003: 157).

*Kamusi Sanifu ya Kiswahili* (TUKI, 2004), inafafanua ukandamizaji kama hali au namna ambayo tabaka fulani linavyonyima haki tabaka jingine kisiasa na kiuchumi.

Kamusi ya *Merriam-Webster* (2015) inafafanua ukandamizaji kama utekelezaji wa nguvu za kimamlaka kwa njia isiyo na haki, iliyosheheni ukatili (Tafsiri Yangu).

Ukandamizaji ni hali ya kutomjali mwenzako, au kitu kingine chochote, kwa sababu unamwona au unakiona kama asiyefaa au kisichofaa kuthaminiwa. *Katiba ya Kenya* (2010) pia inagusia swala la haki za kibinadamu. Katika Sura ya Tatu, Sheria ya Haki, ya katiba hiyo inazungumzia haki za kimsingi ambazo zinafaa kudumishwa na serikali na kila mwananchi wa Kenya. Pia, sura hiyo inagusia umuhimu wa kutambua na kulinda heshima ya watu binafsi na jamaa na kukuza haki za kijamii na utambuaji wa uwezo wa binadamu wote wanafaa.

### 3.1.1 Ukandamizaji wa Watoto Kutoka kwa Watu Wazima

Ukandamizaji wa aina hii unatokea wakati mtu mwenye umri zaidi ya miaka kumi na minane (18) anamdhulumu mtu mwenye umri wa chini ya miaka kumi na minane. Dhuluma hii dhidi ya watoto huweza kutokea kwa njia ya kuwafungia watoto kutopata maarifa au elimu, uchumi, kuendeleza tamaduni na desturi zinazomdhuru mtoto na kutomwezesha kwenda kucheza au kutangamana na wenzake.

Ryanga amedhihirisha ukandamizaji unaoendelezwa kwa watoto kutoka kwa watu wazima. Anaonyesha jinsi watu wazima wanachangia katika kuwakandamiza watoto kwa njia mbalimbali aidha kwa kujua ama kwa kutojua. Ukandamizaji huu unafanyika shuleni na nyumbani na hauchukui mwelekeo wa kijinsia; yaani anayekandamizwa anaweza kuwa mtoto wa kike au wa kiume. Pia, anayekandamiza anaweza kuwa

mwanamume au mwanamke. Ukandamizaji huu una viwango viwili vikuu ambavyo vinajitokeza bayana. Viwango hivi ni kama ifutavyo.

### 3.1.1.1 Ukandamizaji wa Walimu kwa Watoto

Kiwango hiki cha ukandamizaji kinahusiana na walimu kutowatunza wanafunzi wao kwa njia inayotakikana kisheria na kimaadili. Walimu wanafeli kutambua haki za kimsingi za watoto-wanafunzi shuleni mwao na hivyo kusababisha watoto kutokua kwa njia ifaayo.

Mwalimu ana jukumu la kisheria la kumtunza mwanafunzi anayemsomesha. Afisa wa umma anafaa awe na subira, na heshima kila anapowahudumia wanafunzi, wenzake na wananchi kwa jumla, (*Teachers Service Commision Code of Conduct and Ethics*, 2003). Jukumu hili likikiukwa, huwa kuna adhabu ya kisheria anayofaa kupewa mwalimu. Hata hivyo, kwa sababu ya kutojua sheria na haki upande wa walimu, wazazi na hata wanafunzi, hakuna anayechukuwa hatua yoyote kila haki zinapokiukwa.

Pia, mwalimu ana jukumu la kijamii, ambalo pia tunaweza kuliita 'jukumu la kimaadili'. Jukumu hili hutekelezwa kwa misingi ya kiutu na uwajibikaji wa mwalimu husika. Halina sheria zozote. Ni wajibu ambao ni wa kila mwalimu na halijaandikwa popote na jukumu hili linapokiukwa, hakuna hatua ya kisheria itakayochukuliwa. Katika majukumu haya mawili, yote yanapokiukwa, huchangia kukandamizwa kwa mtoto.

Katika matini hii, ukandamizaji huu unajitokeza waziwazi. Katika ukurasa wa hamsini (50), Mwalimu Nyevu anaingia darasani na kuwaamuru wanafunzi watoe madaftari yao ya hesabu.

> "Toeni madaftari yenu ya hesabu. Je, kila mmoja amemaliza mazoezi yake?" (uk 50)

Dago hakubeba daftari lake na anamwarifu mwalimu kuwa alilisahau nyumbani. Wakati wa kipindi cha mapumziko, rafikize Rashid na Juma wanaanza kumkejeli wakimuuliza alikokificha kitabu chake cha hesabu. Wanamvutavuta na kumwimbia kuwa yeye ni kikojozi. Dago analia na anasaidiwa na Mishi ambaye alikuwa darasa la nane. Anawafokea wavulana hao akimtetea Dago. Kelele hizo zilisikika afisini alimokuwa mwalimu Sifa ambaye alitoka nje na kumwambia Dago amfuate afisini.

Mwalimu Sifa akamhoji Dago iwapo anamuona kama adui. Katika hali hii, mwalimu Sifa anataka kumsaidia Dago lakini anamkandamiza kwa kiasi fulani kwani hakuna mawasiliano mwafaka kuhusu anachokisema mwalimu. Kwa upande wake, Dago anamuona kama adui ambaye hamtakii mema kwa kumlazimisha kuwa shuleni. Pia, bila kujua, matamshi ya mwalimu huyu kwa Dago, ni ya kumdunisha, kumbeza na yanamwathiri kijana huyu.

> "Aha, vibarua ndivyo unavyopenda kufanya? Basi hayo tutazungumza baadaye. Sasa kwa nini mvulana wa miaka kumi na miwili kama wewe unaruhusu wengine kukuchezea? Unalialia tu kama mtoto."
>
> Je, ungependa kuwa mtu asiye hili wala lile maishani, bila kufanya kazi yoyote ya maana?" (uk 61)

Katika dondoo hili, mwalimu Sifa anamweleza Dago kuhusu umuhimu wa kutia bidii shuleni. Japo, sauti ya mwalimu inamkwaza Dago kwa sababu mwalimu anazungumza kwa ukali, maneno yake, yanamfanya Dago kukaa kimya na kujihisi kuonewa na mwalimu.

Mwalimu anamkandamiza Dago kwa kutomruhusu kusema yaliyo moyoni mwake kuhusu masomo. Woga wa mwanafunzi kwa mwalimu pia unajitokeza pale ambapo Dago anashindwa kuwataja wanaomchukia darasani mwake anapoulizwa na mwalimu Sifa.

> "Watu hawakupendi! Kuna vijana wangapi darasani mwenu? Kwa nini wewe ndiwe ambaye hupendwi? Isitoshe, ni akina nani ambao hawakupendi? Unaweza kuwataja majina yao?" (uk 58)

Katika kiwango hiki, ni wazi kuwa ukandamizaji wa aina hii unatokea pasi na wahusika kutambua kuwa unatokea. Pande zote mbili, inayokandamizwa na inayokandamiza, haijui kuwa inafanya au kufanyiwa hivyo. Mwalimu Sifa hatambui kuwa anamkandamiza Dago, naye Dago hatambui kuwa anakandamizwa.

Ukandamizaji huu, kama unavyojitokeza katika riwaya, unaashiria kuwa hakuna jinsia ambayo inalengwa. Ni ukandamizaji ambao ni 'huru': 'ukandamizaji huru'. Ukandamizaji huru ni ule ambao haulengi jinsia yoyote ile, yaani, unaoelekezwa kwa wanajamii kwa jumla. Ukandamizaji unaojitokeza katika kiwango hiki haubainishi ubaguzi wa jinsia. Japo tunamuona mwalimu akimkandamiza Dago, taswira tunayoiona si ile ya mwanamume anayemkandamiza mtoto wa kiume bali ile ya mwalimu kumkandamiza mwanafunzi wake.

Nchini Kenya, visa vya walimu kuwanyanyasa watoto vimekithiri. Shule nyingi, hasa za umma, walimu wana tabia ya kutojali wanafunzi. Mara nyingi huwanyanyasa kwa matamshi yao na aidha kuwachapa kupita kiwango. Tumeona walimu wakipelekwa mahakamani kwa kuwaumiza wanafunzi wao. Pia, walimu hawa huwadhulumu kimapenzi au kisaikolojia wanafunzi wao. Mwalimu mmoja katika kaunti ya Nakuru aliwanyanyasa wasichana sita wa shule ya msingi kimapenzi (*The Daily Nation*, Juni 30, 2015). Mwalimu huyo ndiye aliachiwa jukumu la kuwatunza wasichana hao lakini akakaidi maadili ya ualimu na kuwanyanyasa wasichana hao. Mwalimu huyo alifikishwa mahakamani na kushtakiwa na kosa la kuwanyanyasa wasichana wadogo kimapenzi.

Kisa kingine kilichofanyika humu nchini kilitokea katika kaunti ya Taita-Taveta. Mwalimu mkuu wa shule moja ya upili aliwafukuza wanafunzi wa Kiislamu kwa sababu ya kutoheshimu sheria za Kikristo katika shule hiyo (*The Daily Nation*, July 2 2015). Wanafunzi hawa walikataa kuhudhuria misa na wanafunzi wengine Wakristo. Mwalimu huyu anawakandamiza wanafunzi hawa kwa misingi ya kidini. Japo hivyo, ingekuwa vyema ikiwa wangepewa mawaidha kwanza kisha wakikiuka ndipo waadhibiwe kama sheria za shule zinavyosema. Pia, kisa hiki kinaonyesha jinsi wanafunzi wanavyokandamizwa na walimu wao katika hali halisi.

Katika kisa kingine, mwalimu alimnyofoa mwanafunzi wa darasa la saba sehemu zake za siri (*The Daily Nation*, June 2, 2015). Japo mwalimu anapinga kufanya hivyo, ni bayana kuwa lazima alikuwa na mkwaruzano fulani na mwanafunzi huyo kiasi ya kuwa anafikiriwa kuwa yeye ndiye alimkata mwanafunzi huyo.

Visa hivi vinaonyesha wazi kuwa wanafunzi hukandamizwa na walimu wao, kama alivyofanyiwa Dago. Walimu, hata humu nchini Kenya, huwakandamiza wanafunzi wao kiwango cha kuwajeruhi kimwili na hata kisaikolojia.

### 3.1.1.2 Ukandamizaji wa Wazazi kwa Watoto

Ukandamizaji unaotokea katika kiwango hiki unajumuisha wazazi na watoto wao. Ukandamizaji unaweza kuwa wa kisaikolojia au kimwili. Mtoto anaponyimwa haki zake za kimsingi: kutangamana na wenzake, kutopewa elimu, kutusiwa tusiwa, tutasema ananyanyaswa kisaikolojia, yaani kiakili. Ukandamizaji wa kimwili hutokea pale ambapo mzazi atamwadhibu mtoto wake na kumjeruhi. Mara nyingi adhabu hii hailingani na kosa alilolitenda mtoto. Wazazi hufanya mambo kama haya ya kuwaadhibu watoto wao kwa kuwachapa kwa fimbo, na wakati mwingine, hata kwa makofi. Katika harakati hizo, huwajeruhi.

Ukandamizaji wa aina hii, unaonekana kuanzia mwanzo wa kisa hadi mwisho. Mkondo wa ukandamizaji unaochukuliwa hapa si wa kijinsia japo tunayemuona anaendeleza ukandamizaji ni mwanamke (mamake Dago) kwa mtoto wa kiume (Dago). Hata hivyo, tukichunguza, itathibitika nia hiyo ya mwandishi ya kutozingatia jinsia ya anayekandamizwa na anayekandamiza; yaani, mwandishi anataka kuonyesha jinsi mtoto anavyoteswa na wazazi, wala si mtoto wa kiume anavyoteswa na mzazi wa kike.

'Upungufu' wa wahusika kwenye kisa unaweza kuwa sababu mojawapo ya kutomtumia babake kumkandamiza Dago. Ingawa tunaambiwa kuwa babake alikuwa hai, mwandishi ameamua kuua uhusika wake katika maisha ya Dago ndipo aeleze ukandamizaji wa mzazi kwa mtoto kwa njia mwafaka. Hata hivyo, babake Dago anaonekana ana mawazo hasi dhidi ya Dago japo hamwaambii waziwazi. Babake Dago, Mzee Majanda, anaungulika moyoni mara anapokumbuka tabia ya mwanawe. Hili linabainika anapokuwa anazungumza na mkewe kisha anamwelekezea kidole cha lawama kuhusu tabia mbovu ya Dago. Anadai kuwa mamake Dago ndiye amemdekeza mtoto wake hadi akawa mzembe wa kazi na kuwa na tabia ya kisichana. (Tabia ya kisichana ni mtazamo finyu na hasi ambao wanajamii hufananisha na ule wa kiumbe wa kike). Mamake Dago anauliza Mzee Majanda ikiwa Dago ameamka na jibu analolipata ni kuwa yeye ndiye amemtendekeza Dago:

> "Waijua tabia ya mwanao huyo. Umemtendekeza mno, mvulana hafanyi hivyo." (uk 116)

Mamake Dago naye anamjibu akijitetea kuwa malezi ya Dago ni yao wote:

> "Aa, vipi lawama na mimi ndiye ninayekuwa nikimkaripia kila wakati? Tabia hii ya usingizi wa mwanao hujaigundua? Sikiza mume wangu, mara kwa mara hukukumbusha kuwa watoto ni wetu sote." (uk 116)

Mamake Dago anamkandamiza Dago bila kuwa na ufahamu huo. Anafanya hivyo pasi na kuelewa fikira za Dago kwa undani. Alikuwa mtoto wa kiume pekee kwenye familia hiyo na hivyo alitarajiwa afaulu kwa kila alifanyalo. Hii ni sababu mojawapo ya mamake kumchunga sana kusababisha kukandamizwa kwake. Hata hivyo, ni bayana kuwa mamake alikuwa ameathirika na tamaduni ambazo humchukulia mwanaume kama anayetakikana kufaulu maishani.

Kisaikolojia, mamake Dago alishangazwa na tabia ya mwanawe. Mawazo haya yalimfanya amtazame Dago kama kiumbe tofauti ambacho kina kasoro fulani. Kila mara lilimpita moyoni jinsi kijana huyu wake asivyoweza kujimudu kama wenzake na hata kumfananisha na dada zake. Fikra kama hizi zinamfanya mamake amdunishe hata anapompa kazi za kufanya na hata anapoongea naye. Haya ni mawazo ya mamake Dago alipokuwa anamlinganisha na dadake Swafiya ambaye japo alitenda uovu na kupachikwa mimba, alikuwa na bidii shuleni, kinyume na kakake Dago:

> "Lau kama mwanangu wa kiume angejibidiisha kama dada zake. Mafanikio yetu yangekuwa makubwa si haba!" (uk 113)

Ingawa mwandishi anataja kuwa Mama Dago aliwathamini watoto wake sawa, mamake Dago hangeepuka kuhisi uchungu kuhusu matatizo aliyokuwa anayapata Dago kutokana na tabia yake. Mtazamo hasi aliokuwa nao kwa Dago, unasababisha mamake Dago aanze kuwawaza watoto wake wengine ambao japo wamefanya makosa, anawachukulia kama bora zaidi ya Dago ambaye yeye anamuona kama mzembe na mlegevu. Kwake yeye, la muhimu ni bidii shuleni na kwa lolote mtu afanyalo.

Katika kiwango hiki tunakumbana na ukandamizaji huru ambapo mamake Dago anamkandamiza kwa misingi ya uzembe na kitabia wala si ya kijinsia. Japo swala la jinsia linaonekana bayana, si kusema kuwa anakandamizwa kwa sababu yeye ni mtoto

wa kiume. Jinsia inatumika kumlinganisha na dada zake ambao wanaonekana kuwa na bidii katika yote wayafanyayo.

### 3.1.2 Ukandamizaji Baina ya Watoto

Ukandamizaji mwingine katika jamii unaotokea miongoni mwa jamii, ni ule wa watoto wa umri wa juu wakiwakandamiza wenzao wa umri wa chini. Huu ni ukandamizaji mbaya. Na hapa Kenya hutokea zaidi shuleni hususan za mabweni. Ingawaje, walimu wakuu wanapinga haya, wanaohusika hufukuzwa shule kabisa. Ukandamizaji huu, umeangaziwa na Sheila katika *Dago wa Munje.*

Ukandamizaji miongoni mwa watoto hutokea wakati ambapo watoto wanawadhulumu watoto wenzao. Mara nyingi, ukandamizaji huu hutokea bila washiriki wa pande zote mbili kutambua kuwa wanaelekeza ukandamizaji kwa wenzao au wanaokandamizwa. Wao huchukulia ni mzaha lakini ni kwenda kinyume na haki za kibinadamu. Ukandamizaji wa aina hii unaonekana waziwazi katika riwaya hii. Swala la jinsia katika kutekeleza ukandamizaji huu linajificha, na unapoendelezwa, hakuna mwelekeo wowote wa watoto kukandamizwa kwa kuegemea jinsia fulani; ama ya kike au ya kiume. Mara nyingi huchukuliwa kuwa wanaokandamizwa ni jinsia ya kike tu.

Ryanga amewaumba wahusika watoto, wa kiume na wa kike, ambao wanakandamizana baina yao. Watoto wa kike na wa kiume wanamkandamiza Dago, si kwa sababu ya jinsia yake, bali kwa sababu ya tabia yake. Dago anaonekana ana ulegevu wa kufanya kazi, kucheza na hata kuzungumza na wenzake. Hili linawafanya watoto rafikize wamkejeli kwa kumwambia kuwa ‘anafanya kama msichana’. Matamshi haya ni ya udunishaji wa jinsia ya kike. Hutumiwa mara kwa mara katika jamii hapa Kenya, yaani mwanamke hawezi kufanya jambo jema au kazi yoyote ile, bali ya jikoni. Taasubi hii, ndiyo iliyowafanya wenzake Dago kumfananisha na msichana.

Rafiki zake Dago, Rashidi na Juma, walikuwa na mazoea ya kumkejeli kwa kumwita kikojozi na mvivu. Wakati mwingine, wangemwimbia wimbo wa kikojozi:

> Kikojozi kakojoa, na nguo kaitia moto
> Kikojozi kakojoa, na nguo kaitia moto. (uk 53)

Kando na kusoma na Dago katika darasa moja, Rashidi na Juma walikuwa majirani zake huko nyumbani. Walikuwa ni watoto ambao walipenda kutangamana, na wacheshi wakati wote. Hii tabia yao ilikuwa kinyume na ilivyokuwa ile ya Dago, ya kutotaka kutangamana na wenzake.

Wakati wa kipindi cha mapumziko, baada ya mwalimu Nyevu kutoka darasani, wanamchezea shere wakimwambia kuwa alikificha kitabu chake cha hesabu kwa sababu hakuwa amefanya kazi ya mwalimu.

> "Dago ulikificha wapi kitabu chako cha hesabu?" Rashidi aliuliza.
> "Ulikificha, kwa sababu hukufanya kazi yako," Juma alisema kati ya vicheko.
> "Dago mvivu," Rashidi aliingilia, na kumvutavuta Dago huku na kule.
> "Kila siku vitabu vyako vinapotea," wote walimwingilia na kumcheka. (uk 52, 53)

Hayo yakijiri, wanafunzi wengine wanakusanyika hapo na kumzingira Dago na wanamwimbia wimbo wa kikojozi. Alipoona hivyo, Dago alidondokwa na machozi asijue la kufanya kwa sababu walimzuia asitoroke. Msaada unatokea pindi Mishi, rafikiye dadake Swafiya, anapowasili na kuwafukuza wadhalimu wake.

> "Rashidi na Juma, mbona mwenzenu hana raha, ana nini?" Mishi aliwauliza waliokuwapo, na kuingia katikati ya duara. Rashidi na Juma waliangaliana, kisha wakacheka. Mishi aliwakazia macho bila kusema chochote.
> "Mishi, hujatusalimu bado, mbona maswali mengi hivyo?" Juma aliuliza.
> "Habari zenu," alisalimia Mishi.
> "Hatujambo." Walijibu.
> "Sasa nielezeni kisa cha haya yote."

> “Sikiza, Mishi,” alisema Juma, “Dago daima anatuaibisha sisi wavulana. Mwangalie hali yake, yeye daima ni mtoto anayehitaji kufunzwa usafi na adabu.”
> Juma na Rashidi waliangua kicheko. Wanafunzi wengine wakasongea wasikie yanayoendelea. Duara iliyomzunguka Dago iliongezeka isipokuwa sasa hapo katikati walikuwa wawili, Dago, pamoja na Mishi.
> “Uchafu ni wake, nyinyi mwamtakia nini? Mwacheni nendeni zenu mkacheze kwingine. Dago twende zetu.” (uk 54, 55)

Waliokuwapo hapo, walianza kutawanyika mmoja mmoja lakini kabla ya Rashidi na Juma kutawanyika, Rashidi alimkejeli zaidi Dago kwa kumwambia kuwa anahitaji kujilinda yeye mwenyewe kwani yeye ni mwanamume. Juma anaongeza kwa kudai kuwa wao ndio wanafaa kumfunza kwa sababu yeye ni mwanamume kama wao tu:

> “Hadi lini utalindwa na wasichana?” Rashidi aliingilia. “Sisi ndio wa kumfunza ya wanaume!” Juma alisema. (uk 55)

Rashidi na Juma wanafungua ukurasa wa jinsia na kutaja kuwa Dago analindwa na wasichana jambo ambalo linaashiria ubaguzi wa jinsia. Ni katika hatua hii ambayo Ryanga anatuonyesha kuwa hata watoto wana kasumba za jinsia. Mtoto mdogo kama Rashid anatambua kuwa Mishi ni msichana na kulingana naye, hafai kutetea mvulana. Ingawa hivyo, ni bayana pia kuwa marafiki hao hawamkandamizi Dago kwa misingi ya jinsia yake ya kiume. Hata ikiwa wametaja jinsia ya kike, ubaguzi huu wao dhidi ya Dago hautokani na jinsia ya Dago, ambayo ni ya kiume, bali unatokana na sababu zingine nje ya jinsia; mtazamo wa kijamii, kwamba mtu asiyejiweza kwa njia moja ama nyingine hudunishwa badala ya kusaidiwa. Ingekuwa wanatumia jinsia, basi ingekuwa rahisi kwao kumkandamiza msichana ambaye kwao wao ndiye alikuwa hana uwezo wa kujitetea.

Ryanga anaeleza aina hii ya ukandamizaji kuwa ni isiyochagua ni jinsia ipi ambayo inaelekezwa kitendo hicho. Watoto wanaendeleza ukandamizaji bila ya kufuatilia ni

nani wanayemkandamiza kijinsia lakini kwa kutumia kigezo kingine ambacho ni wao wenyewe wanakiumba akilini mwao. Wanaweza kutumia jinsi mtoto mwenzao anavyoongea, anavyotembea, anavyofanya kila jambo lake. Ikiwa anafanya tofauti na wao wanavyofanya, basi watapata sababu ya kumdhalilisha. Ukandamizaji huu ulioangaziwa na kukashifiwa na Ryanga ni wa kiuhalisia, daima unapatikana katika shule nyingi hapa nchini. Kwa hivyo Ryanga anasawiri hali halisi miongoni mwa jamii hapa Kenya, taasubi ya kudunisha jinsia ya kike na ukandamizaji miongoni mwa watoto wa umri tofauti tofauti.

### 3.1.3 Ukandamizaji wa Nafsi

Ukandamizaji wa nafsi una kigezo cha kiakili au kifikra. Hutokea mhusika anapopata changamoto nyingi maishani na hatimaye kujifikiria kuwa yeye ni dhaifu zaidi ya viumbe wengine wa jamii. Anajidhalilisha na kila anapotangamana na wanajamii wengine, anaanza kujikinga kutokana na matamshi au mienendo yao kwake, hata ikiwa matamshi na mienendo hiyo haimdhuru. Huwa amejitenga na wenzake bila kujua kuwa anafanya hivyo. Hii ni hali ya unyanyapaa, yaani mtu kuona maisha hayana maana kwake, hivyo kujitenga na wenzake. Hali hii mara nyingi hutokea iwapo mtu daima anakashifiwa au kudharauliwa kama Dago anavyofanyiwa.

Aina hii ya ukandamizaji pia inajitokeza katika kazi hii, na inaweza kutambuliwa kama ukandamizaji wa kisaikolojia. Ukandamizaji huu unatokea akilini mwa mhusika. Mara nyingi hutokana na hali za nje anazopitia muathiriwa: wanavyosema watu kumhusu, wanavyomtendea au hata matukio aliyoyapitia maishani mwake.

Ryanga amemuumba Dago kama mhusika ambaye aidha hajitambui, hajielewi kabisa au wanaomzunguka wamemfanya asijielewe wala kujitambua. Watu wanamkandamiza kufikia hatua ya kujiona kuwa yeye si bora zaidi ya wengine na hivyo kujidunisha.

Akiwa nyumbani, mamake anamgombeza na kumfanya ajihisi kama asiyetakikana humo nyumbani. Baada ya Dago kukejeliwa na wenzake chuoni, anachelewa kurudi nyumbani. Kwa sababu anajua kuwa atagombezwa, ananyemelea pole pole na kuingia nyumbani lakini kwa bahati mbaya mamake anasikia mkwaruzo wa pipa la maji aliloligonga na kumwita. Anamdanganya kuwa hajihisi mzima lakini mamake hachelei kumgombeza:

> "Ni nani huyo nyumbani? Dago ni wewe?" Mama aliuliza bila kuacha kazi zake.
>
> "Ndiyo, shikamoo mama," aliitikia huku akijikunyatakunyata.
>
> "Dago una nini, mbona sauti hivyo?"
>
> "Sijisikii vyema mama, tumbo linaniuma," Dago aliitikia akifikiri kwamba uongo ungemfanya mama yake asiulize maswali mengi… (uk 104)

Anamuuliza ikiwa amekunywa dawa lakini Dago anamwarifu kuwa anachohitaji ni kupumzika tu. Mamake Dago anaelekea chumbani mwake kumtayarishia Dago kitanda. Anakabiliana na mzizimo wa harufu ya mkojo kutoka kwa godoro la Dago. Mamake anaanza kumsomea bila kutaka kumhoji ili aweze kujua tatizo hasa la Dago kuwa kikojozi hadi umri huo wake ni lipi. Dago anajisikitikia na kuanza kujihoji na kujihurumia kuhusu masaibu anayokumbana nayo shuleni na nyumbani. Anajiona kiumbe dhaifu asiyetakikana duniani.

> Naye Dago alijisikitikia badala ya kusikiliza mawaidha na kutafakari jinsi ya kujiopoa na aibu kama ile mbele ya mama yake. Alikuwa akiwaza, "Shuleni nachekwa, nyumbani nakashifiwa, Amani iko wapi basi?" (uk 106)

Hali hii ya Dago imesawiriwa kimaksudi na mwandishi ili kutuonyesha kuwa katika jamii kuna watu kama Dago na hukashifiwa na kudharauliwa. Ryanga anaangazia hali hii kwa masikitiko. Analotuambia ni kuwa watu kama hawa wanahitaji huruma na

msaada badala ya kukashifiwa na kudharauliwa. Watu kama hawa wanahitaji mapenzi kutoka kwa familia na jamii ili wajirekebishe na wasijione viumbe duni. Kasoro kama hizi zipo na ni za kimaumbile wala si za kujitakia. Jamii iepukane na ukandamizaji kama huu.

Shuleni anaadhibiwa na kuchekwa na wenzake kila mara jambo ambalo limemfanya afikiri kuwa yeye hafai kusoma kama wenzake na kuwa yeye si bingwa darasani. Wakiwa kwenye mapumziko, marafiki zake wanamchezea shere kila mara na hata kumfanya alie (kama msichana).

> "Huyo kikojozi!" Walipokuwa wakisema hivi, walimzunguka. Walifanya duara na kumweka Dago katikati wakimwimbia wimbo wa kikojozi…
>
> Dago alitokwa na machozi, hasa alipowaona wasichana wa shule wakishuhudia haya. Alijaribu kutoroka lakini wenzake walimzuia. Aibu aliyoipata leo, hakuionea mfano wake. Kwa nini walimuonea vile? (uk 53)

Hali yake ya kuwa kikojozi, ambayo si kosa lake na ambayo ni zaidi ya uwezo wake, imebadilishwa na kuwa ambayo amejitakia na hata yeye mwenyewe anajilaumu kwa kuwa kikojozi. Hili limesababisha yeye mwenyewe kutojipenda na kujidhulumu kiasi kwamba hajiamini kwa lolote alifanyalo. Kwa mfano, anapoitwa na mwalimu Sifa afisini mwake, anaulizwa kinachomtatiza kwani kila mara anachezewa shere na watoto wenzake lakini hana jawabu mwafaka, na anamwambia mwalimu kuwa wanafunzi hawampendi. Mwalimu Sifa anamjibu kwa kumuuliza ni kwa nini wanafunzi wenzake hawamo katika shida anazopitia, bali ni yeye peke yake ambaye hapendwi.

> "Dago wakati huu hakujua kama aliitwa afisini humo ili aadhibiwe, au kwa sababu nyingine tofauti. Alionekana kudhoofika kwa uchungu aliokuwa nao moyoni. Hakuweza kufahamu kama ni yeye peke yake ama kama watoto wengine wa rika lake walikumbana na matatizo kama yale. Jambo lililomtia wasiwasi ni kwamba, leo hajapata nafasi

> ya kutulia. Alianza siku kwa matata na yamemfuata hadi sasa. Akilini mwake mlijaa mawazo mbalimbali alipoketi kitini, afisini mle. (uk 57)

Haya yote yalikuwa akilini mwa Dago pindi alipoitwa na mwalimu Sifa baada ya kupatikana akiwa miongoni mwa watoto wengine waliokuwa wanamfanyia fujo. Haya yote ni matatizo ya kisaikolojia. Vitendo vya wenzake, na tabia yake ya kikojozi, imemfanya adhalilike kimoyomoyo.

> "Dago, twende afisini mwangu." Mwalimu Sifa aliposema maneno haya, yalikuwa kama maliwazo kwa Dago…
>
> "Keti hapo kitini Dago." Mwalimu Sifa alisema kwa sauti tulivu…
>
> "Kuna shida gani Dago. Kwa nini siku haipiti bila kukuona ukichezewa na watoto wenzako?" Sauti ya mwalimu haikuwa ya mzaha.
>
> "Sijui mwalimu. Watu hawanipendi." Alisema Dago.
>
> "Watu hawakupendi! Kuna vijana wangapi darasani mwenu? Kwa nini wewe ndiwe ambaye hupendwi? Isitoshe, ni akina nani ambao hawakupendi? Unaweza kuwataja majina yao?" Fikra zilipita nyingi kwa haraka akilini mwake Dago. (uk 57, 58)

Ukandamizaji huu umemfanya Dago azame katika mawazo changamano kuhusu nafsi yake mwenyewe lakini hapati jawabu mwafaka. Dago anawaza kwa nini kila wakati hana furaha moyoni na wenzake wanamchezea shere. Fikra hii inamfanya Dago awe na ukiwa. Huu ni ukandamizaji wa kisaikolojia unaoletwa na kejeli kutoka kwa wanafunzi wenzake, wazazi wake na Mwalimu Sifa.

Ryanga amebainisha waziwazi kuwa mtoto huyu anapitia mengi ambayo yamemlemaza katika kuendeleza shughuli zake kwa njia ya kawaida: amekandamizwa na mawazo ya jinsi anavyojifikiria. Bado hajajitambua yeye ni nani na hili limeshinikizwa zaidi na umri wake mdogo ambapo akili yake haijakua ili kuweza kung'amua haswa njia bora zaidi ya kukumbana na wanayosema wengine kumhusu.

Aina hii ya ukandamizaji inaweza kuwepo kwa mtu wa jinsia yoyote na umri wowote. Japo mwandishi amemtumia mhusika mtoto wa kiume, hakuna ithibati kuwa alikuwa ana ubaguzi fulani wa kiumri au kijinsia kwa sababu ya alivyomkuza mhusika huyu na mandhari anayopitia hadi anapotamatisha kisa chake.

### 3.1.4 Ukandamizaji wa Mwanamke

Aina hii ya ukandamizaji pia imejotokeza katika riwaya ya *Dago wa Munje*. Hata hivyo, ukandamizaji huu haujakithiri kama aina zingine za ukandamizaji zilivyoonekana riwayani.

Babake Dago anamlaumu mkewe kwa udhaifu wa Dago. Anajitenga na majukumu ya malezi ya mtoto wake na kumrushia mkewe. Pia, Babake Dago ana mawazo kuwa wavulana hawafai kutendekezwa. Kwake yeye, wasichana ndio wanafaa kutendekezwa.

> "Waijua tabia ya mwanao huyo. Umemtendekeza; mno, mvulana hafanyi hivyo." (uk 116)

Fikra hii ya Baba Dago ni fikra dunishi mno. Mtoto hulelewa na wazazi wote wawili. Inapotokea udhaifu kwa mtoto, sharti wazazi wote wawili wakubali ni tatizo lao wote, na wawajibike kama wazazi kupata suluhu. Daima katika jamii, fikra kama hizi zipo; kuwa akina mama ndio wawajibike katika tabia za watoto wao. Iwapo kutatokea tabia mbaya kati ya mtoto mmoja, basi lawama huenda kwa mama. Huu ni unyonge wa jamii yetu na ni lazima kupambana nao na kuondoa fikra potofu kama hizi. Kwanza Baba Dago ndiye anafaa kumshughulikia zaidi Dago katika tatizo hili kuliko mamake. Kwa hivyo Baba Dago anachangia ukandamizaji mara mbili; wa mkewe na wa mtoto wake. Ryanga ameliangazia tatizo hili. Kuliangazia hivi ni kwamba hata yeye analikashifu na halifai.

### 3.2 Suluhisho la Ukandamizaji

Suluhisho la ukandamizaji limejitokeza kwa njia anuwai kama tu zilivyo aina za ukandamizaji. Ryanga amedokeza njia ambazo zinaweza kutumika ili kuepukana na unyanyasaji wa mwanajamii yeyote bila kujali umri au jinsia yake. Ili kuweza kutatua tatizo la ukandamizaji, ni vyema mtatuzi kuelewa chanzo cha ukandamizaji huo. Ryanga ametoa suluhisho la ukandamizaji katika riwaya yake kama inavyodhihirika hapa chini:

#### 3.2.1 Suluhu Kutoka kwa Watoto

Katika riwaya hii, Ryanga amedokeza kuwa watoto wenyewe wanaweza kusuluhisha ukandamizaji. Suluhu yao inakuwa ya manufaa hususan pale ambapo anayekandamizwa ni mmoja wao.

Hatua yao ya kutoa suluhu inakuja pasipo wao kutambua ikiwa wanafanya hivyo. Mishi, rafikiye dadake Dago, anamsaidia Dago kutokana na mikono ya wadhalimu wake na anataka kujua ikiwa anayo shida yoyote inayosababisha kuteswa na wenzake.

Juma na Rashid wanapanga mpango wa kumshirikisha Dago katika ushirika wao wa kuenda kufua nguo zao mtoni. Mpango huu una nia ya kumfunza Dago adabu ili aiache tabia yake mbovu ya uzembe na kujiwekea mambo moyoni mwake. Wanapomwendea kumuarifu kuhusu mpango wao, anajaribu kukataa eti anahisi uchovu na kuwa yeye ni mgonjwa. Wanasisitiza na kumtishia kumsema kwa wazazi wake kuwa yeye ni mzembe na hata kuyataja zaidi ya hayo. Ni hapo ambapo Dago anakubali kwa ujasiri kujiunga nao katika mpango huo. Anawajibu kwa sauti ya ukali na yenye hisia:

> “Haya nitakwenda nanyi. Nitakwenda nanyi ili niwaaibishe na kashfa zenu za uongo. Nitakuja nanyi na nitafua nguo zangu. Nitacheza mchezo wa Tarzan na mwingine wowote mtakaochagua. Nitaogelea, niwaonyeshe kwamba Dago si mjinga wala si mtoto kama

> mnavyoamini. Baada ya nusu saa kutoka sasa, nitaungana nayi njiani kuelekea mtoni." (uk 137)

Msisitizo wa Rashid na Juma ulimfanya Dago kujichunguza na hatimaye kujitambua kuwa yeye ni binadamu na mwenye uwezo kama hao wenzake. Alitambua kuwa hakuwa na kasoro yoyote ya kimaumbile, na siku hii ndiyo ilikuwa ya kuwafundisha somo kuukubali wito wao wa kwenda mtoni.

Dago anajikwamua kutoka kwa pingu za ukandamizaji kupitia kwa watoto wenzake. Kwa hivyo hali hii imetokana na watoto wenzake, na kumfanya shujaa na shupavu. Mzaha na ushawishi wa watoto wenzake umekuwa suluhisho kwa matatizo ya Dago. Ingawaje mwandishi ameuonyesha kama ukandamizaji lakini umekuwa suluhisho mwafaka kwa matatizo ya Dago. Imesawiri usemi wa Kiswahili kuwa "unapomkwamua jipu mtu, usimwonee huruma". Udhalimu ndio utamsaidia kupona jipu hili. Msemo huu unaafiki yaliyomtokea Dago bila watoto wenzaka kudhani ni suluhisho la matatizo yanayomkumba Dago.

### 3.2.2 Suluhu Kutoka kwa Watu Wazima

Ryanga ametumia watu wazima katika kutoa suluhisho la ukandamizaji dhidi ya mwanajamii kwa njia mbalimbali.

#### 3.2.2.1 Mama

Wazazi wanatumiwa kumzindua anayekandamizwa kwa kumpa maarifa ya kujitambua nafsi yake. Mamake Dago anamkashifu Dago kila anapotenda na kumrudi kila mara anapokosea.

> "Tabia hii sitaiweza. Kwa nini hukuyatoa matandiko yako asubuhi ulipoamka yakakauka juani? Wewe siye mtoto tena, eti mama akutumikie kiasi hiki? Ni aibu hii!"
> Mama aliendelea kukoka moto chumbani mwa Dago ili umletee joto na kukausha mzizimo uliokuwamo. Hakutaka kuzua mgogoro ambao mara nyingi ulitokea baina yao alipomrudi kuhusu tabia hii yake chafu. (uk 106)

Mamake Dago anafahamu kuwa Dago ni mtoto na anahitaji mawaidha ili kurekebisha tabia yake. Yeye hafanyi hivyo bali anamkemea, na fauka ya hayo, kama mama anayempenda mtoto wake, anakoka moto ili chumbani muwe na joto mtoto wake asidhurike. Mkemeo huu si wa kumchukia Dago na kumlaani bali ni wa mapenzi ya mama ya kumtaka Dago ajirekebishe kwa upande mwingine. Lazima tufahamu kwamba wakati mwingine kemeo kutoka kwa mzazi ni kumtaka mwana wao ajirekebishe wala si chuki.

#### 3.2.2.2 Baba

Babake Dago anapomkashifu mamake Dago kwa kukosa kumfunza ‘mwana wao’ tabia njema, mamake anamweleza kuwa jukumu hilo ni lao wawili bali si lake peke yake.

> “Waijua tabia ya mwanao huyo. Umemtendekeza mno, mvulana hafanyi hivyo.”
>
> “Aa, vipi lawama na mimi ndiye ninayekuwa nikimkaripia kila wakati? Tabia hii ya usingizi wa mwanao hujaigundua? Sikiza mume wangu, mara kwa mara hukukumbusha kuwa watoto ni wetu sote.”
>
> “Nami sijakataa hilo, una maana gani?”
>
> “Naam, wanapokuwa na tabia njema tuwatie moyo wa imani waendelee na wanapozibua tabia mbaya, tuwaongoze sote wawili. Lakini wewe kazi yako iko mbele. Umeniachia peke yangu, wavulana kwa wasichana!” Alisema mama akajiondolea lawama. (uk 116)

Malmake Dago anamwarifu mume wake kuwa watoto wanapokuwa na tabia njema wanafaa kutiwa moyo wa imani ili waendelee, na wanapoenda visivyo wanafaa kukosolewa kwa upendo. Anamweleza kuwa jukumu la kuwarudi watoto ni la wazazi wote bali si la mzazi mmoja. Wazazi wa kiume wanafaa waiche tabia ya kujitia zaidi kazini kutafuta pesa bila kujali watoto wao. Lazima watafute muda wa kuwa nyumbani na watoto wao kuwaadili na kuwapa marudi mema. Hali hii huenda ikasaidia kuondoa matatizo kama ya Dago.

### 3.2.2.3 Mwalimu Sifa

Mwalimu Sifa anajikakamua na kumkashifu Dago pale anapojaribu kukataa kusoma. Anamweleza kuwa fikra za kutotaka kusoma ni fikra za watu wanaoishi kiholela, wanaokuwa majambazi baadaye ama kuwa kupe maishani mwao. Mwalimu Sifa anamweleza umuhimu wa masomo na mwishowe wanapoachana naye, Dago anabaki ameridhia wosia wa mwalimu wake:

> "Rudi darasani mwako! Tena sikiza, kila mara nikikuona unajikunyatakunyata na kujihurumia kana kwamba wewe ni mkiwa, utaniona. Simama imara kama watoto wengine shuleni, na nikikuona umezingirwa tena ili kuchezwa shere, moja kwa moja mimi nitakuadhibu kwa ujinga wako. Ikiwa darasani hufanyi bidii, nitahakikisha unachapwa mbele ya wanafunzi wote wakati wa paredi ya asubuhi. Aibu na maumivu vitakusaidia kufanya bidii." (uk 68)

Ukaripiaji huu, ingawa ni unyanyasaji, unamsaidia Dago. Anabadilika, msimamo wake kuhusu masomo unageuka. Anafanya bidii.

> Itakuwaje achapwe mbele ya wasichana, ambao tayari walikuwa wamekwisha kushuhudia akidunishwa na wavulana wenzake. Hatakuwa na njia ya kuyainua macho yake juu tena. Suluhisho lilikuwa katika mambo mwawili tu aliyoyaona kuwa yamebidi ayazingatie. Kwanza ilikuwa ni kutoroka shule kabla jambo hilo kutokea ama pili, afuate mawaidha ya mwalimu Sifa ya kutia bidii darasani. (uk 69)

> Alifungua sehemu ya maswali na kujaribu kujibu yale aliyokuwa ameyakosa. Hata haya aliyaona kutokuwa magumu. Akajiuliza tena, "Ni kwa nini maswali niliyoyakosa hapo awali sasa naweza kuyafahamu majibu yake bila usaidizi wa mwalimu? (uk 71)

Dago anazinduliwa na mwalimu Sifa na kuambiwa ukweli unaomwacha akiwa anatafakari hatua itakayofuata. Mwalimu huyu kwa mkemeo wake, anamsaidia Dago kujirekebisha.

Watu wazima wanamsaidia Dago kujipa changamoto ya kujua yeye ni nani na uwezo alionao anapokabiliana na changamoto za maisha. Wanamuonyesha kuwa kila mtu ana

mahitaji yake na lazima ajipiganie ili aweze kupewa nafasi yake inayomfaa kwani hakuna ambacho kinakuja bila ya bidii au kupiganiwa. Dago hatimaye anaanza kuona uhalisia wa anayoambiwa na wazazi na walimu wake na anakuwa mshindi: mvulana mwenye kujitegemea. Ingawaje huu ulikuwa unyanyasaji unaokuwa ukandamizaji kwa mtoto, umemsaidia Dago. Hata hivyo ninadhani, njia ya upole ingekuwa mwafaka zaidi badala ya ukali na kashfa hizi. Ryanga kwa kuuonyeha ukandamizaji huu, ni kuwa hauungi mkono, hivyo uachwe na njia bora zaidi zitumike. Mimi ninamuunga mkono. Walimu wanafaa warekebishe tabia za watoto kwa hekima na urafiki ili watoto wasiwe na unyanyapaa kama wa Dago.

### 3.2.3 Utambuzi wa Nafsi

Suluhisho la aina hii linatokea akilini mwa mtu binafsi. Inahitaji anayekandamizwa atambue hali yake na ajaribu kutafakari kuhusu atakachokifanya ili ajiopoe. Pia, anahitajika kuangalia mazingira yanayomzunguka na jamii ilivyo. Ili kujitambua vyema, ni muhimu pia atafute chanzo cha matatizo yanayomkumba, na kwa jicho pevu, changamoto zilizopo katika jamii.

Dago mara kwa mara alifikiria hali yake hususan anapokumbana na tatizo ana kwa ana. Kila mara alipopewa mawaidha na mamake au mwalimu Sifa, angetafakari kuhusu aliyoambiwa na kujaribu kutambua mbona kila wakati iwe ni yeye.

Mhusika Dago anafanya uamuzi wake binafsi na kuamua kuwa dereva wa maisha yake. Hatimaye anapigania nafasi yake na hata kumenyana na wenzake anaowashinda na kutangazwa mshindi. Wote wakamuogopa na kumwona kama binadamu kamili na jasiri.

Ryanga anatuonyesha kuwa suluhisho hili hutokea mtu binafsi anapogutuka na kung'amua kuwa anakandamizwa na wengine. Naye asimame kidete ajikomboe. Dago alifanya hivyo.

### 3.3 Hitimisho

Sura hii imegusia maswala ya watoto kukandamziwa na watu wazima. Mwandishi anaelezea jinsi ukandamizaji unavyoendelezwa bila wanajamii kujua ikiwa wanakandamizwa. Kupitia kwa mhusika Dago, mwandishi anaonyesha njia mbalimbali ambazo mwanajamii anakandamizwa. Anamtumia Dago kama sauti yake katika kuelezea unyanyasaji wa mwanajamii. Katika ulimwengu wa riwaya ya *Dago wa Munje,* watoto wanachukua nafasi ya mbele kusuluhisha maswala yanayomkabili mwanajamii. Katika kufanya hivi, mwandishi hajainua jinsia yoyote na amemtumia mtoto bila kuhusisha jinsia yake. Ameonyesha anayekandamizwa si mtoto wa jinsia ya kike tu bali hata mtoto wa kiume hupitia hali hiyo.

Aidha, japo mwandishi hajagusia swala la ukandamizaji wa mwanamke kwa undani, ameonyesha jinsi athari hasi dhidi ya mwanamke na mtoto wa kike zinamwathiri mwanajamii. Mwandishi ameonyesha jinsi mtu anayekandamizwa anavyoweza kujinasua kutokana na ukandamizaji wa aina yoyote. Dago amekandamizwa bila kurejelea jinsia yake na hivyo basi kupitia kwake tunatambua kuwa ukandamizaji haulengi jinsia bali ni hali ya kijamii. Na, suluhisho la ukandamizaji kama huu ni mkandamizwaji atambue shida hii na apambane nayo vilivyo.

# SURA YA NNE

# UKANDAMIZAJI WA JAMII UNAVYODHIHIRIKA KATIKA *NAKURUTO*

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia jinsi Clara Momanyi alivyouangalia na alivyousawiri ukandamizaji katika riwaya yake *Nakuruto*. Riwaya yenyewe ni ya kusisimua ikiwa msomaji ataelewa muktadha wa kiutopia ulioumbwa na mwandishi Clara. Kwanza tumeeleza kisa chenyewe kwa muhtasari. Tumejadili ukandamizaji wa mwanajamii kwa kupitia jicho la mwandishi mwanamke kwa kuerejelea riwaya hiyo. Tumechanganua mielekeo mbalimbali ya ukandamizaji kama inavyojitokeza katika riwaya ya *Nakuruto* kupitia kwa mawazo ya Clara Momanyi. Tumejaribu kuchanganua jinsi Clara anavyoitazama jamii na aina anuwai za ukandamizaji anazomulika na suluhisho analopendekeza kutekelezwa na mwanajamii anayekandamizwa. Pia, tumechunguza ikiwa ukandamizaji huu unaendekezwa kwa' mwanajamii yupi: je, ni kwa mwanajamii wa kike, wa kiume, mwanajamii mwanamke au mwanamume? Tumeangazia anayetoa suluhisho na ikiwa suluhisho hilo linaweza kutekelezeka.

## 4.1 Mielekeo ya Ukandamizaji

Ukandamizaji kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004), ni hali au namna ambayo tabaka fulani linavyonyima haki tabaka jingine kisiasa na kiuchumi. Maelezo haya yanatuonyesha kwamba kundi fulani la jamii moja huonea lingine hususan lile lisilo na uwezo. Katika tasnifu hii, tumechukulia ugandamizaji kama maonevu ya aina yoyote na athari hasi katika jamii zinazosababishwa na wanadamu wenyewe. Kwa hivyo Clara, kupitia riwaya ya Nakuruto, ameonyesha hali hizi za ukandamizaji. Ukandamizaji umejitokeza katika ncha mbalimbali.

### 4.1.1 Ukandamizaji dhidi ya 'Wanaoota'

Ukandamizaji huu ni ule ambao unaelekezwa kwa wanajamii ambao wana maono ya maendeleo katika jamii. Wanaoota ni wale wanajamii ambao wanataka kuiona jamii iliyokomaa kisiasa na kiuchumi.

Ukandamizaji unaotawala katika riwaya ni ukandamizaji dhidi ya 'wanaoota'; wale wambao wanataka kuiona jamii yote kwa jumla ikiendelea mbele katika nyanja tofauti tofauti bila ubaguzi wowote. Wanaokandamizwa ni wale ambao wanatarajia kuona nchi nzuri iliyo na maendeleo, isiyo na ufisadi, nchi ambayo inahifadhi mazingira, inayowathamini wanawake na kuwapa nafasi ya kuwajibikia jamii; wale ambao wanapigania wanajamii kwa jumla ili waweze kuishi ilivyokusudiwa na Muumba. Hawa ni wanajamii ambao wanakandamizwa na wazee wa jamii, wanawake na viongozi wa serikali. Wanaonekana kama watu wanaoleta usawa ambao ni hatari kwa wakandamizaji hawa kwani wanajamii wakizinduliwa watakuwa werevu zaidi na hatimaye watapinga uongozi mbaya. Katika hali halisi humu nchini Kenya, 'wanaoota' ni wanaharakati na wananchi ambao wanapigania usawa. Mara nyingi, wao hushikwa na kushtakiwa kwa makosa yasiyokuwa na uzito wa kikatiba au hata huuawa kwa njia zisizoeleweka.

Mwandishi Clara anasema kuwa ndoto ni uhalisi wa maisha. Anapoandika kuhusu ndoto ya Nakuruto kupitia riwaya *Nakuruto*, Clara anajaribu kutuonyesha kuwa anayoyakusudia kumpitishia msomaji ni kuwa kila analolifikiria kuwa jema kwa jamii, ndilo linafaa kutekelezwa hata ikiwa huenda linaonekana kama lisiloweza kutendeka.

> "Humu mtaani tu. Nilitaka kukuona ili tupange namna ya kumwondoa haini Welllingtone," Nakuruto alibainisha lengo lake bila kusita. Mfumwa alishtuka na kusimama ghafla.
>
> Ulisema wewe ni binti ya nani? Ati unataka tupange kumwondoa nani? lUmenijia yosayosa hapa ili tupange maanagamizi yetu wenyewe?"…

"Uko na nani katika mpango huu?"
"Peke yangu."
"Hujui wewe umo ndotoni?" (uk 66)

Nakuruto anamwambia chifu Mfumwa kuwa wanahitaji kumwondoa haini Wellingtone ambaye anawanyonya wanajamii lakini Mfumwa anamkataza kuwa hilo haliwezekani na eti Nakuruto anaota. Ni mawazo ambayo yanaakisiwa katika jamii tunayoishi. Wazee hawajawakubalia vijana kuchukua hatamu za uongozi kwani wanafikiria hawana uwezo wa kuongoza. Wanawaona vijana kama wasiokuwa na tajriba na maarifa ya kuhimili sekta muhimu za kiuchumi. Mawazo haya yamesababisha wazee kushikilia idara nyingi za kimsingi bila ya kuwa na maarifa mapya yanayohitajika kuziendeleza (idara) hizo mbele. Kwa upande mwingine, vijana wamejipata katika hali ngumu na kusababisha wao kujiingiza katika tabia mbovu za wizi na kuuza miili yao ili wajipatie hela za kujikimu maishani.

### 4.1.2 Ukandamizaji wa Maazimio ya Vijana

Kudzma (1998) anamfafanua kijana kama mtu yeyote mwenye umri kati ya miaka kumi na minane hadi thelathini na mitano.

Nayo, *Kamusi ya Kiswahili Sanifu,* (2004), inamfafanua kijana kama 'mtu wa makamo mwenye nguvu'.

Hapa, nitachukulia kijana kuwa mwanamume au mwanamke mwenye umri kati ya miaka kumi na minane na thelathini na mitano.

Maazimio ya vijana ni matarajio waliyonayo kuhusu kuiendeleza jamii katika nyanja mbalimbali zikiwemo uchumi na siasa. Ni matarajio yao kuwainua wanajamii wote bila kuwepo na ubaguzi wowote. Ukandamizaji wa maazimio ya vijana unatokea pale

ambapo vijana wanadhalilishwa na kuambiwa kuwa mawazo yao bado ni changa na hayafai kutajwa mbele ya watu wazima.

> …"Tujiunge nao. Nina mawaidha ya kuwafaidi," Nakuruto alimwambia (Mzee Ngocho).
>
> "Nani? Wewe? Ha! Msichana kama wewe una lipi la kuwaambia watu wale walioiva kwa ghadhabu?..."
>
> "Mtu yule atakapokamilisha hotuba yake, nitajitosa pale mbele ili name niwapasulie yaliyo moyoni mwangu. Nadhani watanisikiliza." (Maneno ya Nakuruto).
>
> "Ng'o! Hata usijaribu. Kikao hiki si cha watu wa umri mdogo kama sisi. Hutasikizwa na yeyote bali utafurushwa mbali," Ngocho alimtahadharisha. (uk 111, 112)

Ndoto za vijana zinauawa na wanasiasa na wanajamii wakongwe ambao hawaamini kuwa vijana wanaweza kuleta ukombozi wowote. Wanaonyeshwa kuwa maazimio yao hayana uhalisia wowote na kuwa ni ndoto ambazo haziwezi halisika:

> Nakuruto aliuvinjari ulimwengu wa njozi baada ya kukubali bila hiari kuingia katika mduara huu. Tofauti na uhalisi wa kilimwengu ambao sasa aliupa kisogo, ulimwengu wa kinjozi ulimtuliza ingawa ulimfanya kuwa mtazamaji na mshiriki wa matukio asiyokuwa na hiari nayo. (uk 1)

Katika dondoo hili, Nakuruto anazamishwa katika ulimwengu wa ndoto ili kuweza kutimiza matakwa ya mwandishi. Katika hali ya kawaida, ni vigumu kumuumba mhusika ambaye atatenda kama anavyotenda Nakuruto: matendo ya Nakuruto hayawezi kufanyika katika hali halisi. Hii ni kwa sababu ya jinsi jamii ilivyo. Wanajamii wameshikilia kuwa lazima kuwepo na ufisadi, uharibifu wa mazingira, taasubi ya kiume na maovu mengine ya kiuchumi na kisiasa ndiposa jamii iweze kuendelea. Yaani, ukandamizaji lazima uwepo; wanajamii hawawezi na hawafai kuwa sawa kwa vyovyote vile.

Mwandishi analazimika kutumia njozi ili kukubalisha maono ya Nakuruto kwa sababu akiwa anatenda katika hali ya kiuhalisi hatakubaliwa na wanajamii. Ni bayana kuwa, kiuhalisia, ni vigumu kuyatenda anayoyatenda Nakuruto kwa sababu jamii bado haijakubali matendo ya maendeleo ya kuibadili jamii na wanajamii kwa jumla.

Vijana wanakandamizwa hivi kwamba hata katika kutekeleza ndoto na maono yao, wanapitia magumu na changamoto chungu nzima. Wanaambiwa kuwa wao hawajui chochote kwani hawana tajriba ya maisha na hivyo basi sauti yao haifai kusikizwa. Pia changamoto hizi huwafanya wengi kukata tamaa na kujiunga na wakandamizaji.

Vijana hapa Kenya daima huambiwa watakuwa viongozi wa siku zijazo. Siku hizi hazijulikani ni lini. Na iwapo ni viongozi wazee wastaafu kwanza, basi vijana hao hawatakuwa 'vijana' tena bali wazee wakati ufikapo, na hivyo, vijana kuendelea kungoja. Lazima mawazo haya yabomolewe katika jamii na vijana wapewe fursa ya kuchukuwa hatamu za uongozi ikiwa bado wangali vijana.

Clara anatumia taswira ya pango ambazo zina wanyama na zina hali mbaya ya anga anamompitishia Nakuruto akiwa ndotoni ili kutuonyesha njia ambayo vijana hupitia ili kutimiza maono yao:

> Akiwa katika hali hii (hali ya ndoto), Nakuruto alihisi nguvu fulani ikimsukasuka vibaya sana, kisha ikamwinua na kumpa raha ya mfyatuko kama wa tai anayeruka na kupaa angani. Hakuwa na mbawa lakini alianza kupaa kwa kasi ajabu. Katika kupaa huko, alihisi kama anayepitishwa ndani ya upenyu wa giza, kama mtu anayefukuza wakati kinyume ili kubaini chanzo chake… Ghafla bin vuu, alihisi kama anayepitishwa ndani ya mapango ya kale. Mapango hayo yalionekana kama yaliyofunua vinywa kumpokea. Akimezwa na pango moja, jingine lenye jinywa kubwa hujitoma mbele yake na kummeza. (uk 2)

Taswira ya pango inatumika kuonyesha pandashuka za maisha ya kijana katika jamii katika kutekeleza maono yake. Wakati mwingine hujipata amepata mbawa za kufanya

jambo lakini dhoruba za maisha zinamzungusha hadi anapoteza matumaini. Mapango yanafananishwa na wazee ambao wanawadunisha vijana. Wazee hawa 'huwafinya' ili wasiweze kujiinua kimaarifa na kusababisha vijana hawa kujidharau na kutojiamini hata wanapofanya kazi zao wenyewe.

Humu nchini Kenya, vijana wengi wamejiingiza katika vikundi vya ulaghai na hata vya kigaidi kwa sababu wamenyimwa nafasi serikalini na katika sekta mbali mbali za kiuchumi. Katika kaunti ya Mandera, Garissa, Mombasa na hata Lamu, vijana wengi wamejiunga na kikundi cha kigaidi cha Al Shabaab (*Daily Nation, June 19, 2015).* Imewalazimu maafisa wa serikali ya kaunti kuingilia kati na kuanza kuwarai vijana kutojiunga na kundi hili haramu.

Katika kaunti zingine humu nchini, vijana walionyimwa nafasi ya kuchangia katika maendeleo wanatumika na wanasiasa ili kuendeleza vita vya kikabila katika jamii mbali mbali (*The Standard, June 22, 2015*). Mwandishi wa makala hii, Mohamed Guleid, anasema vijana wa maeneo ya Kaskazini mwa nchi wameachwa bila kushirikishwa katika maendeleo na hivyo basi kubaki bila kazi yoyote. Wanatumia muda wao kuiba mifugo kutoka kwa jamii jirani.

Mapango haya pia yanasheheni taasubi za kiume. Clara anavuta hisia kuwa mhusika mkuu ambaye ni mwanamke-msichana, ndiye anayekandamizwa na 'mapango' haya na hivyo basi kuzua swala la jinsia. Hali ya jinsia huenda inazikwa kwa sababu Nakuruto anawakilisha vijana kwa jumla wala si vijana wa kike pekee; yaani, anawakilisha vijana wanawake na wanaume.
Hata hivyo, tunaweza kusema kuwa Nakuruto anawakilisha vijana-wasichana kwa sababu kuna matukio ambayo wanajamii wanamrejelea na kumuona kama 'msichana' bali si kama kijana mvulana:

> Walipokuwa wakipita kijijini, watu walipigwa na mshangao kumwona shaibu yule akiandamana na msichana aliyevalia kinguzu kama mmoja wa matajiri watawala wa mahali pale. Walipita katikati ya vijumba vya udongo huku macho ya wenyeji yakiwatazama kwa mshangao. Walipishana na watoto waliovaa mararu, wengine wakicheza kando ya njia na kutifua vumbi la hudhurungi. Walipishana na akina mama waliobeba matita ya kuni, magunia ya makaa na ndoo zilizoshiba mchanga. Wengine walisimama kuwatazama watu hao wawili waliotofautiana kiumri na kihali. (uk 63)

Katika dondoo hili, Nakuruto alikuwa anatembea na Mzee Saluda ili akaonyeshwe kwa Chifu Mfumwa. Wanakijiji wanashangaa na kuwatazama huku wakijiuliza ikiwa Mzee Saluda amejinyakulia 'kamwana'. Wanakijiji wanamuona Nakuruto kama msichana wala si kama kijana. Pia, wanamuona kama tajiri na hivyo kumchukulia kama mkandamizaji. Hata hivyo, baadaye wanagundua kuwa yeye ni mmoja wao. Hawamthamini na hata kabla hawajajua kiini cha 'matembezi' yao, washamhukumu tayari! Wanamtazama kama 'kijana-msichana' wala si kama 'msichana-kijana'.

Nakuruto anachukuwa maumbo tofauti tofauti akipania kutekeleza majukumu mengi bila kuleta uhasama wa kisaikolojia wowote na wanajamii. Wakati mwingine anachukuwa umbo la mwanamke mkongwe ili aweze kupitisha ujumbe fulani kwa hadhira husika riwayani na wakati mwingine anaumbwa kama msichana mrembo ili aweze kuifikia hadhira lengwa:

> Nakuruto alifungua mkoba wake lakini wakati huu hakushika kile kishajara bali alichomoa kioo na kujitazama usoni. Sura aliyoiona mbele yake ilimfanya kutabasamu kwani kabadilika si haba. Alikuwa msichana mrembo mwenye uso uliobainisha bashasha ya ujana.
> (uk 77)

Mwandishi amelenga wanajamii ambao hawangemthamini mhusika mkongwe na ndiposa Nakuruto akageuzwa kuwa msichana mrembo. Nakuruto anapoelekea kijiji cha Ipe, anabadilishwa na kuwa mama mkongwe ili kuonyesha jinsi tamaduni na desturi za wanajamii zilivyodorora kutokana na uchafuzi wa mazingira:

> …Alipokuwa akiwazia hili, alitahamaki anashukishwa chini kwa kasi ya ajabu. Kasi hii ilimfanya ahisi kutapika… Akahisi tumbo linamsokota. Polepole likaanza kufura. Akahisi kama ngozi ya mwili wake imevamiwa na mamilioni ya buibui…
>
> Lakini lililomshtua zaidi ni pale alipotazama mikono yake ambayo sasa ilisinyaa kama magome ya mti. Ngozi ilikuwa imesinyaa kama ya kikongwe… Alipojishika uso, alihisi una makunyazi na mikunjo ya uzee.
>
> 'Mama yangu mie! Nimekuwa mkongwe hivi?' … (uk 8, 9)

Anakatazwa kumshika mtoto wa Nariangai binti Nganda ili kuonyeshwa ukatili wa ukandamizaji wa mazingira. Mazingira yameharibiwa na wanajamii wanatumia mbinu mbadala kujitafutia riziki. Mojawapo ni ya kuiba watoto na kuwauza. Hivyo basi, Nariangai binti Nganda anaogopa kumpa Nakuruto mtoto wake kwa kuhofia mtoto wake asiibiwe. Clara anapotaka kuonyesha jinsi nta ilivyowaharibu wanajamii wa kizazi kipya, anambadilisha Nakuruto, anakuwa msichana mrembo ili aweze 'kuuelewa' muktadha wa *disco* wakiwa na kijana Leboni. Leboni anamtembeza Nakuruto katika vilabu ambapo wanaona watu wakifanya kila aina ya maovu: ukahaba, ulevi, na utumizi wa dawa za kulevya.

'Mtoto wa kike' anachukuliwa kuwa asiye na uwezo wa kuchangia katika maswala ya jamii. Ananyimwa nafasi ya kuchangia kwa maendeleo ya jamii. Nakuruto, akiwa amechukuwa umbo la msichana, anajiunga na wanajamii katika kumwondoa bwana Wellingtone kutoka kwa mashamba yao. Anawahamasisha wanajamii na kumfurusha mnguzu huyo lakini hata baada ya kuondoka, bado wanajamii wanazidi kuteseka. Baadaye tena, wanakuja pamoja na kuanza kulaani 'msichana wa kike' aliyewavuruga. Wanasema:

> Nilijua …nilijua mimi. Msichana yule alikuwa kizuka. Kisirani yule alitutoa kikaangoni na kututia motoni… Watoto wetu wanakufa njaa, hakuna chakula. Je tutakula hayo malighafi? Haya yote yametokana na kuzingatia mawazo ya mtoto mdogo tu wa kike anayeota ndoto. Lakini tangu lini jamii hii ikamruhusu mtoto wa kike kuongea mbele ya kaumu ya wazee? (uk 70)

Nakuruto anakashifiwa na wanajamii kwa matatizo wanayokumbana nayo baada ya kumfurusha mnguzu Wellingtone. Hata ikiwa wao ndio waliokuwa na uzembe wa kufanya kazi, lawama inamwendea msichana! Wanadai kuwa 'mtoto wa kike' hafai hata kuruhusiwa kuongea mbele ya wanajamii kwani ni kinyume na tamaduni. Katika hali halisi humu nchini Kenya, hata baada ya kuondoka kwa wakoloni, tumebakia na uongozi mbaya uliokithiri ukabila na ufisadi kupelekea uzorotaji wa uchumi. Waliochukuwa hatamu kutoka kwa wakoloni walikuwa na tamaa nyingi sana ya pesa na rasilmali. Walisahau wananchi, na uongozi wao ukazorotesha maisha ya wanajamii.

Katika jamii ya Abagusii kwa mfano, msichana anachukuliwa kama kiumbe ambaye anafaa kuwa jikoni na kufanya kazi za kinyumbani. Msichana, hususan katika maeneo yaliyo mbali na miji mikuu, wanadharauliwa na wakati mwingine, wao hualazimishwa kuacha shule ili waolewe (mtafiti anatoka jamii hii). Japo hivyo, kupitia elimu na kampeni zingine kutoka kwa serikali na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, wanajamii wanazidi kuzinduliwa kutoka na desturi hizo potovu.

Katika eneo la Bonde la Ufa, msichana wa umri wa miaka ishirini (20) alitembea zaidi ya kilomita hamsini (50) ili kujinusuru kutokana na ndoa ya lazima aliyokuwa amepangiwa na wazazi wake (*The Standard June 22, 2015*). Alikuwa katika kidato cha tatu lakini wazazi wake wakapendekeza wamuoze. Hii ni kwa mujibu wa mila zao ambazo zinawapa wazazi uhuru na ruhusa ya kuwatafutia watoto wao wachumba. Mara nyingi hili hufanyika ili kujipa mali na kukidhi mahitaji ya mila na desturi za jamii. Hatimaye, afisa wa Nakuru anayesimamia watoto aliahidi kuchunguza zaidi na kuwashtaki waliohusika.

### 4.1.3 Ukandamizaji wa Mazingira

Mazingira, kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, TUKI* (2004), ni hali au mambo yaliyomzunguka kiumbe katika sehemu au maisha yake.

Kamusi ya *Oxford Advanced Learners* (2010), inafafanua mazingira kama hali zinazoathiri tabia na maendeleo ya mtu, wanyama au vitu. Inaendelea kufafanua kuwa ni hali zinazoonekana na kuhisiwa na watu, wanyama au vitu visivyo na uhai.

Hivyo basi, mazingira ni hali zozote zile zinazomwathiri binadamu, mnyama au vitu visivyo na uhai kama miti. Mazingira ni uhai wa viumbe vyote: vilivyo na visivyo na uhai. Kwa hivyo, mazingira ni mle tunamoishi na yote ndani yake ikiwemo ardhi, maji, hewa, misitu, nyumba, wanyama, viwanda, barabara, magari na vyote vilivyomo ulimwenguni humu. Riwayani, mwandishi ameliangazia kwa upana, kupitia wahusika, swala la uharibifu wa mazingira.

Mazingira huweza kukandamizwa kwa kutotunzwa vyema na binadamu. Kwa mfano, kukatakata miti kiholela ni kukandamiza mazingira. Pia, kutupa takataka mahali pasipofaa, kumwaga maji taka au kemikali kutoka viwandani katika mito na kulima mashamba kwa jinsi inayosababisha mmomonyoko wa udongo ni ukandamizaji wa mazingira.

Matukio yote kwenye kisa yanazunguka mazingira kwa njia moja au nyingine. Mwandishi anamtumia Nakuruto kupiga vita uharibifu wa mazingira. Nakuruto anapinga hatua za mwanajamii ambaye anaonekana kuwa na ugumu wa kuyafuata maagizo ya kuhifadhi mazingira.

Ukandamizaji huu umezungumziwa na mwandishi huyu mwanamke kwa njia pana na inayogusa moyo. Japo wosia wake ni wa maana ukitumika, ni muhimu kutambua kuwa

wanajamii katika ulimwengu wa Nakuruto, wanashindwa kuutekeleza wosia huo na hata kuukataa:

> "Ole wetu wanavijiji, nta ya Quick Buck imetuvua uasili wetu, ikatuvisha ubinafsi na kutuacha tuning'inie katika wavu tusioelewa ufumaji wake," Nakuruto alilalama
>
> "Ewaa! Mkiritimba huyo kajijengea wavu mpana kisha yeye huishi katikati ya wavu huo akiwa amezungukwa na nta…" alieleza Leboni huku akionekana mwenye kughadhabika.
>
> "Nitabadilisha mambo," alitamka Nakuruto kwa sauti ya juu.
>
> "Hebu tusiambiane uongo hapa," Leboni alimwambia, "Ni mustahili kushindana na upepo wa mabadiliko. Kufanya hivyo, ni sawa na kutwanga maji kwa kinu. Utaumia bure chaurembo." (uk 82)

Maneno haya yanatamkwa na Mzee Leboni baada ya Nakuruto kumwarifu kuhusu suluhisho la vurumai iliyokuwa inakumba kijiji chao. Anamwarifu kuwa ubinafsi wa baadhi ya wanavijiji ndio umewafanya wanakijiji wote kuteseka. Ni hapo anapokataa mapendekezo ya Nakuruto ya kusuluhisha matatizo yao kama tu wafanyavyo wanakijiji wengine, hivyo mazingira kuendelea kuharibiwa na kuzidi kuzorota.

Katika sura ya pili, baada ya Nakuruto kufanya muujiza wa kuumba ziwa na mto, anapeperushwa kutoka sehemu hiyo lakini anarudishwa baadaye ili kujionea hali ilivyoimarika kimazingira. Anashangazwa na anachokiona kwani ni kinyume na alivyotarajia. Anawaona wanajamii wakichafua maji ya ziwa Nakuruto, anakasirishwa sana na tendo hili na anatamani adondoshwe chini ili awaadhibu:

> Nakuruto aliweza pia kuwaona watu wakiloa samaki, lakini wengine walimghadhabisha kwani walitupa maji taka humo ziwani baada ya kufua nguo au kuoga. Alitamani adondoshwe na nguvu ile ili aende kuwazuia kutekeleza uchafuzi huo. (uk 28)

Uchafuzi huu unafanyika baada ya Nakuruto kuliumba ziwa ambalo alitarajia litakuwa ni neema kwa wanajamii wote. Wanajamii wanachafua ziwa hili kwa kumwaga maji-

taka. Maji-taka yanafanya maji kuchafuka na kuwa kisababishi cha magonjwa mengi katika jamii mfano, kipindupindu. Hivyo, Clara kupitia kwa Nakuruto, anaonyesha jinsi wanadamu wanavyoharibu mazingira yao na anaonya jamii dhidi ya uchafuzi wa maji unaohatarisha maisha yao.

Nchini Kenya kumekuwa na uchafuzi wa mazingira katika sehemu mbali mbali. Katika kaunti ya Laikipia, mashamba ya maua yanadaiwa kumwaga kemikali kali katika mito ambayo wananchi watumia maji yake (*Daily Nation, June 30 2015*). Maafisa wa mazingira wa kaunti hiyo wanachunguza baadhi ya mashamba hayo ili kubaini chanzo cha uchafuzi huo ikiwa ni kemikali kutoka mashamba hayo. Hata hivyo, wanaoishi katika eneo hilo wanadai kuwa baadhi ya maafisa wanaoshughulika na kuhifadhi mazingira wamepuuza vilio vyao na huenda wamepewa hongo ili kunyamaza.

Pia, miti katika misitu inaendelea kukatwa na wananchi bila ya idhini ya serikali. Katika kaunti ya Kirinyaga, zaidi ya watu kumi wa wanne walikamatwa na polisi na kufikishwa mahakamani ili kujibu mashtaka ya kukata miti bila ilani katika misitu (*Daily Nation, June 25, 2015)*. Hii ni mifano michache tu ya uchafuzi wa mazingira nchini Kenya. Mambo haya ndiyo yanayoangaziwa na Clara kupitia mhusika Nakuruto na kutahadharisha jamii athari yake. Matokeo haya huathiri vibaya jamii.

#### 4.1.3.1 Athari za ukandamizaji wa Mazingira

Athari za uchafuzi wa mazingira ni bayana, na kuna zile ambazo zimefichika na haziwezi kutambulika kwa urahisi. Athari zinazoweza kujulikana kwa urahishi ni zile ambazo zinaonekana punde tu uchafuzi huo unapofanyika. Uchafuzi wa hewa, maji machafu na mafuriko ni baadhi ya athari zinazoonekana kwa urahisi. Ukame, mvua kupungua na kubadilika kwa hali ya anga ni baadhi ya athari zinazoonekana baada ya muda.

### a) Vifo

Athari mojawapo ni kifo. Mazingira duni yaliyochafuka huweza kusababisha vifo vya binadamu, wanyama pori na hata mimea. Mimea hukauka, hivyo basi kufa, kwa sababu ya kemikali au ukosefu wa maji.

> "Mzee Saluda, naifahamu historia yote ya Maweni. Sikuambiwa wala sikuisoma. Naelewa kwamba wenyeji wake wanaishi katika ardhi kame, ardhi yabisi kama tumbo la tasa. Wamesukumwa hadi ukingoni mwa maangamizi wakaharibu udongo uliohimili uzao wao tangu azali. Nataka kuwarudishia watu hawa ardhi na utu wao. Hii itawafanya waishi tena, wakifurahia asili ya chimbuko lao." (uk 61)

Katika dondoo hili, Nakuruto anaongea na Mzee Saluda, ambaye ni mmojawapo wa viongozi wa wanajamii wa Maweni, kuhusu uharibifu uliosababishwa na Wanguzu. Anamhakikishia kuwa yeye Nakuruto, atawasaidia kuuleta uhai wa mimea na utu kama ilivyokuwa hapo mbeleni. Tunatambua kuwa baadhi ya mimea imekauka na kusababisha njaa ambayo imeleta vifo ndiposa Nakuruto anawahakikishia kuwa wataishi tena ikiwa watapigania haki yao kutoka kwa Wanguzu.

### b) Mafuriko

Katika ukurasa wa ishirini na tatu (23), kabla ya Nakuruto kuliumba ziwa, anatoa masharti ya kufuatwa kabla ya ziwa hilo kuwepo. Anawaarifu wanakijiji kuwa kutakuwa na mtetemeko wa ardhi na kuwa yeyote asitoke nje pindi ukitokea na ambaye angethubutu kutoka, angekufa papo hapo. Haya yote ni ishara ya athari za uchafuzi wa mazingira. Ili kuwepo na ukombozi wa mazingira, lazima kuwe na majeruhi. Kulipopambazuka, kuna wanakajiji ambao walikuwa wamemezwa na 'ukombozi' huo:

> "…wako wapi akina…akina… Ha! Sitowataja majina. Nashelengai, njoo uone wamedidimia wote. Mtaa umegeuka kuwa bahari nyeupe pe pe pe." Alisema Mzee Kikuete, bwanake Nashelengai.
>
> Kwa mbali, waliwasikia majirani wakimaka ovyo. Wengine walipiga mbinja ilhali wengine walipiga mayowe hususan ilipowabainikia kuwa majirani zao wa mtaa wa kati hawako tena. (uk 24)

Dondoo hili linaonyesha athari ya uchafuzi wa mazingira uliosababisha mvua ya kupita kiasi na kuleta gharika. Hewa angani inapoharibiwa na kemikali, mvua ya gharika hunyesha, na athari zake ni hasi mno kwa mwanadamu na wanyama.

### c) Ukame na njaa

Athari nyingine ni kuwepo na ukame na njaa ambayo kwa njia moja au nyingine huleta uhasama baina ya binadamu. Mfano mzuri hai, ni katika jamii za Pokot na Turkana, sehemu za Kaskazini ya Kenya. Wao hupigana daima kwa kung'ang'ania maji na chakula cha mifugo wao (*The Standard June 22*, *2015*). Katika riwaya ya Nakuruto, athari hii inaonyeshwa hivi:

> Nakuruto anarudi kijiji cha Walatimbi na anashangazwa na hali ilivyo. Anakumbana na ardhi iliyoharibiwa na mazingira kuchafuliwa na wanakijiji wakishirikiana na Quick Buck.
>
> Alijihisi kuwa mwingi wa simanzi, akawa kama mzazi aliyefadhaishwa na mienendo potovu ya wanawe. Alijihisi kuwa pweke katika mapambano ya kuirutubisha ardhi ili iweze kutoa mazao asilia tena. Alihisi kitete hasa lilipomjia wazo kuwa mashindano hayo ya kuisaka nta huenda yakaiyumbisha sayari ya pekee iliyohimili uhai wa wanavijiji. Uharibifu wa mali asili katika sakata ya kuimiliki nta ulielekea kuitia sayari waliyotunukiwa na Muumba wao uyabisi ishindwe kuzalisha na kuhimili uhai wa viumbe. (uk 104)
>
> Lakini hakuamini macho yake alipotazama mbele yake na kukumbana na gugumaji lililoota na kugubika nusu ya lile ziwa. Aliona pia watu wawili wakiwa mtumbwini ndani ya ziwa wakielekea upande wake. Ziwa lilionekana kama lililohamwa na wanakijiji…
>
> …Wavuvi walipofika ufuoni, waliegesha mtumbwi wao. Nakuruto aliwatazama akaona nyuso zilizokosa matumaini. Walitupa nje nyavu zao pamoja na makapu yakiwa matupu. (uk 105)
>
> "Ziwa hili halitoi samaki siku hizi? Naona mmeambulia dagaa tu."
>
> "Ah! Samaki watoke wapi dadangu. Gugumaji linatatiza uvuvi na samaki wamehama. Ukame ndio huu. Maji yamepungua mno, samaki watoke wapi?" alilalama Ba Ludao. (uk 106)

Tunaona uchafuzi wa mazingira ukisababisha ziwa kukauka na kusababisha mito kukauka na hatimaye kuleta njaa. Clara ameliangalia suala hili katika riwaya yake kama fasihi lakini lipo katika hali halisi ya maisha ulimwenguni.

Nakuruto, akiwa amechukua umbo la mwanamke mkongwe, anaenda kwenye boma moja la mama anayeitwa Nariangai binti Nganda. Anaomba amshike mtoto wake kama ilivyo desturi, lakini bibi huyu anakataa kwa sababu Nakuruto anavyoonekana, amechakaa. Ukosefu wa hela unamfanya mama yule kumpa bikizee Nakuruto nyama mbichi kwani hakuwa na moto wa kuipikia. Pia, anampa nyama iliyooza kwa sababu hakuna chakula. Japo huenda ikawa ni ukweli kuwa hakuwa na moto, ubaridi wa mama yule unatokana na kiangazi ambacho kimeukumba mtaa ule. Nariangai binti Nganda anasikitishwa na ukame uliopo katika kijiji chao na kwa hivyo hana furaha ya kumpokea na kumtunza Nakuruto. Kiangazi hiki kilitokana na uchafuzi wa mazingira.

Mama Nariangai anaendeleza hujuma yake kwa Nakuruto. Alipokuwa anatoka, Nariangai anamtusi Nakuruto kuonyesha chuki aliyokuwa nayo dhidi yake:

> ‘Ebo! Ana nini ajuza yule? Ataka nimpe mwanangu mchanga amtie dege? Ati anataka chakula! Huko atokako hana wa kumpikia mpaka afuuze mwangu nyumbani? Kisirani gani hiki. Sijui kaibukia mavani au wapi msukumizi yule’, Nariangai alijisemea moyoni. (uk 13-14)

Ukosefu wa chakula uliwakumba wanajamii wote kutokana na uhaba wa mvua kwa sababu ya uchafuzi wa mazingira. Njaa hii iliwafanya wanajamii kukosa ukarimu na kuwa wachoyo. Wageni walinyimwa chakula kila mtu akiwa na ubinafsi.

Uhusiano kati ya ubaridi wa Nariangai na ukosefu wa chakula na uchafuzi wa mazingira unadhihirika hatimaye katika ukurasa wa kumi na tano (15), Nakuruto anapoelekea mtaa wa pili. Hapa, anamkuta mama ambaye, kinyume na yule wa kwanza, anamkaribisha kwa bashasha na kabla hata aitishwe mtoto, mama huyu anamletea

Nakuruto kitoto chake akishike; kama ilivyokuwa desturi. Baada ya gumzo na mama Nashelengai binti Ngonde na kugundua ukarimu wake, Nakuruto anasema:

> …Nawafahamu watu hao. Mzee Magonji tuliishi naye katika kijiji kimoja zamani. Hakukuwa na ukame kama siku hizi. Vyakula viligombania nafasi katika maghala na mvua zilinyesha kila wakati. Leo mvua itoke wapi ikiwa wakongwe wanalishwa viunga wana wa ng'ombe? (uk 14-15)

Uchafuzi wa mazingira unasababisha ukame ambao unafilisisha maghala na kusababisha uhasama baina ya wanajamii. Uhasama huu husababisha ubahili na uchoyo ambao pia huifanya jamii kulaaniwa. Pia, baada ya Nakuruto kufanya muujiza wa kuliumba ziwa na mto, wanakijiji hawa bado wanaendelea na uchafuzi huo wa uhai. Wameshasahau kuwa ukandamizaji huo huo ndio awali ulikuwa umewafanya wateseke na kiangazi na hatimaye njaa.

Nchini Kenya kumekuwepo na visa vingi vya vifo na njaa vinavyotokana na uchafuzi wa mazingira. Mnamo Februari mwaka wa 2015, zaidi ya shule ishirini (20) zilitarajiwa kufungwa kwa sababu ya njaa iliyosababishwa na ukame katika eneo la Pokot Magharibi na Turkana. Wanafunzi kutoka shule hizo wanakosa kufika shuleni kwa sababu ya ukosefu wa chakula na maji unaosababishwa na ukandamizaji wa mazingira. Pia, ukame huu umesababisha jamii mbali mbali kuhamia sehemu zingine ili kutafutia mifugo wao chakula, hatua ambayo inasabisha kuwe na tumbojoto kati ya jamii mbili zinazohusika kwani nyasi na maji ya mifugo hao haziwezi kuwatosha mifugo wa jamii hizi mbili. Hatimaye, jamii hizi hupigana na kusababisha vifo na upweke kwa wajane na watoto watakaopoteza w;aume wao.

### 4.1.4 Ukandamizaji kutoka kwa Serikali

Serikali zinakandamiza wananchi kwa kuwanyima nafasi ya kujieleza wazi wazi. Wananchi hawapewi uhuru wa kutoa maoni au kujieleza au kujitetea. Mara nyingi serikali hutumia rungu la dola kuwanyamazisha wananchi wanaopinga dhuluma au unyanyasaji. Huenda wakawekwa korokoroni kwa muda mrefu bila kufunguliwa mashtaka au kushtakiwa kwa mashtaka bandia na kufungwa jela na hivyo kuwanyima wananchi fursa ya kujieleza ambayo ni haki ya kibinadamu na demokrasia. Pia, serikali zinaendeleza ukandamizaji kwa kuwaruhusu mabwanyenye kuwanyanyasa wananchi kwa kufuja mali ya umma na kuweka sera mbaya zinazoumiza uchumi wa nchi na maendeleo ya miradi mbali mbali. Mabwanyenye hawa aghalabu hupewa nafasi ya kufanya wapendavyo. Mfano ni pale ambapo wananyakua ardhi ya umma na kudai wanaleta maendeleo na kuwaacha wanachi wa kawaida bila ardhi.

#### 4.1.4.1 Unyakuzi wa Ardhi

Aina hii ya ukandamizaji inajitokeza katika sura ya nne ambapo Clara, kupitia kwa mhusika Nakuruto, anatueleza jinsi sera mbaya zilizotungwa na kutekelezwa na serikali zilivyowafukarisha wanakijiji wa Maweni.

Tunaelezwa kuwa watawala wa nchi ndio waliosukumiza sera hizo kwa wanakijiji bila kuwahusisha hata kidogo. Aaendelea kusema kuwa sera hizo ziliwafanya wanakijiji hao daima kuwatunukia wachache waliojizolea mamlaka. Nakuruto anakumbuka jinsi kijiji cha Maweni kilivyokuwa:

> Naam, kile pale kijiji cha Maweni. Pale ambapo walipotoka vibarua wengi kwenda kupalilia konde za kwetu. Watu wa Maweni walifukarishwa mno na sera za watawala zilizoghoshi ubinafsi mkubwa... Mabarakala wale waliishi kunyonya jasho la Wamaweni huku wakistarehe kwa mvinyo na vyakula vya kuchagua. Kisha walipasua vicheko huku wakicheka kwe kwe kwe! (uk 53)

Ukandamizaji huu unasabisha mateso kwa wanajamii. Utajiri ambao ulifaa kuwa wao haumo mikononi mwao na hivyo basi hawana uwezo wa kuzalisha mali. Unyanyasaji huu hujitokeza katika jamii nyingi hususan barani Afrika, na huendelezwa na mabwanyenye ili kujilimbikizia mali kwa njia isiyo halali: kuwanyonya vibarua wanaowafanyia kazi kwa kuwafanyiza kazi nyingi na malipo duni:

> Mabarakala wale waliishi kunyonya jasho la Wamaweni huku wakistarehe kwa mvinyo na vyakula vya kuchagua…Joto hili linalochoma ni ishara ya uharibifu wa mali asili. Ardhi iliyomilikiwa na wachache sasa imekuwa yabisi kwa kufujwa na wanyonyaji wale. (uk 53)

Sera hizo, kwa mujibu wa Clara kupitia kwa mhusika Nakuruto, ndizo zimesababisha kuwepo kwa majanga mengi kwa wanajamii; njaa, ukame, umaskini na uchafuzi wa hewa.

Mfano, katika kaunti ya Nairobi, zaidi ya ekari hamsini za ardhi ya umma ziliibwa na mabwanyenye na kuandikishwa kama za kibinafsi (*The Standard, June 25, 2015*). Ardhi hiyo iliyo chini ya hifadhi ya shirika la ndege, inasemekana kununuliwa na mabwanyenye fulani na kuandikishwa kama ardhi ya kibinafsi.

Vilevile, katika kaunti ya Nakuru, wanasiasa ambao walitaka kulinyakua shamba la umma waliamriwa na korti kutoingilia masuala ya shamba hilo hadi korti iamue ni nani ambaye ni mmiliki halisi wa kipande hicho cha ardhi (*The Standard, June 18, 2015*).

Athari za unyanyasaji huu huonekana hata kuwafikia wanyanyasaji wenyewe. Mmoja wa mkurugenzi wa kampuni ya ununuzi wa mashamba ya Kihiu Mwiri, alipigwa risasi na kufariki papo hapo kwa kile kinachodaiwa kuwa vita kati ya wanachama kuhusu ugavi wa mashamba yanayomilikiwa na kampuni hiyo (*Daily Nation, June 30 2015*). Kwa sababu ya tamaa, zaidi ya wakurugenzi saba wa kampuni hiyo wameuawa. Haya

ni masuala ya unyakuzi wa ardhi ya wanyonge ama ya umma. Jambo hili linapotokea, wananchi wengi hukosa ardhi na kuwa maskwota. Unyanyasaji wa kupitia ardhi ndio Clara anauelezea kupitia mhusika Nakuruto. Suala hili la unyakuzi wa ardhi ni nyeti hapa nchini Kenya na Clara amelieleza wazi wazi katika riwaya hii ya *Nakuruto*.

**4.1.4.2 Ufisadi**

Kwa maoni yangu, ufisadi ni hali ya kupokea mlungula au kitu chochote kile ili kupata huduma usizostahili kupewa. Yaani, unamnyanganya mwenzako anachostahili kupewa kisha unakichukua. Aghalabu, huwa ni pesa zinazobadilishana mikono.

Katika riwaya, wanakijiji wa Maboni wanakubaliana kujenga ukuta wa kuwawezesha kuifikia nta. Waliafikiana kuhusu ujenzi huu baada ya malumbano mengi miongoni mwa wanakijiji. Wanapoanza ujenzi, wizi wa bidhaa za ujenzi unaanza na hatimaye udanganyifu kutoka upande wa mafundi unakithiri. Baadhi ya bidhaa zinaandikwa kuwa zimenunuliwa lakini hazionekani zimetumika wapi:

> Wale waliopewa kandarasi ya kuleta mchanga na kokoto mahali pa ujenzi walianza kuiba bidhaa hizo kutoka kwenye malori. Madereva wa magari hayo walipakia mchanga lakini badala ya kuupeleka mahali pa ujenzi, waliupeleka kuwauzia watu binafsi. Ujenzi ngazi ukachelewa kuanza kwa sababu hii. Lakini kati ya bidhaa zilizoibiwa, hakuna iliyofisidiwa kama simiti. Malori yalipakia simiti hadi pomoni lakini yalipofika mahali pa ujenzi, yalikuwa na bidhaa nusu. (uk 123, 124)

Katika hali halisi, ufisadi ni mojawapo ya unyanyasaji ambao umekuwa ukiendelea kwa muda nchini Kenya na ulimwenguni. Nchini Kenya, kumekuwepo na visa vingi ambapo mwananchi wa kawaida ananyanyaswa na matajiri na wanasiasa kwa kunyang'anywa kilicho chake. Katika kaunti ya Vihiga, wagonjwa ishirini na wawili walifariki baada ya kuugua na kukosa dawa hospitalini. Wagonjwa walifariki kwa kukosa dawa zilizoibwa na baadhi ya maafisa wa afya katika kaunti hiyo (*Daily Nation, June 25, 2015*).

Kwingineko, katika kaunti ya Tharaka-Nithi, zaidi ya shilingi milioni mia nne na tisini na tano (Ksh. 495,000,000) zilifujwa na baadhi ya maafisa wa kaunti (*Daily Nation, June 19, 2015*). Inadaiwa kuwa pesa hizo zilikuwa za maendeleo lakini hakuna miradi yoyote ambayo ilikuwa imeanzishwa katika kaunti hiyo, na kuna uwezekano mkubwa kuwa pesa hizo ziliishia mikononi mwa maafisa wachache wa kaunti. Tume ya kuchunguza ufisadi nchini Kenya, Tume ya Maadili na Kuchunguza Ufisadi (EACC-Ethics and Anti-Corruption Commision) iliahidi kuanzisha uchunguzi dhidi ya maafisa hao na ikiwa watapatikana na makossa, watashtakiwa.

Pia, katika sekta ya wafanyakazi wa serikali, maafisa wakuu wa polisi wanawanyanyasa maafisa wadogo kwa kuwalaghai marupurupu yao (*The Standard, June 20, 2015*). Hii ni desturi katika Idara ya Polisi ambapo maafisa wadogo hutumiwa kama watumwa na maafisa wengine wakuu idarani bila kujali haki zao. Maafisa hawa hufanyishwa kazi nje ya haki zao za kazi. Huosha magari ya 'wakubwa' wao kinyume cha sheria za Kenya.

### 4.1.5 Ukandamizaji wa Mwanamke

Kudzma (1998) anasema kuwa mwanamke ni binadamu wa kike ambaye anazidi umri wa miaka thelathini na tano.

Kwa maoni yangu, mwanamke ni binadamu yeyote wa kike ambaye ana zaidi ya miaka thelathini na mitano na ambaye ameolewa.

Ukandamizaji wa mwanamke hutokea wakati ambapo mwanajamii wa kike anadhulumiwa na wanajamii wengine ama wa jinsia ya kiume au ya kike. Pia, ukandamizaji huu hutokea kila mwanamke anaponyimwa nafasi kwa sababu ya jinsia yake. Yaani kwa mfano, mwanamke huenda akanyimwa kazi ya kuwa mlinzi kwa

sababu wanadhani kuwa hataweza kukabiliana na wahalifu. Sababu yao ni kuwa, mwanamke hawezi kuwa na uwezo wa kimwili wa kukabiliana nao.

Mhusika Nakuruto anawakilisha wanawake na wasichana-vijana au vijana wa kike. Anachukuwa maumbo tofauti tofauti akipania kutekeleza majukumu mengi bila kuleta uhasama wa kisaikolojia wowote na wanajamii. Wakati mwingine anachukua umbo la mwanamke mkongwe ili aweze kupitisha ujumbe fulani kwa hadhira husika riwayani. Clara ameonyesha ukandamizaji wa mwanamke kutoka kwa wanaume na vile vile kutoka kwa wanawake wenyewe.

#### 4.1.5.1 Ukandamizaji wa Mwanamke kutoka kwa Mwanamume

Mwanamume huweza kumkandamizia mwanamke kwa njia mbalimbali. Mara nyingi, ukandamizaji huu huwa na makali ya taasubi za kiume. Mwanamume akimdharau mwanamke kwa misingi ya jinsia, basi huwa tunakuwa na ukandamizaji wa aina hii.

Riwayani, wanakijiji wa Maboni, ambapo pepo za magharibi zilikuwa zimetuama, waliamua kujenga nyenzo ili kuifikia nta. Wanaume wanawekwa mbele katika kuujenga uwenzo huo. Kurunzi ilihitajika kupelekewa wale wajenzi waliokuwa juu ya mnara wakiendeleza ujenzi. Bw. Bullyson alidai kuwa atatumia watu wake kuipandisha kurunzi lakini wanakijiji walikataa wazo hilo. Lakini pale ambapo mwanamke, Sheshije, alidai kuwa anaweza kuipandisha, alikemewa huku akiambiwa kuwa nafasi ya mwanamke ni nyumbani:

> Mwanamke milki yake ni nyumbani sio mahali kama hapa. (uk 132)

Swala hilo linazua mjadala japo hatimaye mwanamke anaruhusiwa kupanda. Sheshije anaviparaja vidato vya ngazi. Mara tu anapoanza kuukwea mnara, wanaume walio karibu wanaanza kupiga vidoko, baadhi ya wanawake wakimtusi huku wengine wakimshangilia. Wanapiga vidoko kwa sababu hawathamini mwanamke kuupanda

mnara. Wanamuona kama kiumbe dhaifu ambacho hakifai kufanya kazi fulani zilizotengewa kufanywa na wanaume. Na hata baada kumruhusu kupanda, wanampa masharti ya jinsi atakavyovaa anapopanda mnara huo:

> Wanaume wengine alipiga vidoko na kumtusi ilhali wachache wao wakimshajiisha azidi kupanda. Wanawake wachache pia waliokuwa mahali pale walimhimiza apande. Punde si punde, sauti kali ikamshtua Sheshije.
> "Hapana. Huwezi kupanda hivyo. Lazima uvae suruali kwani kuna upepo mkali huko juu." (uk 134)

Maneno haya yanatamkwa na mwanamke ambaye anamwarifu Sheshije kuwa lazima ajitambulishe kama mwanamume ndiposa aweze kupanda ngazi. Ni bayana kuwa mwanamke anajidunisha mwenyewe na pia, wakati huo huo, anachangia kudunishwa. Katika hatua ya mwanamke kujikwamua kutoka ukandamizaji wa kijinsia, anakumbana na changamoto. Kikwazo kikubwa kwake ni wale ambao hawaamini kuwa anaweza kupata nafasi katika jamii kama tu wanaume. Kwanza, kuna wanaume ambao hawajakubali kumwona mwanamke kama kiumbe ambaye 'anastahili'. Hawa hawawezi kukubali mwanamke apewe wadhifa wowote na hata akipewa hawatampa heshima. Kuna wale ambao wanaendelea kukua katika ukubalifu wa upya huu wa wanawake kupewa nafasi kuitumikia jamii katika uwanja wa kiuchumi. Hawa huwa wanao moyo wa kuwapa viumbe wa kike nafasi bora kuongoza. Dondoo hili limedhihirisha hali hii, ya wale wanaopinga na wale wanaomhimiza mwanamke atambulike sawa na mwanamume.

### 4.1.5.2 Ukandamizaji wa Mwanamke kutoka kwa Mwanamke

Mwanamke humkandamiza mwanamke mwenzake pale ambapo anaendekeza dharau au hata kejeli kwa huyo mwenzake. Huwa mara nyingi ni kutokana na wivu au kutokana na tamaduni walizokulia wanawake hawa. Wamekuzwa kwa mila na desturi ambazo

zinamdunisha mwanamke kiasi kuwa hawajiamini na hawajiheshimu miongoni mwao: wanakuwa maadui wao wenyewe!

Mwanamke, anayewakilishwa na Nakuruto katika 'maumbo' yake mbalimbali, anasawiriwa na Clara kama ambaye anahitaji nguvu fulani ili kuisaidia jamii. Katika mjadala miongoni mwa wanawake waliokuwa wanafua nguo kando ya ziwa Ipe, wanamkejeli Nakuruto aliyesimama mbali nao akiwatazama. Wengine wanadai kuwa huenda yeye ni 'afisa mazingira', huku wengine wakisema kuwa yeye ni 'mwanamke nyapara'. Bi. Natesha anasema kuwa pengine ametumwa kulikagua ziwa Ipe lakini papo hapo Mama Bintifundi anamkatiza na kumuuliza ikiwa kuna maafisa wanawake!

> "Tangu lini tukawa na maafisa wanawake hapa kwetu! Hicho ni kioja bibi," alitamka Mama Bintifundi huku akibebetua midomo, ishara ya dharau. Kwake, wazo la kumhusisha mwanamke na kazi za ofisini lilimtia kero kwani hastahili kabisa kutwaa madaraka kama hayo. (uk 33)

Maelezo ya Bintifundi ni kuwa wanawake hawafai kupewa vyeo katika jamii hii anayoishi Nakuruto. Wanawake wamekandamizwa hata kukubali ukandamizaji huu kwa kuwa hali ya kawaida. Pia, dondoo hili linamaanisha kuwa sera ya serikali inambagua mwanamke kwa kigezo cha jinsia au kuna ukasumba wa kumfikiria mwanamke kama asiyeweza kuwa afisa wa serikali. Ukandamizaji huu aghalabu hujitokeza zaidi miongoni mwa wanawake wenyewe.

> Kwake (Mama Bintifundi), wazo la kumhusisha mwanamke na kazi za ofisi lilimtia kero kwani hastahili kabisa kutwaa madaraka kama hayo. Aliamini kwamba, mwanamke daraka lake ni mekoni na kutunza watoto ili kuendeleza kizazi cha binadamu. (uk 33-34)

Hapa mwanamke, yeye mwenyewe, anajidunisha na haoni kuwa mwanamke anastahili madaraka. Kwake yeye Mama Bintifundi, mwanamke kazi yake ni ya kupika na kutunza watoto basi. Kwa kweli haya ni mawazo ya utamaduni wa jamii nyingi za

Kiafrika ikiwamo jamii ya Abagusii nchini Kenya atokako mtafiti. Wanawake hawaruhusiwi kufanya kazi nje ya malezi ya watoto na kupika (Miencha, 1993: 77). Kwa hivyo Mama Bintifundi, kama mwanamke, anajienezea kasumba ya kumdunisha mwanamke. Haya ni mawazo ambayo yamepitwa na wakati na vile vile uhalisia wa mambo kwa sasa hivi ulimwenguni. Katika ulimwengu huu, kumekuwa na wanawake shujaa kuliko wanaume, viongozi wa nchi ambayo wametawala vyema kushinda hao wanaume. Mfano hapa nchini, marehemu Profesa Wangari Mathai, kwa ushujaa wake na kuwa mstari wa mbele kupinga uchafuzi wa mazingira, alituzwa tuzo la Nobel. Profesa Olive Mugenda, aliongoza Chuo Kikuu cha Kenyatta hapa nchini Kenya kwa muda wa miaka kumi kama Naibu wa Chansela wa chuo hicho. Na wakati huu wake, chuo hicho kimepiga hatua kubwa katika miundo msingi na upanuzi wa kozi mbalimbali, kama vile Kitivo cha Uhandisi, Kitivo cha Sheria na Kitivo cha Utabibu. Bi Margaret Thatcher, aliyekuwa Waziri Mkuu nchini Uingereza miaka ya tisini, aliongoza vyema sana nchi hiyo na kuzidi kupata umaarufu. Kwa hivyo kasumba ya kumdunisha mwanamke, ni jambo lisilo na mashiko yoyote, na kasumba hii inafaa kutupiliwa mbali katika ulimwengu wa leo. Wanawake wamedhihirisha wanaweza kama alivyoangazia Clara katika *Nakuruto*.

Kunakuwepo na mjadala baina yao na wengine wanamtetea mwanamke na kusema kuwa anaweza kuchukua madaraka yoyote yale ambayo mwanamume anayo:

> "Tangu leo bibie. Huyo hapo basi. Kwani wanawake hawawezi kuwa maafisa?" aliuliza Bi Natesha.
>
> "Wewe unamfahamu au unamjua?" aliuliza Bi. Cheusi.
>
> "Simjui, simfahamu lakini nimemskia," alijibu.
>
> '"Haya mwasikia basi. Wenye uzushi ni hawa. Maneno ya kusikia au kuambiwa kwao ni uhalisi mtupu," alisema Mama Bintifundi huku wengine wakiangua kicheko. (uk 34)

Akina mama hawa wanajadili kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii. Baadhi yao wanasema kuwa mwanamke hafai kuwa na cheo chochote huku wengine wakimtetea mwanamke wakisema kuwa anao uwezo kama wa mwanamume na hivyo basi hakuna jukumu ambalo hawezi kulifanya.

Kutokana na mjadala huo, mwanamke anaonekana kiumbe dhaifu kwa wanawake wenzake na wanajamii wote kwa jumla, isipokuwa wachache ambao wamepata mwangaza wa elimu ya Wanguzu. Hawa ni baadhi ya wanajamii ambao wanaamini kuwa mwanamke hafai kuwa mekoni au kutunza watoto, bali ni kiumbe ambaye anafaa kuwa sawa na mwanamume katika kuiendeleza jamii kwa jumla. Kinyume na mawazo haya, wanajamii wamekuzwa kiutamaduni kuamini kuwa mwanamke ni kiumbe ambaye anamfuata mwanamume katika nyanja zote.

Baadhi ya wanawake wamefunzwa na jamii kuwa nafasi ya mwanamke ni moja: nafasi ya nyumbani na anayejaribu kuikataa ili anyakue nafasi zingine, anaasi ukawaida wa jamii. Mara nyingi, aina hii ya wanawake hukataa hatua yoyote ya kuwakomboa wakijua kuwa ni kinyume cha matarajio yao, na hivyo basi hata ikiwa ni wenzao ambao wanapewa nyadhifa mbalimbali huenda watawakataza au watawazomea. Hii ni kasumba ya utamaduni wa Mwafrika. Ndiposa Clara, hata akimpa mwanamke nguvu katika ulimwengu wa riwaya, anawatahadharisha wanawake juu ya kutowasahau wenzao pindi wayapandapo mamlaka.

Katika sura ya saba ukurasa wa mia moja thelathini na sita (uk 136), Clara analinganisha ubinafsi uliodhihirishwa na wanaume na ule ambao wanawake huwa nao mara wapewapo vyeo au nyadhifa mbalimbali. Anadai kuwa wanawake walioruhusiwa kupanda mnara waliwasahau wenzao hata kupuzilia mbali ujumbe waliopewa:

> (Sheshije) Aliuachilia mkono uliomshika alipowafikia akina Macmapeni na kuwaona wakitabaradi katika harufu ya nta. Matumbo yao yalikuwa yamevimba kutokana na hewa yenye harufu ya nta waliyovuta. Sheshije alivutiwa na yale mazoea yao, kwa hivyo akaamua kufanya mahali pale mastakimu yake. Aliingia kwenye mchakato wa kuitafuta harufu ya nta, akaudharau ujumbe uliotumwa na wanawake wenzake awasaidie kufika kule aliko. Kiburi sasa kilimvaa akakataa abadan katan kusikia kilio chao. (uk 135-136)

Hapa, tunakumbana na mwanamke anayewasahau wenzake waliomsaidia kufikia aliko na kuanza kuwadunisha kwa kujiunga na wanyanyasaji wengine. Sheshije alikuwa anawaleta wanawake pamoja ili kutetea mmoja wao kwani wao ndio wanaoweza kujikomboa wenyewe. Alikuwa mtetezi wa akina mama kijijini lakini alipopewa mamlaka, aliwasahau wenzake kiasi kuwa alianza kuwadharau.

Wanawake, kama Clara anavyojaribu kutueleza, pia ni binadamu kama tu wanaume. Wakipewa mamlaka, huwasahau waliowapeleka kule na kujilimbikizia mali bila kuwajali viumbe wengine. Ni ujumbe anaopitisha kuwa ikiwa tunakashifu uongozi mbaya tusiwe tunafunikwa na jinsia kwani jinsi ambavyo kiongozi mwanamke atakosea ndivyo vile vile ambavyo kiongozi wa kiume atafanya kosa hilo.

Hata hivyo, harakati hizi za kumkomboa mwanamke zinakumbwa na changamoto si haba kutoka jinsia zote na ni vyema kwanza ieleweke, upekee wa mwanamke wa sasa ni tofauti ikilinganishwa na ule wa mwanamke wa zamani. Upekee huu ukibainishwa, itakuwa rahisi kuihubiri nafasi yake miongoni mwa wanajamii. Hivyo basi, mwanamke anafaa apewe nafasi ‘anayostahili’ katika jamiii lakini pia ikumbukwe kuwa anapopewa nafasi hiyo, bado anabakia kuwa mwanamke na hawezi ‘kuwa’ mwanamume. Pia, mwanamke akipewa nafasi katika jamii, hafai kumdunisha mwanamume kwani wanafaa kufanya kazi pamoja ili kuiendeleza jamii kwa jumla. Wote ni binadamu na wana uwezo sawa ila tofauti ni jinsi wanavyoutumia uwezo huo na uzalia wao.

Humu nchini Kenya, wanawake wamepewa nafasi chache katika vyeo vya mashirika mbalimbali ya kiserikali. Pia, Bunge la Kitaifa limecheleweshа sheria ya jinsia iliyofaa kupitishwa kufikia mwezi wa Agosti mwaka wa 2015. Hili limesababisha vyama vya kisiasa na mashirika ya kiserikali kuandamana ili kulazimisha Bunge kupitisha sheria hizi za kikatiba (*Daily Nation, July 2, 2015*). Makala mengi imeandikwa ya kuonyesha kuwa wanawake wanahitaji sheria hii ili wawajibike zaidi lakini wabunge, ambao wengi wao ni wanaume, hawaoni manufaa ya wanawake ili waipitishe sheria hiyo kwa haraka na kwa uyakini unaohitajika. Hatua hii ya kusitisha sheria kama hii inaonyesha bayana kuwa, wanajamii wengi bado hawajawakubali wanawake kuchukua nyadhifa katika mashirika ya kiserikali na na hata yale yasiyo ya kiserikali.

Ni bayana kuwa nchini Afrika, mwanamke ametengwa na jamii. Ripoti kuhusu idadi ya wanawake walio katika bodi za makampuni mbalimbali barani Afrika iliyotolewa na shirika *African Development Bank (AfDB)*, inasema kuwa asilimia kumi na nne (14%) tu ya wanawake ndiyo iko katika mabodi mbali mbali ya makampuni barani Afrika (*The EastAfrican, June 27-July 3, 2015*). Hata hivyo, ripoti hiyo ilionyesha kuwa nchi ya Kenya ndiyo ambayo ina idadi kubwa zaidi ya wanawake katika mabodi hayo barani Afrika. Tukio hili linatia moyo wakereketwa wa kupigania haki za wanawake, mtafiti akiwa mmoja wao. Ripoti hiyo pia inasema kuwa wanajamii wengi hata waliopata elimu ya juu bado hawajamkubali mwanamke kama kiumbe ambaye anaweza kuwajibika katika kazi zake kama tu anavyoweza kuwajibika mwanamume.

Rais Uhuru Kenyatta aliwateua mawaziri wanawake sita (6) alipounda serikali mnamo mwaka wa 2013. Jumla ya mawaziri wote ilikuwa ni kumi na sita. Hatua ya Rais Kenyatta iliashiria kuwa viongozi wameanza kuwakubali wanawake kama walio sawa na wanaume kiasi ya kuwapa majukumu makubwa kama ya mawaziri.

### 4.1.6 Ukandamizaji wa Mwanajamii kutoka kwa Wakoloni

Mkoloni ni mtu yeyote aliyetawala nchi geni ambayo si yake na ambayo ina desturi na makabila tofauti na lake. Wakoloni hawa waliendeleza ukandamizaji kwa wenye nchi.

Ukandamizaji huu unajitokeza Wazungu wanapotumia nguvu zao za kiuchumi na kimaarifa kuwanyanyasa wanajamii. Wazungu hawa wanatumia maarifa yao kuendeleza sera zao za kibepari katika wanajamii na kuwatenganisha miongoni mwao. Clara anatueleza kuwa katika jamii bado kuna ukoloni mamboleo ambao unaendelezwa na nchi za kimagharibi na wenyeji wa nchi za Kiafrika.

Ukandamizaji huu umejitokeza bayana katika riwaya hii katika matukio mengi. Bw. Wellingtone, mzungu kutoka nchi ya Wanguzu, anavamia kijiji cha Maweni na kunyakua rasilmali na mashamba yote. Anakuja na vibaraka wake na kuwahamisha wanakijiji ili aweze kupata nafasi ya kuchimba madini hayo. Wanakijiji wanahamia nchi kame iliyojaa mawe, miamba na kokoto.

> "Watu walikataa kuhamishwa. Lakini wakashawishiwa kuhama baada ya kuahidiwa utajiri mkubwa. Mjukuu wangu, walihamia kwenye ardhi kame iliyojaa mawe, miamba na kokoto tupu. Sehemu isiyoweza kuzalisha chakula…" (uk 57)

Wanakijiji wanaanza kuogelea katika umaskini na njaa inazidi kwani hawangeweza kufanya ukulima. Yeye na vibaraka wake wanasafirisha madini na rasilmali ughaibuni bila kuwajali wanakijiji. Mzee Saluda anawafafanua kama wanyonyaji wasio na utu akimwelezea Nakuruto kuhusu mtaa wanaoishi Wanguzu hao:

> Ule ni mtaa wa wakwasi, makabaila na wanyonyaji wanaofaidi madini bila kuwajali wale waliowaachia ardhi yao. Hao ni watu wanaohonyoa mali ya wanakijiji bila kujali uhai wao. Wanasafirisha madini ughaibuni na kujirundika mapesa chekwachekwa… Katika maksari yale ndipo wanakijiji wanapouza nguvu zao. Kutwa kucha wanawatumikia wakwasi; hao wakinadhifisha makao yao na kuwaandalia mapochopocho. Wengine huhudumia bustani na vitalu vyao ilhali wengine huwatunza mifugo wao. (uk 57)

Katika dondoo hili, wanakijiji wanafanyishwa kazi katika nyumba za wazungu, ambao ni wakoloni, pasi na kuwalipa ipasavyo. Kimsingi, wakoloni hawa wanawatumia vibaya na hivyo basi kuwanyanyasa.

Wanakijiji wananyonywa kirasilimali na kimwili na Wanguzu hawa ambao pia hawawaruhusu kupata tajriba ya kuendesha mashine zao. Wanawafanya wanakijiji kuwa watumwa wao daima:

> Wenyeji hawakuwa na ujuzi wa kukisimamia kile kiwanda cha kusafishia madini hata ingawa wachimbaji walikuwa tayari kurejea kazi zao. Ijapokuwa baadhi ya wanakijiji walikuwa na utaalamu wa kuendeleza shughuli za uzalishaji mali kiwandani, hawakuwa na tajriba ya kuweza kufanya hivyo. Wanyonyaji hao hawakuwapa fursa ya kujifunza mbinu za kuzalisha mali seuze za kuendesha biashara ile. (uk 68)

Hali hii pia inajirudia katika sura ya saba, (uk 123), pale ambapo wananchi wanakuja pamoja kujenga ngazi ya kuwawezesha kuifikia nta. Walikuwa wanataka wajenge ngazi ndefu ambayo ingeufikia wavu wa Quick Buck. Wanapoanza kazi, waliopewa kandarasi, wanaanza kuiba bidhaa hizo kwenye malori. Ba Kikuete anaita mkutano wa kuiteua kamati ya kuchunguza madai hayo ya wizi lakini kura zinaibwa na hatimaye Ba Kikuete analazimishwa kuomba msaada wa jamaa ya Quick Buck. Mmoja wa jamaa ya Buck, Bw. Bullyson, anawasili na kudai kulipwa kiasi fulani cha pesa ndipo aweze kuwaauni. Ngazi inaanza kujengwa kupitia usimamizi uliotolewa na Bw. Bullyson.

> Ba Kikuete aliamua kuita mkutano ili kuteua kamati itakayosimamia ujenzi ule. Uchaguzi ulifanywa na wawakilishi wa wanavijiji kupitia kura ya siri. Lakini hata kabla ya shughuli ya kupiga kura kukamilika, kulitokea uvumi kuwa kuna kura zilizoibwa kutoka kwenye masanduku… Mwishowe, Ba Kikuete aliamua kuomba usaidizi kutoka kwa jamaa ya Quick Buck ili kufanya uchaguzi wa halali bila ghasia…
>
> Hapa aliwasili Bw. Bullyson na wafuasi wake ambao walidai kulipwa kiasi fulani cha mali ya wanavijiji ili kutoa usaidizi. (uk 126)

Wanajamii wamewaruhusu Wamagharibi kutekeleza majukumu ambayo wao wenyewe wanaweza kuyafanya. Wakoloni wamekandamiza akili zetu, Waafrika, kufikiria kuwa hatuna uwezo wa kujisimamia. Wamaweni wanaomba msaada wa Wamagharibi ili kujenga ngazi, jambo ambalo linawagharimu pesa nyingi. Bidhaa yoyote inayokosa, lazima iagizwe kutoka ughaibuni na ikiagizwa lazima iletwe na mmoja wao ambaye atakuja kuiweka; kusababisha gharama yake kuwa ghali kwa wanajamii.

Ukandamizaji huu wa Wanguzu unasababisha rasilimali za wanajamii kutumiwa bila kuwafaidi wao. Umaskini unakithiri. Hali kama hii hupatika Barani Afrika, nchi ya Kenya ikiwa mfano mzuri. Barabara ya reli mpya (Standard Gauge Railway) kutoka Mombasa hadi Nairobi inajengwa kutokana na mkopo kutoka nchini China. Wahandisi wasimamizi wametoka huko na vifaa karibu vyote hutoka huko. Kwa hivyo barabara hii ya reli itawafaidi Wachina zaidi kuliko Wakenya itakapokamilika. Kwa hivyo ukandamizaji huu anaotuonyesha Clara, tuko nao hapa Kenya kwa sasa hivi. Na ni ukandamizaji ambao unafaa kupingwa ili sisi wenyeji wa Kenya tupige hatua ya kimaendeleo bila madeni makubwa makubwa yanayoleta unyanyasaji na ukandamizaji kutoka mataifa yaliyoendelea na umaskini nchini.

### 4.2 Suluhisho la Ukandamizaji

Suluhisho la ukandamizaji limejitokeza kwa njia anuwai kama zilivyo aina za ukandamizaji. Clara amedokeza njia ambazo zinaweza kutumika ili kuepukana na unyanyaswaji wa mwanajamii yeyote bila kujali umri au jinsia yake. Ili kuweza kutatua tatizo la ukandamizaji, ni vyema mtatuzi kuelewa chanzo cha ukandamizaji huo.

#### 4.2.1 Utambuzi wa Nafsi

Anayenyanyaswa au kukandamizwa lazima agutuke na atambue kuwa anakandamizwa ndiposa aweze kujinasua kutoka kwa mtego huo. Pia, ni lazima awe na nguvu au uwezo

fulani ambao utamwezesha kujinasua. Kwa hivyo, hatua ya kwanza ni kuwa na utambuzi wa nafsi, kuwa unakandamizwa, na unakandamizwa kwa njia gani, na nani, kisha uwe na uwezo wa kujinasua.

Nakuruto anapopeperushwa katika nchi ngeni iliyojaa mapango na vitu vya ajabu ajabu, anajaribu kujitoa kwenye hali hiyo lakini anashindwa. Ni taswira ya mwanajamii ambaye amekandamizwa lakini hajui ikiwa yuko katika hali hiyo. Tunaambiwa:

> Alipokuwa akipeperushwa jinsi ile, alijaribu kujifinya ili aone ikiwa alikuwa ndotoni au vipi. Lakini kila alipojaribu kunyanyua mkono, aliuhisi mzito mno. Alibaki kuangama huku kinywa kikiwa wazi kwa mshtuko. (uk 4)

Hapa, Nakuruto haamini anayoyaona. Kutoamini kwake, anajiuliza iwapo anyoyaona ni ndoto. Ili kutaka kujua iwapo yuko ndotoni, alijaribu kujifinya ili athibitishe anayoyaona lakini anashindwa. Kwa hivyo, anashindwa kujinasua. Hii ni hali ya mwanadamu halisi anayekandamizwa, anapouona ukweli hatimaye hudhani si kweli bali ndoto tu. Na kwa vile alikandamizwa kwa muda mrefu mno, kila anapojaribu kujinasua hushindwa na kusalimu amri abaki katika hali hiyo. Hii ndiyo hali Nakuruto anatuonyesha. Lazima anayekandamizwa ajitahidi sana kuondoa hali hiyo au ataendelea kuishi katika utouhalisi huo hadi atakapogutuka na kuingia katika ulimwengu halisi. Ndoto inalinganishwa na ukandamizaji. Mwanajamii asipoweza kutambua kuwa anakandamizwa, ataendelea kuogelea katika hali hiyo hadi pale atakapotambua kuwa yu katika lindi la unyanyaswaji ndipo aanze kutafuta mbinu za kujiopoa.

Dondoo hili pia linachora taswira ya wale wanaokandamizwa, kuwa wanaweza kujinasua kutoka kwa mtego huo ikiwa tu wana uwezo wa kifikra au uwezo wowote ule utakaowawezesha kujitoa kwa hujuma hiyo. Kutambua tu kuwa unanyanyaswa

hakutoshi bali pia unahitaji jitihada na nguvu zaidi za kujitoa katika shimo hilo la hujuma. Nguvu zaidi ni za yule mwenyewe anayekandamizwa. Ama afanye kibinafsi au wanaokandamizwa waje pamoja na kwa nguvu moja walikabili tatizo hilo.

### 4.2.2 Mwanamke

Clara anampendekeza mwanamke kuwaokoa wanajamii kutoka kwa ukandamizaji wowote. Anadai kuwa mwanamke ana uwezo wa kutatua matatizo ya wanajamii na hata kumkomboa mwanamke kutoka kwa viganja vya taasubi ya kiume.

Kupitia kwa mhusika Nakuruto, ambaye ni mwanamke, anaitalii jamii na kutuonyesha matatizo mbalimbali wanayoyapitia. Anatupa mapendekezo kuhusu njia mwafaka za kumaliza ukandamizaji huo. Mwanamke Nakuruto ndiye anatoa mapendekezo hayo.

Mwanamke, Nakuruto, anapendekeza wamwondoe dhalimu Bw. Brooke kutoka kijiji chao arudi Unguzuni. Brooke amewanyonya na kuwadhulumu wanajamii hadi kuwasabishia umaskini. Nakuruto anapendekeza kufanywe mgomo mkubwa ambapo mnyanyasaji Brooke atatimuliwa. Anasema:

> Wenzangu, tutakubali kuwa tambiko la risasi? Tutakubali mauaji ya halaiki hapa Latimbi?... Nisikilizeni kwa makini sana. Nina shauku ya kuwapigania nyie na watoto wenu. Sifanyi mzaha. Ninawahakikishia kwamba mkizingatia ushauri wangu, bila shaka mtafaulu kumwondoa huyu dhalimu anayewataabisha. Nafahamu pia kwamba kula uhondo kwataka matendo, asiye na matendo hula uvundo. Ni hivi, chagueni vijana mabarubaru miongoni mwenu, hasa wale wanaofunuliwa siri na vilinge vya elimu ya hawa wanguzu ili waweze kupanga mapambano murua. (uk 43, 44)

Nakuruto anapendekeza kuwa wenye elimu au waliosoma elimu ya Wanguzu ndio silaha ya mapamblano. Wao ndio wanaweza kukomesha udhalimu huu. Jambo hili lilitokea hapa nchini Kenya tulipodai uhuru. Wale Wakenya waliokuwa wamepata elimu ya kimagharibi, walikuwa msitari wa mbele kupigania uhuru wetu mfano Rais wa kwanza Mzee Jomo Kenyatta na wenzake kama Jaramogi Oginga Odinga, Tom

Mboya, Ronald Ngala, Ochieng Aneko, Bildad Kagia, Paul Ngei, Martin Shikuku (wote marehemu), Rais mstaafu Daniel arap Moi na wengine wengi.

Mwanamke huyu anawahamasisha wanajamii na wanafanya mgomo kumtoa dhalimu Brooke:

> … Nakuruto alitia tabasamu usoni kisha akatamka, "Nina mpango mahsusi ambao mkiufuata, mtaweza kumwondoa huyu…huyo…n'nani huyo?"
>
> "Bwana Bruki," alitamka mzee mmoja.
>
> "Tupange tumwondoe dhalimu huyo katika ardhi yetu asiendelee kuunyonya uhai wetu pamoja na wa watoto wetu. Na hili ndilo ninalotaka tulijadili sasa. Lisingoje kesho maana huenda tusiishi kuiona hiyo kesho." (uk 43)

Japo Clara amempa uwezo zaidi wa ukawaida wa mwanamke, kama jamii ya riwaya inavyomwona, tunaweza kupata ujumbe anaojaribu kupitisha kuwa, suluhisho la ukandamizaji linatoka kwa yeyote; awe mwanamke au mwanamume. Hapa amemtumia mwanamke kuwa anaweza kuwahamasisha wanajamii ili wajikomboe.

Pia, baada ya hamasisho la Nakuruto, wanakijiji wa Latimbi walipata ari ya kumng'oa Bw. Brooke 'mamlakani'. Mwandishi anatuonyesha kuwa katika jamii, mwanamke ni kiumbe ambaye ana uwezo wa kuikomboa jamii kutoka viganja vya ukandamizaji wa watu dhalimu na hata ukandamizaji wowote ule ukiwemo wa kimazingira, wa kijinsia na hata wa kiuchumi. Clara amempa mwanamke uwezo wa kumkomboa binadamu kiasi kuwa anamuumba kuwa lishe na rasilmali ya jamii.

### 4.2.3 Sera za Vijana

Serikali ina jukumu la kuweka sera chanya za kuhakikisha kuwa vijana wanapata asilimia fulani za nafasi za ajira katika afisi na mashirika ya kiserikali na hata katika mashirika yasiyo ya kiserikali.

Kwa sasa hivi, serikali ya Kenya ikiongozwa na Rais Uhuru Kenyatta, imeunda Idara ya Vijana chini ya Wizara ya Ugatuzi na Huduma ya Vijana ili kuwapa vijana fursa ya kuendeleza talanta zao na kupata ajira. Vile vile kuna viongozi serikalini aliowateuwa ambao ni vijana, mfano Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia, Bw. Joe Mucheru.

## 4.3 Changamoto za Ukombozi

Katika kila hatua ya kumnusuru kiumbe yeyote, lazima utakumbana na vikwazo fulani. Vikwazo hivi huweza kutokana na anayenusuriwa au kutokana na njia inayotumika kumnusuru kiumbe huyo. Mara nyingi, changamoto hizi hutokana na anayenusuriwa mara anapopata uhuru wake.

### 4.3.1 Utengano wa Kimawazo Miongoni mwa Wanajamii

Wanajamii, wakati mwingine, hawaoni haja ya kujikwamua kutoka kwa hali ya ukandamizaji japo huenda wanajua bayana kuwa wanakandamizwa. Miongoni mwa Walatimbi, kuna baadhi ya wanajamii ambao wanakataa pendekezo la Nakuruto la kupigania uhuru wao na kusema kuwa wao wana watoto na wake ambao wanawahitaji. Wengine wanadai kuwa mwanamke ni kiumbe dhaifu. Wanawakatiza wenzao tamaa ya ukombozi kwa kuwaeleza kuwa panga na sime haviwezi kufua dafu mbele ya shaba; bunduki, aliyomiliki Bw. Brooke. Mmoja wao anasema:

> Nyie mnaota ndoto za mchana. Mnadhani magongo, sime na panga vitafua dafu mbele ya shaba? (uk 46-47)

Anamalizia akisema kuwa yeye hatakuwepo miongoni mwa watakaogoma kwani bado anathamini maisha yale.

> Mimi simo katika kundi hilo kwani nina tamaa ya kuishi. (uk 46)

Maneno haya yanazungumzwa na kijana Jumanne. Hili linaonyesha kuwa sio wanakijiji wote wako tayari kupambana na haini Brooke. Baadhi yao wanapendelea kushirikiana naye. Ukosefu wa umoja miongoni mwa wanajamii unawafanya kukosa nguvu za kutosha kuwakabili wanyanyasaji. Hali hii ni halisi, mfano hapa Kenya wakati wa kupigania uhuru miaka ya hamsini, walikuwapo watu kama Jumanne. Watu hawa walikuwa wasaliti na walijulikana kwa jina la '*Home Guards'*. Ndio waliwasema wale wenziwao waliotaka Mkoloni atoke nchini Kenya. Kwa hivyo Clara, ametusawiria hali halisi ya maisha.

### 4.3.2 Ukosefu wa Ujuzi na Tajriba

Hii ni hali ya kutojua la kufanya baada ya kupata uhuru. Tatizo hili huenda linatokana na kule kupumbazwa kuwa lazima tuongozwe na watu kutoka mataifa ya Magharibi ndipo tuweze kutunza rasilimali kwa njia bora. Wanajamii pia huchukulia kuwa uhuru unaponyakuliwa, wanajamii hawafai kufanya bidii. Kinyume na matarajio ya Wamaweni, walipata uhuru waliokuwa wanapania ukiwageukia na kuwa utumwa kwa sababu hawakuwa wamejiandaa kuchukuwa hatamu kutoka kwa Wanguzu na pia hawakuwa na ufahamu waliokuwa nao Wanguzu kuhusu kusimamia viwanda:

> Nakuruto aliyaona yote yale lakini hakufurahia matokeo ya baadaye. Wenyeji hawakuwa na ujuzi wa kukisimamia kile kiwanda cha kusafisha madini hata ingawa wachimbaji walikuwa tayari kurejea kazi zao. Ijapokuwa baadhi ya wanakijiji walikuwa na utaalamu wa kuendeleza shughuli za uzalishaji mali kiwandani, hawakuwa na tajriba ya kuweza kufanya hivyo. (uk 68)

Tatizo la ujuzi na tajriba linawafanya wanajamii wengi kutojua la kufanya baada ya kuachiwa uhuru wa kuendeleza uchumi wao kusababisha ukoloni mambo-leo na wakati mwingine ufujaji wa rasilimali. Jambo hili ni dhahiri katika nchi changa zilizojitawala kutoka kwa wakoloni.

## 4.4 Hitimisho

Kupitia riwaya hii ya *Nakuruto*, Clara ameonyesha ukandamizaji wa aina mbalimbali. Ukandamizaji huu ameudhihirisha kupitia mhusika Nakuruto aliye kipaza sauti chake. Ameonyesha wanawake wanavyokandamizwa katika jamii kwa njia kadhaa na wakandamizaji tofauti. Pia ameonyesha jinsi wanajamii wengine wanavyokandamizwa.

Clara amezungumzia umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na athari zinazotokana na kutohifadhi mazingira kwa njia ifaayo. Ameonyesha jinsi jamii inateseka kutokana na athari za njaa na ukame. Mifugo wanafariki, maziwa yanakauka kusababisha uchoyo na uhasama miongoni mwa wanajamii.

Clara pia ameonyesha ufisadi wa maafisa wa serikali kushirikiana na mabwanyenye katika kunyakua mashamba ya wananchi. Sera ambazo serikali inaweka, zinarahisisha matajiri kuwanyanyasa wananchi kiuchumi na kuwadhulumu kwa kuwafanyisha kazi kwa muda unaozidi ule wa kawaida na malipo ni duni. Wananchi wanakuwa watumwa katika nchi yao.

Clara amedokeza jinsi matatizo yanayomkumba mwanajamii yanavyoweza kutatuliwa na wanajamii wenyewe. Wao ndio dawa mjarabu ya matatizo yao na wasisubiri watu kutoka nchi nyingine kuwatatulia matatizo yao.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumeeleza ukandamizaji wa mwanajamii kwa jicho la mwandishi mwanamke na jinsi yalivyomwathiri mwanajamii huyu katika nyanja mbalimbali za maisha: kiuchumi, kijamii na kisiasa. Pia, tumetoa muhtasari wa tasnifu.

Hatimaye, tumetoa mchango na mapendekezo yetu kuhusu mada au sehemu za utafii huu ambazo zinaweza kuhitajika kuendelezwa au kutafitiwa zaidi.

## 5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu uliangazia ukandamizaji wa mwanajamii ulivyodhihirishwa na waandishi wanawake. Ili kufaulisha uchanganuzi huu, tulitumia kazi mbili za kifasihi zilizoandikwa katika lugha ya Kiswahili na zilizoandikwa na waandishi wanawake. Tulichanganua riwaya ya Clara Momanyi, *Nakuruto* na ya Sheila Ryanga, *Dago wa Munje* na kutazama jinsi waandishi wanawake wanalijadili swala la ukandamizaji na jinsi ya kusuluhisha swala hilo. Tasnifu hii ilitathmini anayekandamizwa ni nani na ni kwa nini anakandamizwa. Pia, tulijadili jinsi ambayo mwanamke anavyosuluhisha matatizo ya ukandamizaji yanayomkumba mwanajamii.

## 5.2 Mchango wa utafiti

Humu nchini Kenya, kuna sera ya kuwaruhusu wanafunzi kuchagua ni adhabu ipi wangependelea baada ya kufanya makosa (*Daily Nation, June 19 2015*). Tume ya Kuwaajiri Walimu nchini Kenya (Teachers Service Commission) inasema kuwa inabuni njia mwafaka ambayo wanafunzi na walimu wataweza kujadiliana kuhusu njia bora zaidi ya kumwadhibu mwanafunzi baada ya kufanya kosa.

Ikiwa sera kama hii itabuniwa na kuanza kutumika, itasaidia kupunguza visa vya walimu kuwakosoa watoto kwa kuwaumiza kwa kuwapa adhabu kali na zisizofaa. Aidha itasaidia wanafunzi wasidhulumiane kama inavyofanyika katika shule za upili hapa nchini kwa wanafunzi wageni katika shule hususan wa kidato cha kwanza. Itawafanya wawe na utu na kudumisha haki za wengine. Pia, ni muhimu kwa mashirika yasiyo ya kiserikali kufadhili miradi mbalimbali. Mashirika yasiyo ya kiserikali yanashiriki kutoa suluhisho la ukandamizaji dhidi ya watoto. Mashirika haya huendeleza miradi mbalimbali ambayo huwainua wanafunzi kiuchumi, kielimu na kitabia. Kwa mfano, humu nchini Kenya, kuna mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali ambayo yamefadhili miradi mbali mbali ya watoto. Zaidi ya wanafunzi elfu mbili (2,000) walipewa viatu na mashirika mbali mbali wakati wa kuzindua kampeni dhidi ya funza katika kaunti ya Kisumu (*The Standard, June 18, 2015)*. Hatua hii itawafaa zaidi watoto kwani wanaweza kusoma bila athari zozote zile zinazojitokeza kutokana na ukosefu wa viatu au kuwepo kwa funza. Hili ni suluhisho ambalo linawafaa wanafunzi hususan wale wanaotoka katika familia zisizojiweza kifedha.

Uchunguzi wetu umebainisha kuwa, waandishi wanawake wa karne ya ishirini na moja, wamepanua maswala ya kujadili katika kazi zao. Hawashughulikii tu maswala ya wanawake kama ilivyozoeleka bali wanajadili maswala yoyote yanayoikumba jamii. Ni waandishi wa jamii yote si wa mwanamke pekee. Wanajadili matatizo yanayowakumba wake kwa waume katika jamii. Utafiti umechangia kufafanua hali mbalimbali za ukandamizaji katika jamii. Hili litafunua macho wanajamii. Isitoshe yaliyofafanuliwa yanaweza kuwafunza walimu na maofisa wa ngazi za juu serikalini, hususan wa Wizara ya Elimu, kuangalia upya ukandamizaji shuleni na kupata suluhu la kudumu.

Wanafunzi nao wapatapo fursa ya kusoma tasnifu hii na kuona jinsi wanavyodhulumiana, wanaweza kugeuza mtazamo wao kuhusu kukandamizana shuleni kwani hudhuru masomo ya wanafunzi wengine. Kutokana na ukandamizaji huu, mwanafunzi anayekandamizwa anaweza kuacha shule na kuharibikiwa maishani mwake. Kwa hivyo watabadili tabia zao na kuwapenda wanafunzi wengine kama ndugu zao wa jamii moja hasa wanafunzi wa kidato cha kwanza wanapojiunga na shule za upili nchini baada ya kumaliza masomo ya shule za msingi.

Pia, utafiti huu utachangia katika kuhakiki kazi za fasihi zilizopo hususan riwaya. Wahakiki na walimu wa fasihi katika shule za upili, vyuo vikuu, watafaidika kwa kufahamu mikondo mbali mbali ya kuhakiki kazi za fasihi wanapofundisha somo hili.

## 5.3 Hitimisho

Mwandishi mwanamke amelijadili swala la ukandamizaji wa mwanajamii bila kuegemea jinsia yoyote. Kwa kiwango kikubwa, mwanajamii anakandamizwa kisaikolojia na kiuchumi. Japo kwa viwango tofauti, wanajamii wote wamekandamizwa. Aina nyingi za ukandamizaji huendekezwa kwa mwanajamii bila kujali jinsia yake. Wanajamii wanawake wamekandamizwa zaidi ya wanajamii wanaume, si kwa sababu ya jinsia yao au uuke wao bali kwa sababu wanawake huwa wamesawiriwa kama wanajamii wanyonge wanaohitaji huruma au kupewa nafasi zaidi ya wanaume.

## 5.4 Mapendekezo

Kutokana na mabadiliko ya kijamii kuhusu mitazamo ya wanajamii wanaokandamizwa, ni vyema ijulikane kuwa kuna upya wa unyanyasaji hivi kwamba wanaokandamizwa si wa jinsia moja, bali ni wanajamii wote, wake kwa waume. Mjadala unaoibuliwa na tasnifu hii si wa mwisho. Kuna maswala ambayo

hatukushughulikia katika tasnifu hii na tungependekeza yashughulikiwe na watafiti wengine. Tofauti ya jinsi waandishi wa kiume na wa kike wanavyoangazia swala la ukandamizaji wa wanajamii katika kazi zao, ni swala ambalo litahitajika kufanyiwa utafiti zaidi. Utafiti wetu umeshughulikia waandishi wanawake wawili, mtafiti mwingine ashughulikie wengine tofauti na hawa ili kuonyesha masuala wanayoyazungumzia ili kufikia uamuzi faafu wa mjadala wa waandishi wa kike na kiume. Pia, mtafiti mwingine anaweza kuangalia ‘nafasi ya mwanamume’ katika jamii: je kunayo nafasi kama hii?

Pia, tunapendekeza serikali ianze silabasi ya haki za watoto ili wajitambue zaidi: wajue wajibu wao na haki zao vilevile. Hatua hii itawasaidia watoto kujinasua kutoka mitego ya wenzao na watu wazima ambao wana tabia ya kuwadhulumu. Walimu nao watapewa mafunzo zaidi kuhusiana na haki za watoto na jinsi ya kuwalea vyema watoto hao.

Ili kusuluhisha matatizo ya wanaokandamizwa katika jamii, serikali inafaa kubuni sera za kumchunga mwananchi. Suluhisho hili litatokana na maafisa wa elimu serikalini. Maafisa hawa wanafaa wabuni sera ambazo zitamfaidi mtoto na mwalimu wake kijumla. Sera za kujumuisha mtalaa wa elimu za haki ya watoto, majukumu ya watoto, sheria za elimu na hata haki za binadamu kwa jumla. Elimu ambayo itamwezesha mtoto kukua akitambua umuhimu wake na wa wenzake, akiwa chuoni na hata anapokuwa nyumbani.

**MAREJELEO**


Allen, J. W. T. (1972). *Tendi*. Nairobi: Heinemann.

Babu, O. (2011). *Kopo la Mwisho na Hadithi Nyingine*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Burhani, Z. (1987). *Mwisho wa Kosa.*Nairobi: Longhorn Publishers.

Burhani, Z. (2004). *Kipimo cha Mizani*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Burhani, Z. (1981). *Mali ya Maskini*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Carol, J. O. (1986). *Is there a Female Voice? Joyce Carol Oates Replies* in 'Feminist Literary Theory: A Reader'. Cambridge: Basil Blackwell Ltd. uk. 208.

Carter, D. (2006). *Literary Theory*. Harpenden: Pocket Essentials.

*Daily Nation*, July 2, 2015, "It is the duty of the state to ensure that the gender law is operational".

*Daily Nation*, July 2, 2015, "Principal defends suspension of Muslim students in row" uk 18.

*Daily Nation*, June 19, 2015, "Leaders want answers on lost Sh495 millions" uk 24.

*Daily Nation*, June 19, 2015, "Muslims asked to set up boards on teachings" uk 19.

*Daily Nation*, June 19, 2015, "Students to choose punishment"uk 19.

*Daily Nation*, June 2, 2015, "I did not cut off pupil's organ, tutor tells court" uk 10.

*Daily Nation*, June 25, 2015, "22 die as malaria drugs go missing" uk 10.

*Daily Nation*, June 25, 2015, "Agency heightens fight against illegal logging" uk 19.

*Daily Nation*, June 30, 2015, "Another land firm director shot dead" uk 15.

*Daily Nation*, June 30, 2015, "Farms of polluting water under investigations" uk 23.

*Daily Nation*, June 30, 2015, "Teacher put on trial for sex assault on students" uk 1, 11.

Eagleton, M. (1986). *Feminist Literary Theory: A Reader*. Malden: Blackwell Publishing.

Environment. (2010). *Oxford Advanced Learner's Dictionary* (International Student's Edition, p. 491). London: Oxford University Press.

Habwe, J. (2000). *Maisha Kitendawili*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Himid, R. (2007). *Yanarudia Tena*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Isiaho, J. K. (2001). "Taswira ya Mwanamke katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed" tasnifu ya M. Phil. Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret. Haijachapishwa

Jacobus, M. (1986). *The Difference of View: Women Writing and Writing about Women* in 'Feminist Literary Theory: A Reader'. uk. 216-219. Cambridge: Basil Blackwell Ltd.

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, (2004) Nairobi: Oxford University Press.

Katiba ya Kenya (2010). Nairobi: Government Press.

Kimani, C. W. (2003). "Swala la Dhuluma Dhidi ya Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili." Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu, Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kisovi, C. N. M. (2007). *Dunia Hadaa.* Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi.

Kisurulia, E. S. (2000). "Usawiri wa Wahusika katika kazi za Katama G. C. Mkangi" Tasnifu ya M. Phil. Chuo Kikuu cha Moi. Haijachapishwa

Kobia, J. M. (2004). "Taswira za Mwanamke katika Njuno (Methali) za Kimeru" Tasnifu ya M. Phil. Chuo Kikuu cha Moi. Haijachapishwa

Kudzma, E. C. (1998). Young Adult katika Edelman, C. L. na Mandle, C. L (wah), '*Health Promotion Throught the Lifespan'* (p. 583). Missouri: Mosby.

Kyovi, P. K. (2011). "Fatuma Ninja" katika C. Momanyi na R. Timammy (wah) *'Takrima Nono na Hadithi Nyingine'* (uk 1-12). Nairobi: Longman.

Kyovi, P. K. (2011). "Njugu Karanga" katika T. M. Arege (mh) *'Gitaa na Hadithi Nyingine'* (uk 1-14). Nairobi: Longhorn Publishers.

Kyovi, P. K. (2012). "Isiponyeza" katikaK. Walibora (mh) *'Maskini Milionea na Hadithi Nyingine'* (uk 50-62). Nairobi: Oxford University Press.

Kyovi, P. K. (2012). *Beluwa.* Nairobi: Oxford University Press.

Likimani, M. G. (1974). *What Does a Man Want?* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mazrui, A. (1982). *Kilio cha Haki.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Mboya, T. M. (1997). "The Woman and History in Marjorie Oludhe Macgoye's Fiction" M. Phil Thesis. Moi University.

*Merriam-Webster Dictionary, (2015): Encyclopaedia Britannica Online.* Retrieved June 24, 2015.

Miencha, K. I. (1993). "A Philosophical Analysis of Deterrent Punishment with Special Reference to Curses among the Indegenous Abagusii Community of Western Kenya" M.A Thesis. University of Nairobi.

Mnyetto, M. M. (1994). "Uchambuzi wa Dhamira, Falsafa na Mitindo katika Tamthilia za Chacha Nyaigotti Chacha" Tanifu ya M. Phil. Chuo Kikuu cha Moi. Haijachapishwa

Momanyi, C. (1998). "Usawiri wa Mwanamke katika Jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili." Tasnifu ya Ph. D. Chuo Kikuu, Kenyatta. (Haijachapishwa).

Momanyi, C. (2004). "Ngome ya Nafsi" katika K. W. Wamitila (mh) *'Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine'* (uk 98-114). Nairobi: Focus Publishers.

Momanyi, C. (2009). *Nakuruto.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Momanyi, C. (2011). "Masazo ya Fisadi" katika C. Momanyi na R. Timammy (wah) *'Takrima Nono na Hadithi Nyingine'* (uk 1-12). Nairobi: Longman.

Momanyi, C. (2011). "Mtandao na Ufasiki" katika T. M. Arege (mh) *'Gitaa na Hadithi Nyingine'* (uk 43-65). Nairobi: Longhorn Publishers.

Momanyi, C. (2011). "Mtumbwi wa Maskini" katika C. Momanyi na R. Timammy (wah) *'Takrima Nono na Hadithi Nyingine'* (uk 86-100). Nairobi: Longman.

Momanyi, C. (2012). "Tafrani Kambini" katika K. Walibora (mh) *'Maskini Milionea na Hadithi Nyingine'* (uk 38-49). Nairobi: Oxford University Press.

Muhando, P. (1975). *Pambo.* Nairobi: Foundation Books Ltd.

Muhando, P. (2001). *Lina Ubani.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Muhando, P. (2010). *Nguzo Mama.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Mule, P. K. (1991). "Swala la Wanawake katika Tamthilia ya Kiswahili: Waandishi wa Kike katika Njia Panda." Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu, Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale.* Tanzania Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Mwachofi, A. K. (1987). *Mama Ee.* Nairobi. East African Educational Publishers.

Nandwa, R. (2011). "Balaa bin Belua" katika K. Walibora na P. I. Iribemwangi (wah) *'Sina Zaidi na Hadithi Nyingine'* (uk 101-110). Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Nandwa, R. (2011). "Rafiki Yangu" katika O. Babu (mh) *'Kopo la Mwisho na Hadithi Nyingine'* (uk 145-156). Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Nandwa, R. (2012). "Haramu Tamu" katika K. Walibora (mh) *'Maskini Milionea na Hadithi Nyingine'* (uk 81-91). Nairobi: Oxford University Press.

Noordin, M. M. (2008). 'Nadharia ya Ufeministi wa Kiislamu katika Fasihi ya Kiswahili' katika N.O. Ogechi, N.L. Shitemi na K. Simala. *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. uk. 143-154. Eldoret: Moi University Press.

Ogbu, J. U. (1998). *Voluntary and Involuntary Minorities: A Cultural-Ecological Theory of School Performance with Some Implications for Education.* USA: American Antropology Association.

Oppression. (2006). *Merriam-Webster's Dictionary and Thesaurus* (p. 740). Springfield, Massachussetts.'

Ryanga, S. A. (2008). *Dago wa Munje.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

*Saturday Nation*, February 28, 2015, *"*20 schools may close as food shortagebites*"* uk 8.

Schermerhorn, R. A. (1960). *Toward a General Theory of Minority Groups.* Atlanta: Clark Atlanta University Press. http://www.jstor.org/stable/273779.

Senkoro, F. E. M. K. (1976). *Utamaduni katika Riwaya ya Kiswahili*. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, 46(2): uk.74-97.

Shake, R. (2000). “Mwendawazimu” katika M. Mbatiah (mh) *‘Mwendaqwazimu na Hadithi Nyingine’* (uk 1-10). Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Showalter, E. (2000) *Feminist Criticism in the Wilderness* in D. Lodge and N. Wood (eds) ‘Modern Criticism and Theory: A Reader’. (p. 307-330). London: Pearson Education Limited.

*Teachers Service Commision Code of Conduct and Ethics* (2003). *The Public Officer Ethics Act*, uk. 5-6.

Tertiary. (2008). *Merriam-Webster’s Collegiate Dictionary*, (11th ed.). Springfield, MA.

*The East African*, June 27 – July 3, 2015, “Where are the women in Africa’s corporate boardrooms?*” uk 24-25.*

*The Standard,* June 18 2015, “2,000 pupils get free shoes in jigger campaign” uk 28.

*The Standard,* June 18, 2015, “Drive against radicalisation launched” uk 8.

*The Standard,* June 18, 2015, “MP, school warned over disputed land” uk 8.

*The Standard,* June 20, 2015, “Senior police in allowances scandal” uk 6.

*The Standard,* June 22, 2015, “Girl flees to avoid forced marriage” uk 24.

*The Standard,* June 22, 2015, “NEP conflicts: When small things matter” uk 14.

*The Standard,* June 25, 2015, “Aviation authority loses more land” uk 15.

Timammy, R. (2004). “Uteuzi wa Moyoni” katika K. W. Wamitila (mh) *‘Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine’*. Nairobi: Focus Publishers. uk 7-19

Timammy, R. (2011). “Haki Yangu Naidai” katika C. Momanyi na R. Timammy (wah) *‘Takrima Nono na Hadithi Nyingine’*. Nairobi: Longman. uk 13-39

Timammy, R. (2011). “Mama Mkwe” katika O. Babu (mh) *‘Kopo la Mwisho na Hadithi Nyingine’*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd. uk 157-168

Timammy, R. (2011). “Picha ya Hadaa” katika K. Walibora na P. I. Iribe Mwangi (wah) *‘Sina Zaidi na Hadithi Nyingine’*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd. uk 69-74

Timammy, R. (2011). “Thamani ya Mwanamke” katika C. Momanyi na R. Timammy (wah) *‘Takrima Nono na Hadithi Nyingine’* (uk 134-142). Nairobi: Longman.

Wachira, J. W. (2006). “Taswira ya Mwanamke kama Inavyojitokeza katika Nyimbo za Kisasa za Rap”. Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu, Kenyatta. (Haijachapishwa).

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* (uk 157)Nairobi: Focus Books.

Wandera, P. W. (2002). "Utafiti wa Maswala ya Kijinsia katika Kiswahili." Katika *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press.

Wegesa, B. B. N. (1996). "Mwanamke katika Tamthilia za Ebrahim Hussein," Tasnifu ya M. Phil. Chuo Kikuu, Moi. (Haijachapishwa).

Zakaria, Y. (2001). "Entrepreneurs at Home: Secluded Muslim Women and Hidden Economic Activities in Northern Nigeri". *Nordic Journal of African Studies*, 10(1), uk 107-123.